# UCHANGANUZI WA LUGHA NA ITIKADI ZA MAMLAKA YA KIJINSIA KATIKA NYIMBO ZA HARUSI KUTOKA JAMII YA WAKIKUYU WILAYA YA KIRINYAGA.

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY
19 SEP 2013
P.O. BOX 536
EGERTON
ACQUISITION SECTION

**KENNETH MAINA WAKIURU**

Tasnifu Hii Imewasilishwa Katika Shule ya Mafuzu Kwa ajili ya Kutimiza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili Katika Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Egerton.

**CHUO KIKUU CHA EGERTON**

**JUNI, 2013**

EULIB
041 022

## UNGAMO NA IDHINI

### UNGAMO

Ninaungama kwamba hii ni kazi yangu binafsi na haijawasilishwa katika chuo kikuu chochote.

Sahihi.............................................. Tarehe.....25-06-2013.....

**Kenneth Maina Wakiuru**

AM12/2326/09

### IDHINI

Tasnifu hii ya uzamili imewasilishwa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.

Sahihi.............................................. Tarehe.....25.6.2013.....

**Prof. James Ogola Onyango**

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi

Chuo Kikuu cha Egerton.

Sahihi.............................................. Tarehe.....25.06.13.....

**Dkt. Furaha Tchai**

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi

Chuo Kikuu cha Egerton.

# TABARUKU

Nachukua fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa Mungu Mwenyezi kwa kufanikisha kazi hii. Umenigharimu muda mwingi lakini kamwe hakuniacha pweke. Vilevile shukrani tele ziwaendee wasimamizi wangu wapendwa Prof. Onyango James na Dkt. Furaha Tchai kwa msaada na msaada bora walionipa. Kamwe hawakuvunjika moyo kunirekebisha na kunisahihishia kazi yangu. Sitasahau Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu kwa usaidizi walionipa. Kadhalika ni asante sana kwa Prof. Catherine Kitetu, Prof. Mutiti na Dkt. Wendo Nabea kwa motisha walionipa. Mungu azidi kuwakirimia hekima na busara tele.

Shukrani zaidi zimwendee mke wangu mpendwa Margaret Maina na mwanangu Marx Maina kwa mapenzi na uvumilivu tele kwa wasaa mwingi niliotengea kazi hii. Siwezi kusahau wazazi wangu, Mzee Jotham Maina na mamangu Susan Maina ambao kwao kiu ya masomo imekuwa ni dira inayowafanya kuwasukuma na kushajiisha wanao kuandama maarifa zaidi. Rambirambi za buriani zimwendee bibi yangu Bi. Wamaitha Maina ambaye alitazamia kuona hatima ya masomo haya ila hakujua kuwa Mungu alikuwa kapendezwa na roho yake. Ulikuwa ni wakati mgumu yeye kuaga nilipokuwa nikifanya mtihani wa kozi hii. Hata hivyo Mungu alinipa ukakamavu na nikafuzu mitihani yote.

Pongezi kwa Shule ya Upili ya Dadaab kwa msaada walionipa wa kutumia vifaa na malighafi ya shule. Nafasi njema walionipa ya kufanya kazi huku nikiendelea na masomo yangu ya Uzamili ni jambo adimu ambalo siwezi kuchukulia kwa mapuuza. Sitasahau Bw. Gerishon Kinyua na Bw. Jackson Kamau kwa maarifa yao na msaada walionipa kuhusiana na taaluma ya teknolojia na mawasiliano. Mungu awabariki.

Bila shaka siwezi kutaja watu wote ambao walichangia kufanikiwa kwa kazi hii. Niliosoma nao katika shahada hii Bw. Chris Kirui, Bi. Janice Mutua, Bi. Roseline Riroh na Bi. Beatrice Okere nawatakia kila la heri katika uwanda huu wa lugha ya Kiswahili. Mawaidha yenu na motisha mlionipa pamoja na muda tuliokaa kivulini tukijadiliana, vimekuwa ni rutuba ndani ya moyo wangu. Siwezi kuwasahau. Ningehimiza tukumbuke usemi wa Prof. Onyango kwamba tusiwe mburukenge katika msafara wa mamba.

# IKISIRI

Itikadi ni mfumo wa mawazo, kaida na thamani ambazo hutambulisha mfumo wa imani wa jamii. Itikadi hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia taasisi fulani za jamii. Lugha inayotumika katika nyimbo za harusi hubeba ujumbe ambao husheheni itikadi zinazotazamiwa kuongoza maisha ya watu. Hii ndiyo sababu ambayo ilichochea kufanywa kwa utafiti huu, ambao ulinuia kuchunguza lugha na itikadi zenye mamlaka ya kijinsia katika nyimbo za harusi za Kikuyu. Usemi uliohusu itikadi zenye mahusiano ya mamlaka ya kijisia katika jamii ya Wakikuyu ulihakikiwa kwa kina. Utafiti huu ulijikita katika jamii ya Wakikuyu ambayo imesheheni wilaya tano za kiutawala zinazochukuliwa kuwa ni himaya asilia ya Wakikuyu. Madhumuni ya utafiti yalikuwa ni kueleza sifa za lugha inayotumika katika nyimbo za harusi, kuchunguza jinsi itikadi zinavyoendelezwa kupitia nyimbo za harusi na kubainisha jinsi mamlaka ya kijinsia yanavyoendelezwa kupitia nyimbo za harusi za Kikuyu. Nyimbo zozote tano zinazoimbwa katika sherehe za harusi zilichanganuliwa ili kuchunguza athari za lugha katika kuendeleza mamlaka za kijinsia na itikadi. Kazi hii iliegemea katika nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi. Muundo wa kimaelezo wa utafiti ndio uliongoza utafiti huu, kisha uchanganuzi wa data kiuthamano ukafuata. Mbinu za utafiti zilizotumika ni kusoma maktabani na uchanganuzi wa usemi katika matini za nyimbo za harusi. Vyombo vya utafiti vilivyotumiwa ni kinasa sauti na kanda za kunasa sauti. Utafiti huu ulichanganua aina za maneno zitakazojitokeza katika matini za nyimbo za harusi za Kikuyu, kama vile: nomino, viwakilishi, vivumishi, vitenzi, sitiari, pamoja na maudhui ya nyimbo hizo. Uchunguzi ulibainisha kwamba lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za Kikuyu huwa na sifa maalum na huendeleza itikadi za mamlaka ya kijinsia kwa namna ya ushawishi sana. Utafiti huu utawanufaisha watafiti wa masuala ya kijamii, washauri katika masuala ya ndoa, wanasheria wanaohusika na kesi za ndoa, hata wasomi kuhusu masuala ya kijinsia, na vilevile watafiti wanaotumia nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi.

# ABSTRACT

Ideology is a system of ideas, principles and values that characterize the belief system of a community. Ideologies are passed on from one generation to another through varied institutions of the society. The language used in wedding songs conveys great messages that carry along ideologies perceived to govern the life of the people. This study set out to analyze language of gendered power ideologies, in Kikuyu wedding songs. The discourse surrounding ideologies of gendered power relations among the Kikuyu community was thoroughly analyzed. Ideally, the Kikuyu community entails five administrative districts which are the ancestral land from where the Kikuyu community is perceived to have originated. The study aimed at describing linguistics features that are comprised in Kikuyu wedding songs. It also aimed at analyzing how ideologies are propagated through Kikuyu wedding songs. Finally, it also aimed at finding out if gendered power ideologies are propagated using Kikuyu wedding songs. Five Kikuyu wedding songs were collected and treated as text for analysis to shed light on the effect of language in the promotion of gendered power and ideologies. The study was based on the theory of Critical Discourse Analysis (CDA). Descriptive research design was used followed by a qualitative analysis of data. The research methods used included library research and analysis of text in the Kikuyu wedding songs. The tools of data collection were tape recorder and audio visual cassettes. The research has scrutinized nouns, verbs, pronouns, adjectives, verbs, metaphors and themes pertaining marriage ideologies. The study showed that the language used in the Kikuyu wedding songs has distinct linguistics features and conveys gendered power ideologies that are passed on in a very persuasive or convincing way. The study will benefit researchers in social sciences, marriage counselors, law firms dealing with the marriage cases, scholars interested in gender issues, and also researchers using CDA theory.

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

# YALIYOMO


**UNGAMO NA IDHINI** .......... ii

**TABARUKU** .......... iii

**IKISIRI** .......... iv

**ABSTRACT** .......... v

**YALIYOMO** .......... vi

**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... ix

**RAMANI YA WILAYA YA KIRINYAGA** .......... x

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**

1.1 Usuli wa Mada .......... 1

1.2 Suala la Utafiti .......... 2

1.3 Madhumuni ya Utafiti .......... 2

1.4 Nadharia Tete .......... 2

1.5 Umuhimu wa Utafiti .......... 3

1.6 Upeo na Mipaka .......... 3

1.7 Maelezo ya Istilahi .......... 4

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI**

2.1 Utangulizi .......... 5

2.2 Mapitio ya Maandishi .......... 5

2.2.1 Dhana ya Itikadi .......... 5

2.2.2 Asili ya Tofauti ya Nafasi ya Wanaume na Wanawake katika Jamii .......... 5

2.2.3 Mahusiano ya Mwanamume na Mwanamke Yanavyoendelea .......... 6

2.2.4 Maandishi Kuhusu Itikadi za Kimamlaka katika Jamii ya Wakikuyu .......... 7

2.2.5 Tafiti Kuhusu Picha ya Mwanamume na Mwanamke Kulingana na Mahitaji ya Mila na Itikadi za Jamii .......... 10

2.2.6 Maandishi Kuhusu Nyimbo za Harusi .......... 13

2.3 Msingi wa Nadharia .......... 14

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI**

3.1 Utangulizi .......... 19

3.2 Mahali pa Utafiti .......... 19

3.3 Muundo wa Utafiti .......... 19

3.4 Uteuzi wa Sampuli....................19
3.5 Mbinu za Kukusanya Data....................20
3.6 Uchanganuzi wa Data....................20

**SURA YA NNE: MSINGI WA KIHISTORIA WA JAMII YA WAKIKUYU NA UBAINIFU WA ITIKADI ZA KIMAMLAKA KATIKA NYIMBO ZA HARUSI ZA KIKUYU KUTEGEMEA JINSIA**

4.1 Msingi wa Kihistoria wa Jamii ya Wakikuyu....................22
4.1.1 Utangulizi....................22
4.1.2 Asili ya Wakikuyu Kulingana na Visasili....................22
4.1.3 Asili ya Wakikuyu Kulingana na Ithibati ya Kihistoria....................25
4.1.4 Hali ya Kijamii ya Wakikuyu....................25
4.1.5 Hali ya Kisiasa ya Wakikuyu....................26
4.1.6 Hali ya Kichumi ya Wakikuyu....................27
4.1.7 Hali ya Maisha ya Kijamii ya Mkikuyu....................29
4.1.7.1 Desturi za Kuzaliwa kwa Mtoto....................29
4.1.7.2 Desturi za Ndoa....................33
4.2 Ubainifu wa Itikadi za Kimamlaka katika Nyimbo za Harusi za Kikuyu Kutegemea Jinsia....................37
4.2.1 Utangulizi....................37
4.2.2 Awamu ya Bwana Harusi Kufika Nyumbani kwa Bibi Harusi Kumchukua....................38
4.2.3 Awamu ya Kuungamanisha Bwana na Bibi Harusi....................41
4.2.4 Awamu ya Kusherehekea Bw. na Bi. Harusi kufanya Ndoa....................44
4.2.5 Awamu ya Kutoa Ushauri kwa Bw. na Bi. Harusi....................46
4.2.6 Awamu ya kutoa Zawadi kwa Bw. na Bi. Harusi....................49
4.3 Muhtasari wa Uchanganuzi Huu....................53
4.3.1 Lugha....................53
4.3.2 Maudhui....................57
4.3.3 Maana....................58

**SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

5.1 Utangulizi....................60
5.2 Hitimisho....................60
5.3 Changamoto zilizomkabili mtafiti....................62

5.4 Mapendekezo......62
**MAREJELEO**......64
**VIAMBATISHO (Nyimbo mbalimbali za harusi)**......67


**ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali 1: Njia tatu za kufanya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi.....................................16

Jedwali 2: Istilahi za lugha zilizotumiwa katika nyimbo za harusi za Kikuyu......................54

Jedwali 3: Tofauti baina ya mwanamume na mwanamke inayojitokeza katika nyimbo za harusi za Kikuyu..................................................................................57

**RAMANI YA WILAYA YA KIRINYAGA AMBAKO UTAFITI ULIFANYWA.**




**Source: Kirinyaga District Development Plan 1997 - 2001**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Nyimbo ni sehemu ya lugha ambayo hutumiwa kuburudisha, kuyatafakari, kuyapima maisha na kufunzia jamii. Nyimbo za harusi kwa hiyo sio tu hutumika kuburudisha watu bali pia hutumika kufunza maadili ya kijamii na itikadi zao. Kulingana na Wandera (1996) hakuna fasihi yoyote ambayo imechipuka na kuendelea kuishi katika ombwe tupu. Fasihi yoyote (nyimbo za harusi zikiwemo) hupata uhai wake na maudhui kutoka kwa jamii inayoichipuza. Mamlaka na itikadi ni mojawapo wa maswala ya kitamaduni yanayorithishwa kupitia kwa kitendo cha ujamiishaji kinachohalalishwa na kuendelezwa na asasi mbalimbali za kijamii kama vile ndoa/harusi kupitia kwa nyimbo, ngano, methali, vichekesho na kadhalika.

Kumekuwa na mikakati ya kitaifa na kimataifa ya kushughulikia maswala ya kijinsia na hasa kuhusu nafasi ya mwanamke. Hali ambayo haijabadilika sana hata leo hii. Chomba (2005), Collins (1991) na Eagleton (1996) ni wasomi ambao tafiti zao zinaegemea sana Ufeministi na zinaonekana kutosababisha mabadiliko sana kwa sababu huwa zinamwangazia mwanamke kama ambaye daima anateswa na mwanamume. Hazionyeshi ni sehemu gani ambazo mwanamke anakuwa na mamlaka ya kuamua mambo. Ni tafiti zinazotumia sana nadharia na mitazamo ya uelemea kike. Tatizo linaloibuka ni kwamba wanaoshikilia sana mikabala ya Ufeministi wanamsawiri mwanamume daima kwa ukatili na mwenye dhuluma kwa mwanamke. Wakati mwingine baadhi ya wanaoshikilia mikabala hii ya kifeministi hudai kuwa wanawake wanaweza kuishi bila kumtegemea mwanamume na hata kutoshelezana katika maswala ya ndoa. Hili linaashiria umuhimu wa kushughulikia suala hili, yaani kuondoa mvutano baina ya mitazamo kuhusu mwanamke na mwanaume. Ni utafiti ambao umechunguza jinsi lugha inavyotumika kueleza itikadi za kijamii na kufanya makundi fulani ya jamii kuonekana kana kwamba yamepewa umuhimu zaidi kuliko mengine. Ni katika kuchunguza matumizi ya lugha ambapo matatizo ya kijamii yanaweza kusuluhishwa hasa yanayohusu mume na mke na kuwafanya waishi kwa kukubaliana na kuelewana.

Halliday (1978) anasema kwamba mtoto anapojifunza lugha huwa pia anajijengea taswira ya uhalisia unaomzunguka. Nyimbo za harusi kama chombo cha ujamiishaji kinachotumia lugha kama msimbo wa kupitisha ujumbe wake, huakisi kwa kiwango fulani hali ya maisha ya

wanajamii. Lugha vilevile hutumika kama ishara ya kufasiria mifumo na miktadha ya kijamii na kiutamaduni. Kama anavyosema Kenyatta (1978) mtoto huishia kujifunza majukumu yake yaliyoainishwa na jamii na kulingana na uana wake.

Ni muhimu kuchunguza kwa kina amali hizi zinazopitishwa kama mirathi katika kuona jinsi mamlaka na itikadi zilivyozuliwa na zitakavyojitokeza katika nyimbo za harusi. Utafiti huu ulichunguza hali hiyo katika nyimbo za harusi za Wakikuyu kwa uhakiki katika kuonyesha itikadi za kimamlaka katika hali halisi ya Wakikuyu, na kubainisha jinsi itikadi hizo zinavyoathiri maisha ya mwanamke na mwanamume.

## 1.2 Suala la Utafiti

Katika kushughulikia maswala ya kijinsia, tafiti nyingi zilizofanywa kitaifa na kimataifa, kama vile Chomba (2005), Collins (1991) na Eagleton (1996), zinaegemea kudhirisha jinsi mwanamke anavyodunishwa katika tamaduni nyingi zilizo na itikadi za kiume. Hata hivyo, suala la itikadi za kimamlaka kukuzwa, kuhalalishwa na kuendelezwa katika jamii ya Wakikuyu kupitia kizazi kimoja hadi kingine kupitia nyimbo za harusi bado halijafanyiwa uchanganuzi hakiki. Suala hilo linapelekea kuwepo migogoro ya kijinsia kuhusiana na mamlaka yanayoibuliwa na itikadi. Utafiti huu ulichunguza kwa uhakiki lugha na itikadi za kimamlaka kwa misingi ya kijinsia katika nyimbo za harusi kutoka jamii ya Wakikuyu.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

(i) Kueleza sifa za lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za Kikuyu.

(ii) Kuchunguza jinsi itikadi zinavyoendelezwa kupitia nyimbo za harusi za Kikuyu.

(iii) Kubainisha jinsi mamlaka ya kijinsia yanavyoendelezwa kupitia nyimbo za harusi za Kikuyu.

## 1.4 Nadharia Tete za Utafiti

(i) Lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za Kikuyu ina sifa maalum.

(ii) Nyimbo za harusi za Kikuyu huendeleza itikadi katika jamii ya Wakikuyu.

(iii) Nyimbo za harusi za Kikuyu huendeleza mamlaka ya kijinsia.

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika uchunguzi wa kiisimu wa itikadi za kimamlaka ya kijinsia katika juhudi za kufafanua lugha inayotumika katika nyimbo za harusi katika jamii ya Wakikuyu. Matokeo ya utafiti huu yatakuwa ya manufaa kwa watafiti wa maswala ya kijamii, washauri katika maswala ya ndoa na hata wanasheria wanaohusika na kesi za ndoa. Aidha utawanufaisha wasomi wanaotafiti kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi na wanaojihusisha na maswala ya umenke katika jamii.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu uliangazia nyimbo tano za harusi katika jamii ya Wakikuyu ili kuangazia jinsi lugha inavyotumika kuendeleza itikadi zenye mamlaka ya kijinsia. Shughuli za ndoa ziko katika msambao unaoanzia wakati wa kulipa mahari hadi wakati mwanamke anapokabidhiwa mumewe na wazazi wake katika tukio la harusi. Siku ya harusi huwa ni kilele cha shughuli zilizochukua siku nyingi kukamilika. Hivyo basi data kutoka kwa nyimbo tano katika awamu tofauti za harusi inaweza kuwakilisha kikamilifu masuala yanayohusiana na mamlaka ya kijinsia hasa inapofanyiwa uchanganuzi hakiki. Lugha iliyotumiwa ilikabiliwa kwa kuangazia nomino, viwakilishi, vitenzi, sitiari, tashbihi na maudhui katika nyimbo za harusi. Data ya nyimbo za harusi ilikusanywa kutoka kwa fanani ambao ni gwiji katika kuongoza nyimbo hizo, kwenye tukio la harusi. Utafiti huu ulifanywa katika Wilaya ya Kirinyaga.

## 1.7 Maelezo ya Istilahi

Desturi – jambo ambalo mtu hulifanya kama kawaida: tabia, hulka, mazoea, ada au kaida.

Fanani – ni mtu mwenye maarifa na ujuzi wa kuongoza nyimbo.

Itikadi – ni mfumo wa mawazo, kaida na thamani ambazo hutambulisha na kuwaongoza wanajamii katika kufanya maamuzi yanayohusu amali na hali mbalimbali anazokumbana nazo mwanajamii katika maisha.

Jamii – kundi la watu maalum wanaotofautiana na makundi mengine kwa misingi ya lugha, desturi na mila.

Jinsia / uana – hali ya kuwa mwanamume au mwanamke kimaumbile; kigezo kinachotumiwa kugawa majukumu katika jamii.

Mdahalo – usemi ambao unaweza kuwa ama umetamkwa au uko katika maandishi.

Mamlaka – uwezo ambao unaweza kutwikwa mtu au kundi fulani ili liweze kudhibiti masuala yanayohusu kundi hilo.

Mila – mambo yafanywayo na jamii ya watu kwa mujibu wa asili na utamaduni wao.

Ubabeume – mfumo wa kijamii unaozingatia itikadi ya kuumeni. Itikadi ambayo huchukulia amali za kiume na mawazo yao kuwa kaida za kufuatwa katika jamii nzima.

Utamaduni – maisha ya kawaida ya watu husika; mazoea yao kama vile dini, mila siasa na mfumo wa kiuchumi (Wandera 1996).

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti anaangazia maandishi ya wasomi mbalimbali pamoja na tafiti zilizofanywa kuhusiana na mada hii. Inamulika kuzuka kwa itikadi tofauti kuhusu mwanaume na mwanamke, itikadi hizo katika jamii ya Wakikuyu, mahusiano ya mwanamume na mwanamke yanavyoendelea, tafiti mbalimbali kuhusu picha ya mwanamume na mwanamke katika jamii tofauti tofauti. Vilevile, inaangazia kuhusu msingi wa nadharia inayoongoza utafiti huu.

## 2.2 Mapitio ya Maandishi

### 2.2.1 Dhana ya Itikadi

Kwa manufaa ya utafiti huu mchango wa Destult utakuwa muhimu kufafanua dhana hii ya itikadi. Destutt de Tracy (1806) aliona itikadi kama sayansi ya mawazo ambayo alitazamia ingebainisha matendo ya kiakili ya watu wanayofanya bila kudhamiria. Vilevile humaanisha tabia za kiakili kama vile imani, matamanio na madhanio ambayo huelekezwa kwa ulimwengu ili kuupa muundo na maana ambazo huongoza shughuli zetu za kisiasa na kijamii. Wodak (1989) anasema katika jamii ya kisasa mamlaka hudhihirishwa kwa namna ya kidemokrasia ambapo kimsingi hailazimishwi, bali ni kwa namna ya kushawishi – ambayo ni itikadi. Itikadi hizi za kimamlaka ambazo zinadhihirishiwa jamii kukubali kwa namna ya ushawishi ndizo zilikuwa msingi wa kuchunguzwa katika nyimbo za harusi za Kikuyu.

### 2.2.2 Asili ya Tofauti ya Nafasi ya Wanaume na Wanawake Katika Jamii

Kulingana na Engels (1975) mwanamume na mwanamke walikuwa sawa hadi pale palipotokea migawanyiko ya kitabaka. Ingawa habainishi wazi wakati maalum wa migawanyiko hii ya kitabaka kutokea, anadai kwamba, katika enzi hizo wanajamii walikuwa wakiishi maisha ya ujima. Jamii hizi zilibadilika na kuanza kuwa na ustaarabu. Huu ndio wakati ubabeume ulianza kutawala mahusiano yote ya jamii (Makori 2008). Kuanzia kwa mfumo huo ni wakati kazi za wanaume kama vile usasi na ufugaji zilianza kuleta faida kuliko zile za wanawake za nyumbani. Hali hii iliwafanya wanaume kuanza kuwa na ubinafsi uliosababisha hali ya kurundika umuhimu kwa shughuli zote zilizokuwa na uhusiano na mwanamume. Kulingana na

Engels, huu ndio ulikuwa mwanzo wa wanawake kutegemea wanaume kiuchumi. Kulingana na hali hiyo, itikadi ya mwanamume kuchukuliwa kama mtu wa hadhi ya juu katika jamii ikaanza.

Kutokana na maoni hayo ya Engels, mtafiti alipata mshawasha wa kutaka kujua iwapo hali hii inajitokeza miongoni mwa Wakikuyu kupitia kwa nyimbo za harusi. Hamu zaidi kwa mtafiti inatokana na ukweli kwamba jamii hii inajihusisha na shughuli za ufugaji kama ilivyo katika jamii aliyokuwa akizungumzia Engels. Kazi ya utafiti huu ilijihusisha na kutambulisha jinsi lugha inavyotumika kujenga na kuendeleza itikadi na mamlaka katika ndoa baina ya mume na mke.

### 2.2.3 Mahusiano ya Mwanamume na Mwanamke Yanavyoendelea.

Utafiti uliofanywa na taasisi ya Marekani inayoshughulika na masuala ya mahusiano, *Relation Institute,* imedhihirisha kwamba wanaume na wanawake kwa jumla huzungumzia mtoto mvulana kwa sauti nzito, kavu na yenye kufoka, huku wakimzungumzia mtoto msichana kwa upole na ubembelezi. Wanaeleza kwamba wavulana hurejelewa kwa kuamrishwa na hutakiwa kufanya kazi zinazohitaji nguvu pia hawahitajiki kudhihirisha hisia za uchungu au maumivu. Kwa upande mwingine wasichana huwa ni wa kuonewa huruma na wazazi ambao huonyesha hisia nyingi msichana anapopatwa na machungu.

Wavulana huhitajika kuonyesha ukakamavu kwa kutolia na anayeonyesha kulia hukemewa na kulinganishwa na mwanamke. Wavulana huhitajika kutokuwa na woga katika kupambana na kazi yoyote, kudhihirisha ujasiri na kutoshindwa. Wasichana hudhaniwa kuwa wanyonge na hivyo kuachiwa kazi zinazoonekana laini kama vile: kupika, kutunza nyumba, kufua nguo, kushona na kadhalika.

Kwa miaka ya karne na ishirini na moja ambapo jamii imekubali kuelimisha wavulana na wasichana, bado tabia zinazotofautiana zinaendelea kudhihirika baina yao. Wasichana hupendelea kuzungumza kuhusu watu wengine, kuhifadhi siri zinazodumisha urafiki wao na kupenda kusema matamanio na mahitaji yao. Wavulana nao hupenda kuzungumza kuhusu vitu au vifaa na shughuli tofauti tofauti. Hupenda kuona wanachangia vipi na ni nani mzuri katika tendo fulani miongoni mwao.

Katika maisha ya ukubwani wanawake huzungumza kuhusu mada zinazohusu mahusiano, watu, lishe bora, mavazi na maumbo yao yanavyoonekana. Nao wanaume hupenda

kuzungumza mada zinazohusu michezo, kazi, pesa, magari, habari, siasa na utendaji-kazi wa vifaa vya kimekaniki.

Kwa ujumla, wanaume hujihisi kujivunia kibinafsi wanapofanikiwa katika jambo fulani. Kufanikiwa katika jambo ni ishara ya uwezo, mamlaka na kujimudu katika nafsi ya mwanamume. Wanaume hupenda kujihusisha na vitu na mambo wala sio kujihusisha na watu na hisia zao. Ni vigumu wanaume kusema kuhusu shida zao isipokuwa kwa mtaalam – wanapotaka ushauri wake. Kutaka msaada wakati anaweza kufanya kitu huonekana kama ishara ya udhaifu. Wanaume hudhihirisha ukali, kupenda kupambana na kulinda. Mwanamume hupata fahari anapotia fora katika kazi na masomo. Kinachovunja mwanamume moyo ni kufeli na kupungukiwa na fedha.

Kwa upande mwingine wanawake huthamini sana mapenzi/kupendwa, mawasiliano, urembo na mahusiano. Nafsi ya mwanamke hukamilika kupitia hisia na thamani ya mahusiano yao. Wao hutumia muda mwingi kushajiishana, kusaidiana na kushirikiana kupitia kuhusiana. Utambulisho kwa mwanamke huwa ni muhimu sana hasa anapojidhihirisha kupitia mavazi, mawasiliano na wengine, anavyozungumza na kushirikiana na wengine humfanya ajihisi mkamilifu. Kulingana na wanawake, kusaidia sio ishara ya udhaifu bali ni kudhihirisha kujali na moyo wa kusaidia. Mwanamke hupenda kutunza sana hadhi yake kama anavyoonekana.

Matatizo yanayozuka kati ya mwanamume na mwanamke yanaelekea katika kulaumiana; kila jinsia ikiilaumu nyingine. Mathalan wanaume hudai kuwa kila mara wanawake hutaka kubadilisha wanaume. Nao wanawake hukiri kwamba kila wakati wanaume hawawasikilizi. Hili ndilo huwa chanzo kuu cha kung'ang'ania mamlaka. Kwani mwanamke anapojaribu kumbadilisha mwanamume au anapotaka kumshauri mwanamume, mwanamume huhisi anaonekana asiyejiweza au asiye na mamlaka juu ya jambo fulani. Matatizo hayo ndiyo ambayo utafiti huu ulikuwa ukichunguza ikiwa yanajitokeza kupitia nyimbo za harusi za Kikuyu.

### 2.2.4 Maandishi Kuhusu Itikadi za Kimamlaka Katika Jamii ya Wakikuyu

Bottignole (1984:32) anasema kwamba lilikuwa jukumu la mama kufunza wanawe wa kike majukumu ya ndoa naye baba akifunza wanawe wa kiume. Anaendelea kutaja kwamba shughuli ya biashara ilihusu wanaume na wanawake, ambapo wanawake walibadilishana nafaka na mboga nao wanaume wakibadilishana ng'ombe, mbuzi na kondoo. Hata hivyo, ubadilishanaji wa mifugo ulifanywa kwa makini sana kwani ulikuwa sio tu kigezo cha utajiri bali mifugo hao

walitumika wakati wa kutoa mahari kwa wazazi wa msichana anayeolewa. Utafiti huu unaonyesha jinsi nyimbo za harusi za Kikuyu zinavyobainisha itikadi na mamlaka ya mwanamume na yale ya mwanamke na kueleza ni kwa nini yakagawanywa jinsi hiyo.

Aidha, Bottignole (ibid) anaendelea kueleza kwamba, hata ingawa taadhima kubwa ilipewa mwanamke Mkikuyu kwa jukumu lake la uzazi na kuelimisha, utamaduni haukumpa nafasi ya usemaji katika hafla za umma hasa suala la siasa, ambalo lilikuwa ni la wanaume ambao waliwakilisha makundi ya familia zao. Utafiti huu unabainisha itikadi za kisiasa / utawala zinazobainika kupitia nyimbo za harusi za Kikuyu.

Dutto (1975:121) anasema kwamba uhusiano baina ya wanaume na wake wao huwakilisha dhana nyingi zinazotofautiana kulingana na misingi ya watu kama eneo mtu anakotoka, umri, tofauti za kibinafsi na uteuzi wa mtu binafsi. Miungano inayounganisha wanaume na wake wao huelekea kuwa changamano na yenye usiri. Katika uchunguzi wake huko Nyeri, anatoa maoni ya mwanamke aliyesoma, kama kiwakilishi cha itikadi wanazoshikilia wanawake walio katika ndoa kuhusu wanaume Wakikuyu (uk 121).

> "Watu ambao ni changamano sana kwetu kujua ni wanaume wetu. Wanaume Wakikuyu kwa ujumla huwa hawajali kueleza mambo kwa wake wao. Hili pengine ni kutokana na mawazo yao na jinsi wanavyomchukulia mwanamke. Neno 'upungufu' halifai sana, lakini kwa hakika matamanio ya mwanamke huonekana tofauti na ya mwanamume. Mwanamke yuko hapo tu; hahitajiki kueleweka au kuelezwa mambo….Wakati mwanamume anafanya makosa, hawezi kukubali kwamba makosa hayo ni yake, hata kama yako wazi kwa mtoto. Mke ndiye wa kulaumiwa….Wakati wanaume wanazungumza pamoja, hasa wazee, wanawake wanafaa kukaa kando kimya. Ikiwa mwanamke atajaribu kusema neno, ataulizwa – "kwa nini unaongea wakati watu wengine wanazungumza?" Mielekeo hii hudhihirishiwa wavulana walio kwenye umri mdogo. Mvulana anapofanya kosa, yeye hukemewa na kuulizwa, kwa nini anafanya hivyo kama mwanamke. Kwa hivyo wavulana hukua wakiwa na mielekeo hiyo." (tafsiri yangu)

Kwa upande mwingine, Dutto (ibid) anatoa maoni ya mwanamume wa zaidi ya miaka 30 ambaye pia ameoa kudhihirisha itikadi walizo nazo wanaume kuhusu wake wao. Anasema:

> "Huwezi kumwamini mwanamke. Unapomwambia mambo mengi, atayasimulia yote kwa rafiki zake, na kabla hujatambua, utajipata mashakani."( tafsiri yangu)

Utafiti huu ulichunguza iwapo itikadi hizo ambazo anabainisha Dutto zinajitokeza katika lugha inayotumika katika nyimbo za harusi katika jamii hiyo hiyo ya Wakikuyu aliyochunguza, ingawa utafiti wake ulijikita mjini Nyeri.

Kenyatta (1978:3-20) anasema kwamba itikadi zinatokana na desturi kuu ya utamaduni wa Kikuyu, kwamba jukumu kubwa la mwanamke ni la nyumbani. Anasisitiza kwamba jukumu la mwanamke Mkikuyu katika nyumba ni la umuhimu mkubwa. Anaendelea kueleza, nyumba ni kiungo muhimu cha maisha ya kila siku, na wakati mwanamke ako kwa nyumba, yeye ndiye mwenye nyumba. Kukomelea hoja hiyo zaidi, Dutto (1975:122) anamnukuu mwanamume mmoja wa umri wa makamo anayesema kwamba, "Mwanamke mzuri hagombani wala kupigana na wanawake wengine. Hapotezi muda wake. Yeye hupika chakula cha familia yake cha kuwatosheleza. Yeye ndiye huosha, kufanya kazi zote za nyumbani na zaidi ya hayo yeye ndiye mama na mlezi wa watoto." Maoni ya Kenyatta na utafiti huo wa Dutto ni msingi bora wa kutathmini itikadi ya mamlaka ambayo yamepewa mwanamke iwapo yanajitokeza katika nyimbo za harusi za Kikuyu.

Itikadi nyingine ni kwamba mwanamke Mkikuyu anajulikana kufanya kazi hadi umri wa uzeeni (Kenyatta 1978:18). Anaeleza kwamba, wanaume na wanawake wengi hukubali kwamba "mwanamke mzuri ni mwanamke anayejiweza ('*Mutumia mwihoti*'). Yaani ni mwanamke ambaye ana uvumilivu mwingi na mwenye siha nzuri na hupenda kusisitiza kwamba ana nguvu hata kuliko mwanamume. Wanawake hawa ndio huona fahari kutaja kwamba, "wanaume hawana nguvu kama walizo nazo wanawake. Wanaume hawawezi kubeba mizigo mizito. Wanawake Wakikuyu wana nguvu nyingi." Itikadi hiyo kama inavyobainishwa na Kenyatta, ilichunguzwa iwapo inajitokeza katika nyimbo za harusi za Kikuyu.

Japo ndoa katika jamii ya Wakikuyu imeathirika sana na dini, hasa ya Kikristo, bado kuna itikadi nyingi za kiutamaduni zinazopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kama inavyobainika kupitia ulipaji wa mahari. Itikadi ya mwanamume mmoja kuwa na wake wengi ni mojawapo ya zile itikadi ambazo zinazidi kufifia kabisa katika jamii ya Wakikuyu. Hata hivyo, kulingana na utafiti uliofanywa na Dutto (1975:123) huko Nyeri, anasema kwamba wanawake wengi walioolewa ni waaminifu kwa waume wao, lakini wanaume wengi huwa na uhusiano nje ya ndoa. Utafiti huu ulichunguza ikiwa itikadi kuhusu uaminifu inajitokeza katika nyimbo za

harusi na kubainisha iwapo lugha inayotumika katika nyimbo hizo inashajiisha mwanamume kuwa na uhusiano nje ya ndoa.

### 2.2.5 Tafiti Kuhusu Picha ya Mwanamume na Mwanamke Kulingana na Mahitaji ya Mila na Itikadi za Jamii.

Tafiti nyingi za miaka ya thelathini na tisini, zimeonyesha kwa ujumla majukumu ya mwanamke na mwanamume na kusisitiza kuwa mwanamke ananyanyaswa au kukandamizwa katika jamii nyingi za kiafrika. Hata hivyo tofauti hizi zinamulika kauli ya mwanamume kwa mkabala hasi. Kwa kutumia mielekeo ya kike na nadharia zinazoegemea upande wa kike, tafiti nyingi zinakashifu sana mamlaka na majukumu ya mwanamume wanayobainisha. Tatizo ni kwamba tafiti hizi hazionyeshi jinsi migogoro ya itikadi na mamlaka baina ya mwanamke na mwanamume inavyoweza kusuluhishwa. Baadhi ya tafiti hizo ni kama zifuatazo:

Mbiti (1969) anabainisha jinsi migawo ya majukumu katika jamii nyingi za Kenya ilivyoamuliwa na utamanduni wa jamii husika. Katika itikadi ya utawala anadai kwamba maswala mengi ya jamii yaliongozwa na kutatuliwa na baraza la wazee katika mahakama za kijadi. Anasisitiza kwamba, mabaraza haya yalikuwa yakiongozwa na wanaume. Anakiri eti kutokana na mabaraza hayo, mwanamume alitakiwa kudhihirisha ushujaa daima. Itikadi hiyo ilichunguzwa katika utafiti huu, kubainisha iwapo inajitokeza katika lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za Kikuyu.

Materu (1982) anaeleza kwamba wanaume wanadunisha wanawake katika hadithi fupi. Anaendelea kueleza kuwa wanaume huwaona wanawake kama vyombo vya kumalizia uchu wao na vifaa vya kufanya kazi ya sulubu. Ingawa kazi za hadithi fupi ni za kubuni na huenda maudhui yake yadhihirishe matendo ya jamii, maoni hayo yanaweza kuwa muhimu katika kuchunguza iwapo itikadi hiyo inabainika katika lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za Kikuyu.

Mbughuni (1982) aliandika makala kuhusu picha ya mwanamke katika maandishi ya kiriwaya ya Tanzania. Anasema kwamba, taswira inayoendelezwa kupitia kwa riwaya ni ile inayomwonyesha mwanamke kama mlaghai na mhalifu katika jamii. Anatumia mhusika Hawa kwenye Biblia kama kielelezo mwafaka cha mwanamke. Maoni hayo ya Mbughuni yanaonyesha itikadi ambayo inaegemea upande mmoja pasipo kuonyesha hali ya mwanamume. Hata hivyo

utafiti huu ulichunguza ikiwa itikadi za kihalifu na kilaghai kuhusu mwanamke zinajitokeza kupitia lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za Kikuyu.

Senkoro (1982) alichunguza wahusika wa kike katika riwaya ya Kezilahabi – Dunia Uwanja wa Fujo. Ingawa ni kazi ya fasihi, anasema kuwa itikadi katika mfumo wa kibepari, imembidhaaisha mwanamke na kumwonyesha kama kiumbe duni ambaye jukumu lake liko jikoni na kitandani. Utafiti huu ulichunguza lugha inavyotumika kubainisha majukumu haya katika mfumo wa ndoa kupitia nyimbo za harusi za Kikuyu, wala sio katika mfumo wa kiutawala na kiuchumi wa kibepari aliouchunguza Senkoro.

Kipury (1983) akirejelea jamii ya wamaasai anasema kuwa wanaume waliwatumia wanawake katika kazi nyingi huku wao wakifanya kazi chache. Anabainisha kazi ambazo zilikuwa zimetengewa wanawake kama kujenga nyumba, kutafuta kuni, kuteka maji, kukamua ng'ombe, kutayarisha chakula, kunadhifisha nyumba na maboma ya mifugo, pamoja na kulea watoto. Anaendela kueleza kwamba, ingawa kazi ya kulisha mifugo ni ya mwanamume, mara kwa mara wanawake waliulizwa kusaidia. Utafiti huu wa Kipury, unaegemea sana kubainisha majukumu ya mwanamke wa Kimaasai. Aidha habainishi majukumu ambayo yalitengewa wanaume wakati mwanamke anatekeleza hayo yote. Hata hivyo utafiti huo ulikuwa na umuhimu katika kubainisha mamlaka na itikadi zinazojitokeza katika nyimbo za harusi za Kikuyu.

Chesaina (1987) akitafiti kuhusu uwakilishi na majukumu ya wanawake katika michezo ya kiafrika ya uigizaji, anakubaliana na Abdulaziz (1979) kwamba wanaume huwapa wanawake majukumu yanayowafanya kuwagandamiza ili wajinufaishe wenyewe. Maoni hayo ya Chesaina na Abdulaziz ni msingi mzuri wa kuelewa nafasi ya wanaume na wanawake katika suala la kazi zinazotekelezwa kama ambavyo utafiti huu ulinuia kubainisha kupitia nyimbo za harusi za Kikuyu.

Kerre (1989) anasema kuwa katika jamii nyingi za kiafrika mwanamume ndiye anayetambulika kama kiongozi na mlinzi wa jamii. Aidha anaendelea kutaja kuwa kazi za kujenga nyumba na kutayarisha mashamba zilikuwa za mwanamume. Anasisitiza kuwa hata michezo ambayo watoto wa kiume walishiriki ilihusu ujenzi wa nyumba na maswala ya vita. Maoni haya Kerre yana uhusiano na utafiti huu. Anazungumzia kuhusu jamii nyingi za kiafrika, Wakikuyu wakiwemo. Kutokana na hali hiyo mtafiti alitaka kuona ikiwa lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za Kikuyu itadhihirisha itikadi hiyo.

Mule (1991) anashughulikia picha ya mwanamke kama inavyojitokeza katika tamthilia za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wa kike - Ali Katini Mwachofi na Sheila Ali Ryanga kutoka Kenya na Peninah Muhando na Anjelina Chogo kutoka Tanzania. Anaonyesha eti kuwa wanawake wamepewa kazi za nyumbani na ulezi, ambazo ziliwazuia kuwa na muda mwingi wa kusoma sawa na wanaume. Utafiti huu ulibainisha itikadi zinazohusu majukumu ya mwanamume na mwanamke katika nyimbo za harusi za Kikuyu.

Okindo (1995) anaangalia kuhusu picha ya mwanamke katika methali za Ekegusii. Anasema kuwa methali nyingi za Kikisii zinasisitizia mwanamke kuwa mtiifu na mwenye tabia njema ili hata atakapoolewa awe mtu wa kutegemewa. Vilevile anabainisha kuwa mwanamke ni mwenye kuhitaji kulindwa. Utafiti huu ulichunguza iwapo lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za Kikuyu inadhihirisha itikadi zinazohusiana na maadili au masuala kuhusu ulinzi kwa mwanamke.

Okindo (1995:15) anamnukuu Lugano (1989) anayehakiki usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya nne za Kezilahabi. Anatumia nadharia ya kifeministi na anadai kuwa Kezilahabi anaendeleza falsafa ya jamii kogwe kuhusu mwanamke, inayochukulia mwanamke kuwa kiumbe duni na aliyekuwa chini ya utawala wa mwanamume. Ingawa kazi ya Lugano inaegemea upande mmoja wenye mtazamo wa Uelemea Kike, utafiti huu ulitumia nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi na kubainisha jinsi lugha inavyotumika dhidi ya itikadi za mwanamume na mwanamke katika nyimbo za Kikuyu.

Wandera (1996) alichunguza usawiri wa mwanamke katika ushairi wa Kiswahili wa karne ya 1800 hadi 1900. Katika utafiti huo anasema kwamba picha ya mwanamke Mswahili imejengwa na mielekeo ya utamaduni wa wakati huo. Anasema kwamba utamaduni huo haukuwa wa kugandamiza mwanamke wala mwanamume, bali ulitenganisha majukumu na nafasi ya kila mmoja kwa misingi ya vigezo vya uana, maumbile, sheria ya dini ya Kiislamu, mila, siasa na mfumo wa kiuchumi. Utafiti huo wa Wandera ulikuwa na nafasi kubwa katika utafiti huu ambao ulichunguza itikadi zinazohusiana na nyanja hizo kwa kila mwanamume na mwanamke katika lugha inayotumika kwenye nyimbo za harusi za Kikuyu.

Maclenness (1998) anabainisha jinsi masharti ya kihistoria na ya kitamaduni yanavyohalalisha mielekeo na mitazamo tofauti ya kijinsia (katika Makori 2008). Anasema kuwa ubabe hauwezi kubainishwa kama sifa ya mwanaume, bali hutokana na itikadi na utamaduni wa jamii husika. Itikadi maalum za kihistoria zinazodhibiti imani za mume na mke katika jamii ni

majukumu yao. Kama anavyosisitiza Richmond (1992), jamii ni taasisi muhimu sana inayojenga na kuratibu majukumu na shughuli za kijamii kiuana. Maoni ya Macleness na Richmond yalikuwa nguzo muhimu katika utafiti huu katika kuchunguza iwapo lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za Kikuyu inabainisha itikadi na mamlaka kutegemea jinsia.

Chomba (2005) anachunguza usawiri wa mwanamke katika methali za kikuyu. Kwa kutumia nadharia ya Uelemea kike Hakiki / kifeministi, anadhihirisha kuwa mwanamke mkikuyu ananyanyaswa na kutwezwa na mwanamume. Katika kutetea mwanamke anatoa picha ya mwanamume ambaye hajali mwanamke. Tofauti na utafiti wake Chomba, utafiti huu ulitumia nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ambayo huchanganua hali zozote zinazohusika bila kuwa na mtazamo hasi kuhusu upande wowote. Kwa hivyo matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha itikadi zote kuhusu mwanamume na mwanamke Mkikuyu na kuonyesha nafasi ya lugha katika kujenga na kuendeleza itikadi hizo kupitia nyimbo za harusi.

Makori (2008:13) anasema uwezo wa wanaume hujikita katika misingi ya kibaolojia na mielekeo, imani na matarajio ya utamaduni wa jamii. Ananukuu Izugbara (2005) anayesema kuwa sura ya mwanamume hujengwa kutokana na matarajio ya itikadi na utamaduni husika. Kulingana na West na Rhoda (1990) uume katika mwanamume ulionekana katika misingi huru ya kijinsia, ushindani, ushari, uwezo wa kuongoza, kuamuru na kuzuia. Hivyo basi katika jamii nyingi za kiafrika kuna itikadi kuwa mwanamume huhusishwa na uwezo na ufanisi wa kukimu na kutosheleza mahitaji ya familia. Maoni hayo ya Makori na Izugbara ni muhimu sana kwa utafiti huu katika kubainisha iwapo lugha inayotumiwa katika nyimbo za harusi za Kikuyu inabainisha mamlaka ya kiuwezo baina ya mwanamume na mwanamke.

### 2.2.6 Maandishi Kuhusu Nyimbo za Harusi

Timammy (2002) alifanya uhakiki wa mbinu za lugha katika nyimbo za harusi za Kiswahili huko Mombasa. Utafiti wake uliangazia matumizi ya mbinu za lugha kama zinavyojitokeza katika nyimbo za harusi. Mbinu hizo ni kama tashbihi, jazanda, nahau methali na mafumbo. Tofauti na 'utafiti wa Timammy, utafiti huu ulilenga kuhakiki jinsi lugha inavyotumika kujenga na kuendeleza itikadi za kimamlaka katika nyimbo za harusi za Kikuyu.

## 2.3 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu utaongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi (*Critical Discourse Analysis – CDA*) inayodokeza kwamba mdahalo na jamii hutegemeana na kujengana. Vilevile usemi huweza kufungamana na muktadha wa kihistoria. Hii inamaanisha kwamba, usemi hautolewi bila muktadha na vivyo hivyo hauwezi kueleweka bila kutilia maanani muktadha wa kitamaduni. Aidha usemi hufanya kazi ya itikadi. Itikadi ni jinsi fulani ya kuwakilisha na kupanga jamii ambayo hutoa mahusiano yasiyo sawa ya mamlaka, udhibiti na ukandamizaji (Fairclough na Wodak, 1997). Usemi ni tendo la kijamii ambalo linaweza kutumiwa kuzindua mahusiano ya kiuwezo. Huu ni mkabala wenye mitazamo mbalimbali. Hata hivyo mtazamo na maoni yaliyodokezwa na mtaalam Ruth Wodak yatakuwa mihimili mikuu katika utafiti huu. Haya yanahusu Itikadi, Mamlaka na Uhakiki.

Kwa misingi ya kazi hii mambo yafuatayo yatakuwa ni muhimu sana kwa nadharia hii:

(i) Lugha ni zao la jamii.

(ii) Sio mtu binafsi tu, bali taasisi na makundi ya kijamii huwa na maana mahususi na thamani ambazo hudhihirishwa kupitia lugha kwa utaratibu fulani.

(iii) Matini ni viungo muhimu vya lugha katika mawasiliano.

(iv) Wasomaji ama wasikilizaji huwa sio wapokeaji tu wasiotambua uhusiano wao na matini. (Kress, katika Wodak 2001 b:6)

Uhakiki humaanisha kuangalia usemi au matini kwa jicho la upekuzi na kuweka wazi hali zote pasi kuegemea upande wowote. Itikadi ni njia ambazo maana huundwa na kuwasilishwa kwa viashiria vya aina tofauti (Wodak 2002). Katika mipaka ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi, itikadi huonekana kama hali zinazoibua na kudumisha mahusiano yasiyo sawa ya kimamlaka. Wodak anaeleza kwamba tofauti katika makundi ya kijamii na itikadi zao zinatokana na mahusiano ya kimamlaka ambayo huzalishwa na kuhalalishwa katika kiwango cha itikadi na maana ili kudhibiti watu wengine. Wodak (1989) anasema katika jamii ya kisasa mamlaka hudhihirishwa kwa namna ya kidemokrasia ambapo kimsingi hailazimishwi, bali ni kwa namna ya kushawishi – ambayo ni itikadi. Kuhusiana na mamlaka, nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi hujihusisha kuchunguza jinsi jinsia inavyoundwa ikihusishwa na thamani zisizolingana. Katika muktadha wa lugha, Uchanganuzi Hakiki wa Usemi hujihusisha *kuchanganua lugha ya walio na mamlaka ambao wanawajibika kwa kutokuwepo na usawa, na*

wale walio na namna na nafasi za kuboresha hali hizo (Wodak 2002:10 katika Onyango 2007). Huu ndio msingi ulioongoza kufanywa kwa utafiti huu.

Wodak (2002) anaeleza kwamba jukumu la nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ni kuchunguza tofauti za kijamii zinazodhihirishwa, kutambulika, kuratibishwa na kuhalalishwa katika matumizi ya lugha. Huhusika haswa na miundo ya kimamlaka ambayo huzalishwa na kudumishwa kupitia usemi. Huhusu hali zote za viashiria ambavyo ni katika maandishi, mazungumzo na ishara zisizo za lugha, na hutambua uzito ambao lugha na usemi zimepewa katika migao ya kijamii, kiuchumi na kimamlaka.

Fairclough na Wodak (1997) wanashikilia kwamba lugha ni tendo la jamii. Wanasisitiza umuhimu wa muktadha wa matumizi ya lugha. Ni nadra usemi kuwa zao la mtu mmoja. Wanasema, usemi huongozwa na tofauti za kimamlaka ambazo ni sehemu ya jamii. Kupitia tofauti za kimamlaka, itikadi kuhusu makundi tofauti huibuka na kujengwa ama kuendelezwa kupitia lugha. Itikadi hizi zinaweza kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, kisha huzoelewa na wanajamii na kuonekana kama 'kawaida' au 'halali'. Hii ndiyo sababu maoni hayo yao yalikuwa ni muhimu sana katika utafiti huu – kuchunguza iwapo kuna itikadi ambazo huchukuliwa kuwa za kawaida na halali kupitia nyimbo za harusi za Kikuyu.

Nadharia hii hujihusisha na jinsi ambavyo wanajamii hupata na kuendeleza uwezo na mamlaka katika jamii husika. Pia, hubainisha utendakazi na kuendelezwa kwa itikadi katika taasisi za kijamii. Aidha, huonyesha jinsi vile usemi huundwa na kuongoza mielekeo na mitazamo ya wanajamii. Hali hii ilichunguzwa katika utafiti huu katika kuangazia matini za nyimbo za harusi za Kikuyu.

Kama anavyosema Wodak (2001) uchanganuzi hakiki haumaniishi kuwa na mkabala hasi kuhusu jambo bali kuwa mdadisi. Yaani kuwa katika hali ya kutoa suluhisho kwa matatizo ambayo nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi inaweza kutambua. Utafiti huu ulilenga kuchanganua kihakiki lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za Kikuyu, kutambulisha iwapo kuna matatizo yanayohusiana na itikadi, na ikiwa yapo – kupendekeza masuluhisho kwa matatizo hayo.


Kulingana na Fairclough (1992), nadharia hii ina nguzo tano: kwanza, mdahalo huundwa na jamii. Pili, mdahalo husaidia katika kuunda (na kubadilisha) maarifa, mahusiano ya jamii na utambulisho wa jamii. Tatu, mdahalo huundwa na mahusiano ya kiuwezo/kimamlaka na

umesheheni itikadi/aidiolojia. Nne, kuundwa kwa mdahalo ni suala kuu katika kinyang'anyiro cha uwezo/mamlaka. Tano, nadharia hii inaonyesha jinsi lugha na mdahalo hujengana.

Fairclough (1996:62) anaendelea kusema kwamba, itikadi na mamlaka hudhihirika na hutolewa katika matumizi ya kila siku ya mazungumzo na matini ambazo huonekana kuwa za kawaida na zilizokubalika. Ni katika mawazo kama hayo ya Fairclough, ambapo utafiti huu ulichunguza matini za nyimbo za harusi za Kikuyu, kuchunguza iwapo lugha inabainisha itikadi na mamlaka.

Anaendelea kueleza kwamba mdahalo huchangia katika ujenzi wa nyanja zote za muundo wa jamii, katika kuziunda au kuzikwamiza kupitia kaida zake, mahusiano, utambulisho pamoja na taasisi zinazosheheni miundo hiyo. Anasisitiza kuwa mdahalo ni tendo la kuwakilisha, kuashiria, kuunda na kujenga ulimwengu kimaana. Anadokeza vipengele vitatu vya kudhihirisha athari za mdahalo: kwanza, mdahalo huchangia katika ujenzi wa utambulisho wa kijamii. Pili, mdahalo husaidia katika ujenzi wa mahusiano ya kijamii miongoni mwa watu. Tatu, mdahalo husaidia katika ujenzi wa mfumo wa maarifa na imani. Mambo haya yatakuwa muhimu kuyachunguza katika utafiti huu kwa sababu, matini za nyimbo za harusi za Kikuyu ziliangaziwa ili kutathmini jinsi lugha inavyochangia katika kujenga mahusiano kati ya mume na mke, kuleta uhusiano wa kijamii, na athari ya lugha hiyo katika masuala ya ndoa.

Fairclough (1989) anapendekeza njia tatu za kufanya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi. Yaani uchanganuzi ushughulikie Uchanganuzi wa Matini, Uchanganuzi wa tendo la Mdahalo (Maingiliano) na Uchanganuzi wa tendo la Jamii (Miktadha). Njia hizo tatu zimeonyeshwa katika jedwali lifuatalo:




**Jedwali 1. Njia za kufanya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi.**

Uhusiano kati ya matini, tendo la jamii (muktadha) huoanishwa na tendo la mdahalo (maingiliano) katika kueleza jinsi matini huzaliwa na kufasiliwa kutegemea tendo la jamii ambalo matini inalihusu; muundo wa matini na sifa zake rasmi na za kimtindo huchunguzwa. Vilevile, mchakato wa uzalishaji wa matini hurahisisha ufasili wa matini.

Kutokana na jedwali hili, nadharia hii ina misingi mitatu ambayo huenda sambamba na hatua tatu za kufanya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi:

i) **Ufafanuzi:** Huhusu kuhakiki sifa rasmi za matini kama vile msamiati, sarufi na miundo ya matini.

ii) **Ufasili:** Hueleza mahusiano kati ya matini na maingiliano (tendo la mdahalo) hivi kwamba, matini huangazwa kama zao la mchakato wa uzalishaji na kama raslimali ya mchakato wa ufasili. Kaida zinazotumiwa hubainishwa na jinsi zilivyotumika huchunguzwa pia.

iii) **Maelezo:** Hujihusisha na uhusiano kati ya maingiliano (tendo la mdahalo) na muktadha wa jamii (tendo la jamii). Sifa za kijamii zinazoathiri michakato ya uzalishaji na ufasili pamoja na athari za kijamii huchunguzwa. Hatua hii ya maelezo pia huchunguza mchango wa mdahalo kwa tendo la jamii, athari za mdahalo katika uundaji wa maarifa, mahusiano na utambulisho wa kijamii. Athari za kiitikadi/aidiolojia, kisiasa na kimamlaka zilizotumika huangaziwa.

Brown na Yule (1993:1) wanaunga mkono mtazamo wa Fairclough wanaposema kuwa uchanganuzi usemi ni uchanganuzi wa lugha katika uamilifu wake. Hivyo basi uchanganuzi huu hauwezi kuwekewa mipaka katika isimu pekee, bali katika uamilifu wa lugha kwenye shughuli za binadamu. Ndio sababu utafiti huu ukachunguza uamilifu wa lugha katika kuendeleza itikadi na mamlaka kupitia nyimbo za harusi za Kikuyu.

Chomsky (1965) anataja kwamba binadamu hujifunza lugha inayopatikana katika mazingira anamokulia. Lugha ndiyo huweza kusheheni itikadi za kitamaduni zilizo katika mazingira fulani. Hivyo basi kazi ya Chomsky ya kuchanganua sarufi ilikuwa muhimu sana kubainisha miundo ya kiisimu yenye kudhihirisha mamlaka na itikadi katika matini za nyimbo za harusi za Kikuyu.

Van Dijk (1997) anasema kuwa nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi huzingatia matatizo mbalimbali ya kijamii na hivyo, huchanganua mtazamo wa wale ambao hutwezwa na

kuchanganua jukumu la vipengele mbalimbali vya lugha vinavyotumika katika kuhalalisha ngazi za kiutawala na kulinganisha na wanaomiliki mamlaka, njia na nafasi za kusuluhisha matatizo haya. Utafiti huu ulichunguza iwapo matumizi ya lugha katika nyimbo za harusi za Kikuyu inabainisha hali ya 'kundi fulani kutwezwa' na kuwepo kwa itikadi na mamlaka.

Uwezo/mamlaka, itikadi, muktadha na historia ni dhana nne muhimu ambazo nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi imejengeka. Kwa hiyo kila usemi na matini ya lugha husika hudhihirisha historia na mielekeo ya jamii, kwa vile usemi na matini huwa na maana katika kipindi fulani cha kihistoria, katika muktadha maalum. Usemi huo na matini hiyo huhalalishwa na itikadi za jamii na hasa kundi lenye kumiliki mamlaka zaidi katika jamii.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaangazia jinsi utafiti wenyewe ulivyofanywa. Inaangazia mahali halisi data ya utafiti ilikusanywa, uteuzi wa sampuli, mbinu za kukusanya data zilizotumika, na jinsi data iliyopatikana ilivyochanganuliwa.

## 3.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika Mkoa wa Kati, Wilaya ya Kirinyaga. Wilaya ya Kirinyaga iliteuliwa kwa kuwa imesheheni takribani koo zote za Wakikuyu. Hivyo basi yaliyokusanywa yangeweza kuwasilisha na kuwakilisha mielekeo, mitazamo na itikadi za jamii yote ya Wakikuyu. Vilevile Wilaya ya Kirinyaga ilikuwa inafikika na mtafiti. Kwanza, mtafiti alilenga kukusanya nyimbo za harusi za Kikuyu na hivyo ikawa ni rahisi kupatana na kutembelea fanani ambao ni gwiji wa kuongoza nyimbo hizo. Pili, mtafiti alijigharamia katika utafiti wake hivyo basi suala la uchechefu wa hela lingeweza kuwa kikwamizo cha kusafiri mbali kufanya utafiti.

## 3.3 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulioongozwa na Utafiti wa Kimaelezo. Huu ni muundo wa kisayansi unaohusu utazamaji na uelezaji wa hali ya kitu pasipo kukishughulisha kwa njia yoyote, Mugenda, O. na Mugenda, A. (1999). Utafiti huu ulilenga kuchunguza kwa uhakiki lugha inayotumiwa katika nyimbo kwenye tukio halisi la harusi miongoni mwa jamii ya Wakikuyu.

## 3.4 Uteuzi wa Sampuli

Mtafiti alichanganua nyimbo tano za harusi za Kikuyu ambazo zilirekodiwa kutoka kwa fanani waliopatikana kwenye tukio la harusi. Nyimbo tano ziliteuliwa kutoka awamu tano tofauti katika shughuli za harusi. Hii ni kwa sababu shughuli za ndoa hufuatana katika msambao wa matukio yanayochukua siku nyingi tangu posa, kutoa mahari hadi ndoa. Fanani hao huwa ni mabingwa wanaofahamu nyimbo zenyewe na ambao ndio huziongoza katika sherehe husika za harusi. Kuunga mkono Milroy (1987:84) sampuli hiyo ilikadiriwa kuwa itatosha kwani matini ndogo huweza kuzalisha data nyingi hasa ikifanyiwa Uchanganuzi Hakiki wa Usemi. Vilevile kuteuliwa kwa nyimbo tano za harusi kama matini ya kuchanganuliwa, kuliwezesha

kuchanganua maswala ya kihistoria, mila, na itikadi ambazo zinaweza kuendelezwa kupitia lugha.

### 3.5 Mbinu za Kukusanya Data

Mbinu ya kunasa nyimbo za harusi za Kikuyu ndiyo iliyokuwa mbinu kuu iliyotumiwa ili kupata data iliyochanganuliwa. Mtafiti alitembelea fanani ambao walikuwa wakiimba nyimbo hizo katika shughuli za harusi huku akizirekodi kwa kinasa sauti. Vilevile mtafiti alikusanya nyimbo zilizokuwa zikiimbwa katika shughuli nzima za harusi, kuanzia wakati kundi la Bw. Harusi linapoingia uani kwa Bi. Harusi wakiomba kuondoka naye hadi mwisho wa shughuli nzima. Hili lilisaidia mtafiti kupata nyimbo zilizokuwa zikiimbwa katika awamu tofauti tofauti na pia kupata fanani, waimbaji na hadhira katika tukio lile la utendaji. Nyimbo hizo zilichanganuliwa kama matini teule kufanikisha utafiti huu.

Vilevile utafiti wa maktabani ulitumiwa kupata yale ambayo yamekwishafanywa kuhusu itikadi na mamlaka, pia kuhusianana na nadharia ya utafiti. Hali kadhalika kudurusu katika mitandao kulitumiwa ipasavyo.

### 3.6 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kueleza na kubainisha nomino, vivumishi, viwakilishi, vitenzi, sitiari/jazanda, pamoja na maudhui ambayo hubainisha itikadi tofauti za kimamlaka katika ndoa na zinavyodumishwa. Data ilitolewa kutoka kwa nyimbo teule tano za harusi za Kikuyu ambayo ndiyo ilikuwa matini ya kuchanganuliwa. Umaratokezi wa aina hizi za maneno kwenye matini za usemi wa nyimbo ulibainishwa ili kutoa kauli ya kijumla kudhihirisha jinsi itikadi zinavyoendelezwa kupitia lugha. Aidha maelezo ya uchanganuzi kuhusu majukumu ya washiriki katika muktadha ule yalitolewa kuzingatia nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi.

Katika kuchanganua data ya nyimbo zilizo kwenye viambatisho, hatua zifuatazo ziliweza kuzingatiwa:

(i) Kutafsiri matini za wimbo kutoka lugha ya Kikuyu hadi lugha ya Kiswahili. Tafsiri huru ilitumika ikilenga kupata visawe vya maneno katika lugha zote mbili. Hii ni kwa sababu data iliyotarajiwa ilikuwa katika lugha ya Kikuyu, lakini mahitaji ya kazi hii yalihitajika kuwa katika Kiswahili. Tafsiri ya Kiswahili ikatolewa kando mwa wimbo wa Kikuyu.

(ii) Kufafanua sifa rasmi za matini kwa kueleza matumizi ya maneno yaliyo katika wimbo wenyewe na yalivyotumika kuibua maana kamili ya wimbo mzima, yaani maudhui. Matumizi ya aina fulani za maneno yakahakikiwa kubainisha yanadhihirisha maana gani katika muktadha wa jamii ya Wakikuyu, na katika muktadha wa matumizi.

(iii) Kupitia nyimbo zote zilizochanganuliwa basi dhana zinazoibua itikadi zilirekodiwa na kuonyeshwa kwa maelezo kamili yanayofananua jinsi lugha inavyotumika kutambulisha na kudumisha itikadi za kijamii kwa namna ya ushawishi.

Mtafiti vilevile alichanganua kwa maelezo nafasi ya washiriki na majukumu yao katika muktadha mzima wa shughuli ya harusi. Kwa kuzingatia nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi kila muktadha ukibainishwa ili kumulika kwa nini usemi huo ukatolewa katika tukio lile.

EGERTON UNIVERSITY LIBRAR

# SURA YA NNE

# MSINGI WA KIHISTORIA WA JAMII YA WAKIKUYU NA UBAINIFU WA ITIKADI ZA KIMAMLAKA KATIKA NYIMBO ZA HARUSI ZA KIKUYU KUTEGEMEA JINSIA

## 4.1 Msingi wa Kihistoria wa Jamii ya Wakikuyu

### 4.1.1 Utangulizi

Katika sehemu hii mtafiti ataangazia jinsi ambavyo mwanajamii Mkikuyu anavyojamiishwa tangu anapozaliwa hadi uzeeni. Hii ni kwa sababu nyimbo za harusi kama mojawapo wa tanzu za fasihi huwakilisha maisha katika uhalisia wake na kama anavyosema Chomba (2005), fasihi huibuliwa na asasi mahsusi za kijamii. Itatambulika kuwa utamaduni wa jamii unaodhihirika kutokana na historia yao huibua mitazamo na falsafa ya wanajamii hao kuhusu maisha na mazingira yanayowazunguka.

Suala la uana ni jambo ambalo linaoteshwa mizizi na tajiriba na mielekeo ya watu kuhusu uwezo, siasa, utamaduni na maingiliano ya kila siku. Dhana ya majukumu yaliyoainishwa kulingana na uana, tabia na matarajio ya jamii hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia kwa ujamiishaji. Kulingana na Kenyatta (1978) watoto hufunzwa kuhusu uana wao tangu wanapozaliwa. Wanajifunza kutenda mambo ili kuonekana kama mvulana au msichana na hivyo kukubalika katika jamii husika. Karega (1994:34) anasema kuwa uchunguzi wa fasihi simulizi huhusisha utalii wa hali ya kuangalia jinsi lugha inavyotumika kuendeleza itikadi za mamlaka ya kijinsia. Mhimili wa nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi unashahidisha umuhimu wa kuangalia lugha inavyotumika kuendeleza itikadi za mamlaka ya kijinsia kupitia nyimbo za harusi.

Ni kulingana na kauli hiyo na nguzo ya nadharia husika ambapo mtafiti ilimbidi kuangalia nyanja zifuatazo za maisha ya mwanajamii Mkikuyu kama hatua ya kufafanua zaidi maana na matumizi ya lugha inayobainisha mwanamke na mwanamume Mkikuyu.

### 4.1.2 Asili ya Wakikuyu Kulingana na Visasili

Jamii ya Wakikuyu ilikuwa na imani kubwa kwa Mungu wao aliyeitwa *Ngai*. Kulingana na Kenyatta (1978:2), Wakikuyu wanaamini kuwa Mungu aliishi katika kilele cha mlima Kirinyaga (Mlima Kenya). Kilele cha mlima Kenya palikuwa na theluji nyeupe mno iliyoshinikiza imani ya Wakikuyu kwamba hiyo ni ishara ya Mungu mwenyewe. Ule weupe wa

theluji ukaeleweka kama ishara ya utukufu wa Mungu. Wakawa kila walipoomba walikuwa wakielekea kwenye kilele cha mlima huo. Inaaminika kuwa baada ya kuumba nchi nzuri, *Ngai* aliumba mwanamume aliyeitwa Gikuyu ili aweze kutunza na kudhibiti nchi hiyo. Vilevile *Ngai* alimuumbia mwanamke msaidizi aliyeitwa Mumbi. Watu hawa wawili waliteremka kutoka mlima Kirinyaga na kuelekea upande wa kusini na kufanya makao yao mahali palipoitwa Mukurwe wa Nyagathanga – Murang'a.

Huku wakiendelea kuishi mahali hapo, Gikuyu na Mumbi walijaliwa kupata watoto kumi wa kike. Suala hilo lilimtatiza sana Gikuyu. Wasichana hao walipofikisha umri wa kuolewa, Gikuyu aliomba Mungu amjalie wavulana ambao wangeoa mabinti zake. Ili Gikuyu amfurahishe Mungu, alichukua beberu wa rangi moja na kumchinja kama kafara chini ya mti wa mkuyu (*Mugumo*). Mti huu wa mkuyu ulikuwa na umuhimu mkubwa wa kidini miongoni mwa Wakikuyu. Eneo la mti huo lilionekana kama mahali patakatifu na chini ya kivuli cha mti huo pakawa pakitumiwa kama madhabahu.

Gikuyu alimchinja beberu na kumchoma kama sadaka. Aliamini kuwa harufu tamu ya nyama ingesafirishwa na upepo hadi kilele cha mlima Kirinyaga palipoaminika kuwa makao yake Ngai. Kitendo hiki cha kumtolea Mungu sadaka chini ya mti wa *Mugumo* kilikuja kuwa mashuhuri miongoni mwa jamii ya Wakikuyu hasa pale ambapo jamii hii ilikumbwa na janga lolote. Basi Mungu alikubali ile kafara ya Gikuyu na akaamua kumkirimia ombi lake. Mungu alimwambia Gikuyu kwamba amchukue mkewe na binti zake nyumbani. Kisha baada ya kufanya hivyo alitakiwa arudi chini ya ule mti wa Mugumo ambapo alikuta wavulana watanashati ambao walikuwa tayari kuoa binti zake kwa masharti atakayopendekeza yeye na familia yake (Kenyatta 1978:2). Jamii hii ilianza kufuata mfumo wa itikadi za kukeni. Majina ya mabinti hawa yalikuja kuwa utambulisho wa mbari za jamii ya Wakikuyu. Mbari hizi ni kama zifuatazo:

| Mzazi | MBARI (*MUHIRIGA*) |
|---|---|
| 1. Wanjiku | Agaciku |
| 2. Wambura | Ambura (Mwithaga) |
| 3. Wamuyu | Aicakamuyu |
| 4. Wangari | Angari |
| 5. Wairimu | Airimu (agathigia) |
| 6. Wangui | Angui (aithiegeni) |

7. Wambui — Ambui
8. Wanjiru — Anjiru
9. Wangeci — Angeci (aitherandu)
10. Wanjeri — Achera (Kenyatta 1978:4)

Jambo la kutatanisha ni kwamba mbari za Wakikuyu zinatambuliwa kuwa tisa. Hii ni kwa sababu inachukuliwa kuwa mwiko kuhesabu viumbe wenye uhai hasa binadamu kwa kuhofia kwamba wangepatwa na mkosi. Mbari hizi hutajwa kuwa *"kenda muiyuru"* (tisa zilizojaa). Umuhimu wa mbari katika jamii ya Wakikuyu ni mkubwa mno. Zilitumika kama kigezo cha kumpa mtu utambulisho.Watu wa mbari moja walishirikiana sana katika shughuli nyingi kama vile hafla ya ndoa, tohara, mazishi na kadhalika.

Muriuki (1974) anaeleza kwamba baada ya Gikuyu kuoza binti zake, aliwaamuru waondoke kwa kuwatawanya kila mmoja njia yake. Aliwabariki na kuwaeleza waongezeke na kusambaa kote ili wajaze na kutunza ardhi waliyopewa na Ngai. Hii ni imani mojawapo ambayo hufanya Wakikuyu watamani kwenda kufanya makao yao mbali na eneo walikozaliwa. Wakikuyu huamini kuwa jamii ya Wakamba na Wameru ni miongoni mwa Wakikuyu waliosambaa mbali na makazi yao ya asili. Hali hii inatokana na ukweli kwamba baadhi ya mila na desturi zao zinarandana na zile za Wakikuyu. Lugha yao vilevile inashabihiana na ile ya Wakikuyu.

Jamii ya Wakikuyu ilizingatia itikadi za kukeni kwa muda mrefu (Kenyatta 1978:4). Wanawake walikuwa na madaraka makubwa dhidi ya wanaume. Chini ya utawala wa jagina Wangu wa Makeri, wanaume walikuwa wamehiniwa na kudhalilishwa pakubwa. Baada ya kukabwa sana na maonevu ya wanawake, wanaume walipanga njama ya kutwaa uongozi kutoka kwa wanawake. Hata hivyo jambo hilo halikuwa rahisi kwa kuwa zana zote za vita zilikuwa mikononi mwa wanawake. Wanaume wakaamua kutekeleza mapinduzi ya amani.

Wanaume walikaa kwenye baraza na kukubaliana kwamba kila mwanamume aliye na mke aende ampachike mimba. Hii ni kama anavyosema Chomba (2005:23), mwanamke mwenye mimba na aliye na jeraha hawana tofauti. Wanaume walifahamu kuwa katika hali hiyo mwanamke hangeweza kupigana wala kutetea haki zake kwa dhati. Matokeo yakawa ni wanaume kutwaa mamlaka na hivyo mfumo wa kukeni ukapigwa kumbo huku itikadi ya kuumeni ikishika kani.

Visasili vya Wakikuyu vimeaminiwa sana na hata kurejelewa na wasomi maarufu kama vile Ngugi wa Thiong'o (1970:70) anaposema kuwa:

"kabla ya Agu na Agu, mwanzo wa yote Murungu (Mungu) muumba aliumba Gikuyu na Mumbi, baba na mama wa jamii ya Agikuyu. Aliwafanya kusimama katika mlima mtakatifu akawaonyesha ardhi yote ile na kuwatunuku."

Hili linamaanisha kuwa visasili hivi vilithaminiwa sana na wanajamii hawa.

### 4.1.3 Asili ya Wakikuyu Kulingana na Ithibati ya Kihistoria

Kulingana na Muriuki (1974), jamii ya Wakikuyu ni tapo moja la kundi la watu wanaofahamika kama Wabantu wa Mashariki. Kulingana na ithibati za kihistoria Wakikuyu, Wakamba, Wadigo, Mijikenda, waduruma na jamii zingine zinazokurubiana, walihama kutoka eneo la Kusini mwa nchi ya Kidemokrasia ya Congo. Wakateremka kusini mashariki wakipitia kusini mwa ziwa Victoria na kukalia maeneo ya milima ya Taita. Nadharia hii inakiri kuwa wengi walielekea kwenye maeneo ya upwa wa bahari ya Hindi na kuelekea hadi kusini mwa Somalia sehemu inayoitwa Shungwaya. Sehemu hii ilikuwa na rotuba nyingi kwa kilimo na lishe kwa mifugo yao. Palitokea vita baina ya Wagalla na Wabantu kwa sababu ya malisho. Kitendo hicho kiliwalazimisha Wabantu kuhama kufikia mwaka wa 1600. Wakatawanyika katika maeneo ya upwa na kati ya Afrika Mashariki. Walipendezwa sana na maeneo ya milimani ambayo waliitwa na kufweka vichaka na kuanza shughuli za kilimo na ufugaji mifugo.

Historia inaelekea kueleza kuwa hali hiyo ndiyo ilipelekea Wakikuyu kuchukua sehemu za Mlima Kenya (Mlima Kirinyaga) na kufanya makao yao hapo. Kipindi hicho kilikuwa ni nusu ya kwanza ya karne ya 18. Ndiposa baadaye walisambaa katika maeneo ya Kiambu, Murang'a, Nyandarua, Nyeri (Ruare) na Kirinyaga pia.

### 4.1.4 Hali ya Kijamii ya Wakikuyu

Familia ndicho kilikuwa kiungo muhimu cha kimsingi. Familia kadhaa ziliweza kuunda ukoo. Katika umri wa kubaleghe wavulana na wasichana walikwezwa katika utu uzima kupitia kwa baadhi ya mivigha iliyohusu tohara. Waliweza kufunzwa mambo yanayohusu thamani na mila za jamii (Kenyatta 1978: 76).

Wavulana waliotahiriwa pamoja waliunda *riika* na moja kwa moja wakawa walinzi wa jamii. Jukumu lao lilikuwa ni kulinda jamii kutokana na mashambulizi yoyote kutoka nje.

Wanarika walikuwa ni kama ndugu. Mfumo huu ulisaidia kuunda mshikamano mkubwa wa kindugu baina yao. Watahiriwa wapya hutwaa nafasi ya rika lililokuwepo huku rika hilo likipata majukumu makubwa ya kijamii kama ya kiutawala na kusuluhisha mizozo.

Muriuki (1974) anaendelea kusisitiza kuwa Wakikuyu waliabudu Mungu mmoja mkuu *Ngai* ambaye waliamini kuwa ni mwenye nguvu zote na mwenye kuongoza kila kitu. Iliaminika kwamba Mungu aliishi kwenye kilele cha Mlima Kenya (Kirinyaga). Imamu waliongoza maombi kupitia kwa roho za mizimu katika madhabahu takatifu. Nabii (*Murathi)* alifasiri ujumbe wa Mungu na kuwatabiria mambo yanayokuja. Nabii vilevile alitoa kafara za kuonyesha shukrani au kuomba baraka za Mungu. Mganga (*Mundu Mugo)* naye alitibu wagonjwa na kutoa pepo mbaya.

### 4.1.5 Hali ya Kisiasa ya Wakikuyu

Kisiasa jamii ya Agikuyu ilikuwa ni katika hali ya ugatuzi (Kenyatta 1978:100). Yaani mamlaka yalikuwa ni katika viwango vya kimakundi. Kundi ndogo la mamlaka lilikuwa ni familia, ikiongozwa na baba. Lilikuwa ni jukumu la familia kufunza watoto amali zote za jamii, huku wazazi wakiwa ndio walimu wa kwanza kwa mtoto katika kumjamiisha. Kungelikuwa na jambo, kungefanywa halmashauri ya familia (*ndundu ya mucii)* ikiongozwa na baba. Lolote lililozungumzwa lilihitajika kubaki kama siri ya familia hiyo. Ndiyo sababu ya methali *cia mucii ti somo* (mambo ya nyumbani hayana rafiki eti ajulishwe).

Familia kadhaa ziliweza kuunda ukoo, kiungo cha kimsingi cha kisiasa kilichohusisha mamlaka ya milango *(Mbari)*, waliokuwa nyanda moja. Ukoo uliongozwa na baraza la wazee (*Kiama)* ambapo mwenyekiti (*Muramati)* aliheshimiwa sana kwa busara yake. Alikuwa na jukumu la kuunganisha watu na alimiliki sifa nyingi za uongozi. Wazee hawa walikuwa ni wazee wenye umri wa miaka zaidi ya hamsini. Wazee hawa walijulikana kama rika la *Maina* na *Mwangi.* Pia walijulikana kwa jina lingine kama *Irungu.* Rika moja liliongoza kwa kipindi cha kati ya miaka thelathini hadi arobaine na kisha kuachia uongozi rika lingine ambalo limetimia umri huo wa kutawala. Mamlaka na madaraka yote ya kuendesha jamii yalikuwa chini ya baraza la wazee. Baraza moja lilikuwa ni kama mahakama. Muriuki (1974) anasema kuwa hakuna mwanamke ambaye alijumuishwa katika baraza hizi za wazee.

Kenyatta (1978: 105) anasema kwamba jukumu kubwa la baraza lilikuwa ni kutatua mizozo ya shamba na haki za umiliki, kutatua kesi za raia na za jinai, na pia kuongoza shughuli za kidini au sherehe maalum ya jamii. Kipande cha ardhi kilikuwa ni muhimu sana katika jamii ya Wakikuyu. Wavulana walirithi kipande cha shamba kutoka kwa baba zao hasa baada ya wao kutahiri. Baada ya kifo cha baba, mvulana wa kwanza alichukua mamlaka ya kuiongoza familia ile. Mvulana huyo pia alitambuliwa kama *Muramati* – mtunzaji. Kwa upande mwingine, Baraza kuu la Wazee wakongwe wenye hekima (*Kiama Kia Ndundu)* liliteuliwa kutoka kwa mabaraza hayo na lilitumika kama mahakama ya rufaa.

Kwa kila kiwango cha kiutawala, kila kundi lilikuwa na wajibu wake wa kutekeleza. Hakuna suala lolote la kijamii ambalo halingetatuliwa na Baraza kuu la Wazee. Waliokosea wangepigwa faini ya mifugo kiasi fulani, kuchapwa mijeledi, au hata kufukuzwa kabisa kutoka jamii ile. Hakukuwa na majumba maalum ya kufanyia kesi na kutolea maamuzi. Kesi zilifanywa kwenye kivuli chini ya mti katika maeneo wazi, hasa iwapo zilihusisha watu wengi. Lakini iwapo ni katika kiwango cha familia, kesi zilifanyiwa kwenye nyumba ya mzazi wa kiume iliyofahamika kama *thingira.*

Mabaraza hayo yalijumulisha wanaume waliokuwa na ujuzi wa maswala ya jamii hii na hayakujumlisha wanawake miongoni mwao. Kenyatta (1978) anasema kuwa ingawa kulikuwa na kamati zilizoshughulikia mambo ya wanawake, kamati hizo ziliendeshwa na wanaume. Utafiti huu ulichunguza jinsi lugha inavyotumika kubainisha hali ya kisiasa na mamlaka kupitia nyimbo za harusi za Kikuyu.

### 4.1.6 Hali ya Kiuchumi ya Wakikuyu

Njia kuu ya kiuchumi ilikuwa ni kilimo. Kenyatta (1978:17) anafafanua kuwa mfumo wa ukulima ulioendeshwa ulikuwa ni ule wa kufyeka sehemu ya msitu na vichaka kwa sababu ya kupanda vyakula. Wanaume walikuwa na jukumu la kufyeka vichaka nao wanawake walipalilia shamba. Jambo hilo linatufahamisha kuwa ugawanyaji wa majukumu uliendelezwa sana na jamii hii. Hii ni amali inayopitishwa na kurithishwa kupitia ujamiishaji. Hata ingawa kipande cha ardhi kingekuwa kidogo vipi, kila mwanajamii alitakikana kutia bidii ili aikimu familia yake. Suala la kutia bidii kazini lilienziwa sana miongoni mwa Wakikuyu. Walipanda wimbi, mtama, maharagwe, mahindi, mihogo, miwa, ndizi na kunde. Vilevile walifuga ng'ombe, kondoo na

mbuzi. Wazee walithamini sana wingi wa mifugo. Mifugo walitumiwa katika shughuli nyingi za jamii hii, kama vile lishe nyumbani, kulipa mahari, kulipia fidia, kutoa kafara, na kadhalika. Ilikuwa ni kipimo cha bidii ya mtu kuwa na mifugo wengi na hivyo kuwa na utajika mkubwa.

Biashara za karibu baina ya majirani walio nyanda zilizokaribiana ilishamiri. Bidhaa kama vifaa vya chuma, mifugo, chumvi, mchanga mwekundu, vifaa vya udongo, vikapu, tumbaku, na nafaka viliuzwa. Siku ya nne kwa wiki shughuli za biashara zilifanywa katika soko maarufu kama vile Kiambu, Gakindu, Karatina na Muthithi. Kadhalika, Wakikuyu walishiriki biashara na majirani zao. Walinunua asali na pembe za ndovu kutoka kwa jamii ya Ogiek kwa kubadilishana na nafaka. Pia walipata vyuma, nguo na glasi kutoka kwa Wakamba kwa kubadilishana na mifugo na pembe za ndovu. Biashara baina ya Wakikuyu na Wamaasai ilifanywa na wanawake wakiandamana na mwanaume mkalimani. Walizuru Naivasha, Narok, Kajiado, na Nanyuki kupitia vichochoro vya wasafiri (*Njira cia Agendi)* kuuza maharagwe, mtama, tumbaku na mchanga mwekundu kwa kubadilishana na mifugo, ngozi, maziwa na siagi (Muriuki 1974: 76).

Kulikuwepo pia na wahunzi waliobobea ambao walitengeza vifaa vya vyuma kama vile jembe, mbugi, visu, shoka na mikuki. Ilikuwa ni kazi ngumu ya kuchoma vipande vya vyuma kwa muda mrefu kwenye makaa, na kisha kuvipondaponda kwa mawe hadi kuchukua umbo linalotarajiwa la mikuki au visu. Kisha kulikuwa na aina maalum ya mawe yaliyotumika kunolea ala hizo. Ushonaji/usukaji vikapu (*Ciondo)*, teo (*Itaruru,)*, pakacha la kuhifadhia nafaka (*gitete)* na ufinyanzi wa vyungu ulifanywa na wanawake huku wanaume wakienda kuwinda na kukusanya wanyama wa pori, matunda na mizizi. Kazi hii ya ushonaji na usukaji ilifanywa wakati wa ziada. Aidha ufugaji wa nyuki na utengenezaji wa ngoma za muziki yalikuwa ni matendo anuwai muhimu ya kiuchumi kwa jamii hii.

Ushonaji wa mavazi kwa kutumia ngozi za wanyama ulifanywa. Wanawake walivalia *nguo ya ngoro* iliyofunika kifuani, *muthuru* iliyofanana na rinda, na *mwengu* iliyovaliwa sehemu ya mbele kuanzia kiunoni. Nao wanaume walivalia *githere* na *githii* hasa wakati wa tamasha. Vazi la mwanamume lilisetiri upande wa mbele na makalio tu. Aidha, kutokana na wanyama wa pori waliouawa, wanaume walihifadhi ngozi zao na kuziunda kama mavazi ya kifahari au ya viongozi katika mabaraza yao. Mathalan, ngozi ya chui na ngozi ya chatu zilivaliwa na kiongozi wa mbari fulani.

Biashara ilifanywa kwa kubadilishana vitu. Hii ni kabla ya kuja kwa sarafu. Thamani ya vitu ilikadiriwa kwa kutumia kondoo na mbuzi, au mazao ya shambani. Ifahamike kwamba wanyama hawa walikuwa na majukumu mengi miongoni mwa jamii ya Wakikuyu. Mbuzi walitumika kulipia mahari huku kondoo wakitumika sana kutolea kafara na shughuli zingine za kidini.

Utafiti huu ulichunguza jinsi lugha katika nyimbo za harusi za Kikuyu inavyodhihirisha hali ya kiuchumi miongoni mwa Wakikuyu.

#### 4.1.7 Hali ya Maisha ya Kijamii ya Mkikuyu

Maisha ya Mkikuyu hayakuwa na maana yakitenganishwa na matendo na maisha ya wanajamii wenzake. Kwa mfano, ilikuwa ni nadra sana kwa mwanajamii hasa mtoto kumwita mwanajamii mwenzake kwa jina (Kenyatta 1978:6). Njia iliyokubalika ya kumwita mtu ilikuwa ni kwa kumhusisha na maharimu wake; yaani mtoto wake au jamaa yake kama vile baba fulani ama nyanya fulani. Watoto na vijana ndio waliitwa kwa majina yao. Mtoto alipozaliwa na kukua hadi kufikia mtu mzima, alipitia hatua mbalimbali ambazo zilimsaidia kumuelimisha kuhusu kushirikiana na watu wengine. Kabla ya kuamua kufanya lolote mwanajamii angetafuta ushauri kutoka kwa jamaa yake au rafiki wake wa karibu.

Ushirikiano wa watu wa jamii moja hudhihirika waziwazi kupitia kwa hatua mbalimbali anazopitia mwanajamii. Hatua hizi huwa kama kaida na anayekiuka kaida hizi hutengwa na kuonekana kama mwasi. Tabia za kila Mkikuyu huongozwa na mila na desturi zilizowekwa na ambazo zinazingatiwa kama katiba ya kuwaongoza wanajamii katika mahusiano yao ya kila siku. Hatua hizi zitasaidia kupambanua na kudhihirisha mtazamo wa wanajamii hawa kuhusu uana, jambo ambalo litashahidishwa na nyimbo zitakazochambuliwa. Katika sura ya tano, mtafiti anaeleza awamu za tukio la harusi na kuchanganua nyimbo zinazoimbwa na matumizi ya lugha katika nyimbo hizo ili kubainisha hali inayotarajiwa kuhusu mwanamke na mwanamume katika jamii ya Wakikuyu.

##### 4.1.7.1 Desturi za Kuzaliwa kwa Mtoto

Wakati wa mwanamke kujifungua ulipotimia mkunga aliitwa. Kenyatta (1978:60-65), Iwapo mtoto aliyezaliwa ni wa kiume, wanawake waliokuwa hapo walipiga kemi tano kuashiria kuwa ni mvulana. Endapo alikuwa ni wa kike, kemi nne zilipigwa kuashiria kuwa ni msichana.

Kisha mtoto huyo alirambishwa maji yaliyokamwa kutoka kwa miwa (*ngogoyo)* au asali kumkaribisha kwa maisha mazuri ya dunia. Jamii ilishangilia sana ilipopata mtoto kwani walijua kuwa kizazi kitaendelea. Wasichana walipozidi kukua walijihusisha na mama yao na kufunzwa mambo ya kitamaduni – mila na desturi za jamii. Nao wavulana walipozidi kunenepa walijihusisha na baba yao ambaye pia aliwafunza itikadi na mila za utamaduni wao. Waliandamana na baba zao kwenda kuchunga mifugo na shughuli zingine za mchana kutwa.

Mtoto alipozaliwa alipewa jina la mzazi wa babake. Yaani watoto wawili wa kwanza wakiwa ni mvulana na msichana, walipewa majina ya baba na mamake baba yao. Waliofuata wawili (mvulana na msichana) nao walipewa majina ya baba na mama wa mama yao. Suala hili linahakikisha kuwa majina ya familia ambazo ni chimbuko la wazazi yaliendelezwa kupitia vizazi vyote na kukumbukwa.

Mtoto mdogo hadi miezi mitatu alitegemea maziwa ya mamake. Kisha baadaye alitanguliziwa kulishwa ndizi (*mitahato)* zilizotafunwa pamoja na uji wa mtama au wimbi. Watoto walianza kupewa mafunzo kupitia nyimbo hasa bembelezi. Ni nyimbo zilizokuwa zenye kuwaongoa na hata kuwafahamisha majukumu yao. Licha ya kwamba watoto hao hawangesikia, walezi waliamini kuwa nyimbo hizo zilikuwa na athari fulani katika maisha ya watoto hao. Watoto walithaminiwa kwani walikuwa ni ishara ya uhai wa jamii katika siku za usoni. Watoto wa kiume walitarajiwa ndio wangeshikilia jamii kisheria kwa kurithi na kwa utawala, nao wanawake wakiendeleza jamii kwa uzazi, ulezi na kufunza maadili mema ya kijamii.

Kenyatta (ibid) anafafanua kuwa mwanamume Mkikuyu alikubaliwa kuwa na wake wawili au zaidi iwapo angedhihirisha kuwa ana mali na angeweza kuwakimu. Ama vilevile, kuwa na watoto wengi kulithaminiwa sana na kulikuwa ni ishara ya mwanamume mwenye bidii. Mke mmoja angepata hata watoto zaidi ya kumi. Aidha, iwapo mwanamke angekosa kujifungua mtoto wa kiume, aghalabu mwanamume alishawishiwa sana kuoa mke mwingine ili apate mvulana ambaye angerithi mali yake. Hii ilikuwa ni kwa sababu wasichana walitazamiwa kuwa wangeolewa wakati fulani na hivyo waondoke katika boma hilo.

Japo kina mama walikuwa na jukumu kubwa la ulezi, suala la kuadabisha watoto lilishirikisha kila mwanajamii. Mtu yeyote aliyezidi umri aliweza kuadhibu mtoto huyo. Baada ya shughuli za mchana, usiku ulikuwa ni wakati wa watoto kupewa maarifa na nyanya au babu zao kupitia kwa utambaji wa ngano, vitendawili, mafumbo, methali, nyimbo na kadhalika. Vikao hivi vilitumiwa na wanajamii kama shule kuelimisha wanajamii kuhusu maswala yanayohusu

maisha yao. Watoto walifunzwa majukumu yao kulingana na uana wao. Wasichana walifunzwa kuhusu kupika, kutunza watoto, ususi, usukaji na kazi zingine za nyumbani ilhali wavulana walifunzwa kuhusu ufugaji, ukulima, ulinzi, uhunzi, usasi, uchongaji na kazi zingine za kiufundiufundi.

Wakati wa kipindi hiki watoto walifunzwa mambo mengi yanayohusu itikadi na desturi (miiko) za kijamii. Muriuki (1974) anakiri kuwa katika jamii hii ya Wakikuyu, wavulana walio kati ya miaka kumi na minane hadi arobaine ndio walipewa jukumu la kulinda jamii. Wavulana walihimizwa kuwa na ujasiri mwingi na kujitoa mhanga kwa ajili ya jamii. Wasichana walihimizwa kuwa na heshima kwa wanaume, wawe watiifu na wenye mapenzi hasa pale mwanamume alikuwa na wake wawili. Hadithi nyingi na nyimbo zilikuwa na maudhui yenye kuhimiza ushirikiano, maadili mema, bidii kazini na utu bora kwa ujumla.

Ili kuingilia utu uzima, tohara ilikuwa ni lazima kwa wavulana na wasichana. Baada ya kupashwa tohara ndipo walitambulika kuwa ni watu wazima na wangepewa majukumu kamili ya kuiongoza na kuendeleza jamii. Kama anavyosema Kenyatta (1978:133) katika jamii ya Wakikuyu tohara ilikuwa ni ishara muhimu kama ilivyokuwa miongoni mwa Wayahudi. Ni tukio ambalo lina umuhimu wa kidini, kitamaduni na kielimu kwa wanajamii Wakikuyu. Tohara ni tendo linalothaminiwa sana miongoni mwa Wakikuyu. Kufuatia maajilio ya wamishonari miaka ya 1844, tohara ya wasichana ilipingwa sana. Dini ya Kikristo ilipoendelea kukita mizizi katika majanibu ya Wakikuyu ndipo upinzani mkubwa uliendelezwa dhidi ya tohara ya wanawake. Wanajamii wengi waliendelea kuasi kutahiri wanawake. Tendo la tohara ndilo lilimzamisha mwanajamii kabisa katika utamaduni na mila za jamii. Watu ambao walikwepa tohara au hawakutahiri na walipaswa kutahiri walirejelewa kwa majina yenye madharau sana. Wavulana waliitwa *ihii* nao wasichana waliitwa *irigu*. Mvulana ambaye hakutahiri hata angekuwa mzee vipi hakuheshimiwa kamwe wala hangejiunga mjadala na mtu yeyote aliyetahiri. Angeishi kukejeliwa na hata kuonekana mwenye kuaibisha familia yao nzima. Kwa hivyo ingebidi atahirishwe kwa lazima.

Kipindi cha tohara ndicho kilikuwa mwafaka cha kutolea mafunzo kwa vijana kuhusu majukumu kamili yaliyowasubiri kama wanajamii kamili. Kinuthia (2005) anasema wasichana walifunzwa jinsi ya kuwatumikia waume wao watakapoolewa. Nao wavulana walifunzwa kuhusu kutamalaki na kulinda jamii dhidi ya uvamizi kutoka nje.

Kupitia kwa mashauri yaliyotolewa kama mafunzo kupitia kwa nyimbo, hadithi na kadhalika wanajamii hasa vijana walikubali majukumu yao. Hali hii ndiyo Wodak (2007) anasema kwamba kuna njia za kiutamaduni za jamii za kushawishi wanajamii kukubali hali fulani pasipo kutumia nguvu. Ndio sababu nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi inajikita kuchunguza jinsi lugha inavyotumika kushawishi wanajamii kuchukua majukumu yanayotazamiwa kuwa yao ya kijaamii. Ni baada ya tohara ambapo mtu alifunzwa mambo hata ya kimapenzi na hata kuruhusiwa kuyafanya ambayo awali hangeshiriki, kama vile kuoa. Vilevile tukio la tohara liliwafanya wanajamii kushirikiana kwani ulikuwa ni wakati wa jamii kuja pamoja na kusherehekea.

Kabla ya siku ya tohara, vijana walitengwa kwenye nyumba maalum kando na makwao. Huko walipewa mafunzo ambayo yalihusu kuchapwa mijeledi. Hawakutakikana kulia. Ilikuwa ni njia ya kuonyesha ushari na ujasiri. Baadaye walikula kiapo cha kutumikia na kulinda jamii kwa ujasiri na kuweka siri palipohitajika kutoka kwa wazee. Vilevile walifunzwa mambo ya kulinda familia zao. Baada ya mafunzo hayo ndipo siku ya tohara ilipowadia waliamshwa alfajiri sana na kuhitajika kukwea mti wa Mkuyu kukata matawi. Uhodari wa kukwea mti pia ulikuwa ni kigezo cha ubabe wa mvulana. Matawi hayo yangeokotwa na wasichana ambao pia wangepashwa tohara wakati ule ule ingawa katika mazingira tofauti. Kisha wavulana walihitajika waingie mtoni ili wakufe ganzi hasa sehemu za uzazi kutokana na maji baridi ya asubuhi ile, ili wasije wakahisi uchungu sana wakati wanakatwa.

Walipotoka mtoni walimkuta ngariba akiwa tayari na vijisu au nyembe kali tayari kuwapasha tohara (Kenyatta 1978:82). Wakati huo huo nyimbo za kuwapa motisha na ujasiri ziliimbwa. Vilevile zilikuwa ni nyimbo zilizokejeli yeyote ambaye angedhihirisha ishara za woga. Hakuna mvulana ambaye alitakikana kulia wala kuonyesha hisia za uchungu. Iwapo angelia, huyo angeaibisha rika lote ambalo lilienda tohara naye. Endapo mtu angelia angeishi kukejeliwa na jamii nzima hata wakati mwingine asingepata mke wa kuoa. Tohara za wavulana na wasichana ziliendeshwa wakati mmoja lakini katika mahali tofauti. Jamaa za waliotahiri waliwaletea watahiriwa chakula cha kila aina mahali ambako walikaa kwa miezi minne wakiendelea kupewa mafunzo ya majukumu yaliyowangoja. Watahiriwa hawakuruhusiwa kufanya kazi mpaka walipopona kabisa.

Kipindi hiki cha tohara kilikuwa na umuhimu mkubwa kwa Wakikuyu. Kilikuwa ni kipindi ambacho walikuwa wakiunganika na Mungu pamoja na mizimu ya walioaga kupitia kwa

mganga au nabii (*Mundu Mugo*). Kwa vile damu ingemwagika mchangani ambako mababu walizikwa, nabii angepiga ramli na kuwaomba wabariki na kuwaondolea laana vijana ambao wangepashwa tohara kwani ndio wangeshikilia jamii na kuiongoza. Kwa hivyo wakati huu waliokosana waliombwa kusameheana na kuridhiana ili jamii nzima iweze kupata baraka kutoka kwa Mungu na hata kwa mizimu ya watu wa kale (Kenyatta 1978:84).

#### 4.1.7.2 Desturi za Ndoa

Kenyatta (1978:87) anasema kwamba ndoa ni awamu/asasi iliyothaminiwa sana na wanajamii wote Wakikuyu. Kila mwanajamii alitazamia kwamba katika umri wake wa ukubwani atakuwa na familia yake na kuendeleza mbari yake kupitia ndoa. Suala la kuishi kama kapera, mseja, ubasha au ushoga halikutambulika kamwe katika jamii ya Wakikuyu. Mtoto alipoendelea kukua alifunzwa jinsi ilivyo muhimu kuoa au kuolewa ili mtu amiliki familia yake na kuendeleza jamii. Kwa hivyo mambo ambayo hayangelingana na kujenga ama kuendeleza familia hayakuwepo akilini mwa wanajamii hii.

Ndoa ilikuwa ni jambo ambalo lilihusisha jamii nzima na wala haikuwa ni tendo la mtu mmoja binafsi. Watoto walionekana kama matunda ya ukamilifu wa ndoa. Yaani utasa na ugumba ni jambo ambalo lilionekana kama laana kutoka kwa mababu walioaga au jamii kukasirisha Mungu.

Baada ya tohara vijana walipewa mawaidha chungu nzima kuhusu walichohitajiwa na jamii kutekeleza. Njia kadhaa kama vile nyimbo, hadithi au ngano, methali na mafumbo zilikuwa zikitumiwa sana kuwanoa kiakili. Walifahamu kwamba kufikia sasa walikuwa tayari kuoa au kuolewa ili waendeleze kizazi cha jamii hii. Mvulana au msichana alikuwa huru kuchagua mchumba. Hata hivyo wazazi walikuwa na uamuzi wa mwisho kuhusu suala hilo.

Muriuki (1974) anaunga mkono Kenyatta (1978:87) kwamba ndoa katika jamii ya Wakikuyu halikuwa ni tendo la siku moja. Mvulana alipovutiwa na msichana fulani aliwafunuliwa siri marafiki wake wa karibu hasa rika lake waliotahiri pamoja. Marafiki hawa walikuwa na jukumu la kuchunguza matendo ya msichana huyo hasa ikiwa alikuwa ni mwenye bidii kazini. Wangejificha mahali na kutazama anapoenda na wengine kukusanya kuni, kuteka maji, anavyozungumza na kadhalika. Ni wazi kwamba matendo ya msichana yalichunguzwa kwa undani. Vijana ambao ni rika moja na mvulana anayetamani kuoa wangetoa ushauri wao kumhusu huyo msichana na kuthibitisha iwapo ako sawa.

Mvulana naye alitafuta muda wa kukutana na msichana huyo faraghani na kisha kumtongoza. Mvulana angemfahamisha msichana huyo nia yake ya kutaka kumuoa. Msichana angehifadhi hilo kama siri hadi pale wazee wa mvulana wangekuja rasmi kwao nyumbani. Baadaye mvulana angemwambia babake azma yake ya kuoa. Hapo basi babake angeita rafiki zake wawili au watatu wa mbari yao kama makachero ambao wangechunguza kuhusu familia ya msichana. Jukumu lao lilikuwa ni kuchunguza mbari ya msichana huyo, kujua iwapo mbari hiyo hujihusisha na mambo mabaya kama uchawi, wizi, uhuni, ulaghai na kadhalika. Iwapo ilikuwa ni familia au mbari yenye matendo mema basi wazee wale pamoja na baba mvulana waliandamana baada ya muda hadi kwa familia ya msichana. Walibeba buyu la pombe iliyotengenezwa kwa asali na miwa na hivyo kuomba kuwa na kikao na baba msichana. Babake msichana angeita wazee jirani zake kama mashahidi wake kwa yale yatakayonenwa na wageni wale. Wazee wa mvulana wangemjulisha babake msichana kwamba mvulana wao ameona msichana katika boma ile na amewaomba waje waombe wazazi wake posa. Msichana yule angeitwa pale katika baraza hilo la wazee kutoka pande zote na kufahamishwa habari iliyoletwa na wazee wale. Basi aliulizwa ikiwa anamfahamu huyo mvulana anayesemewa. Alipokubali kwamba anamfahamu, basi alihitajika kutwaa ile pombe iliyoletwa na wazee wale na kuwatilia kwenye pembe maalum na kisha kuwapatia wazee wale wanywe, akianzia na baba mkwe mtarajiwa. Kisha alimtilia babake, halafu kuwapatia wazee hao wengine. Kwa kufanya hivyo aliruhusiwa kuondoka. Walipoendelea kunywa, wazee hao waliomba wahesabiwe mahari (*ruracio)* ambayo wangehitajika kutoa.

Haikuwa vigumu kutaja mahari ambayo ingetolewa kwani baba ya msichana alihitajika kimila kudai mahari ya binti yake sawa na aliyoitishwa alipokuwa akimuoa mkewe, yaani mamake msichana. Hapo basi shughuli za kulipa mahari ambapo wazee kutoka kwa mvulana hupeleka mifugo ambayo ilikuwa ni mbuzi, kondoo na ng'ombe. Katika mifugo hao ilitakikana wale ambao hawajazaa kwa vile ilitarajiwa kuwa ni ishara ya kizazi kipya. Idadi ya mifugo huwa ishakubalianwa kati ya kundi la wasichana na lile la wavulana. Hata hivyo palikuwepo na utaratibu wa kufuatanisha jinsi ya kutoa wanyama wenyewe. Kondoo *(Mwati)* alitakikana aingizwe zizini kwanza akifuatiwa na mbarika *(Harika)*. Kisha mitamba (*Mori* ), yaani ng'ombe ambao hawajazaa wangeingizwa zizini. Katika jamii ya Wakikuyu ulipaji wa mahari ulitakikana kuendelea katika kipindi kizima cha uhai wa wahusika. Kwa hivyo, hata kama familia ya mvulana ingekuwa na uwezo wa kulipa mahari yote, haikuruhusiwa kufanya hivyo. Ulipaji mahari ulitakiwa kuwa ni ishara ya uhusiano mwema wa kudumu baina ya zile familia mbili. Ndio sababu kulipa mahari

yote kungeonekana kama dua mbaya. Baada ya kulipa mahari kufikia kiwango fulani kilichotajwa na wazazi wa msichana, basi angeruhusiwa kumchukua (Kenyatta 1978:87-91).

Kenyatta (ibid) anaendelea kueleza kwamba, kama ishara ya kukubaliana ndoa baina ya msichana na mvulana, sherehe iliandaliwa nyumbani kwa msichana ambapo wazazi wa mvulana hutoa beberu (*thenge*) na kondoo wa kiume (*ndurume*) wachinjwe na nyama zao kuchomwa ili jamii zote mbili wale zile nyama pamoja. Uchinjaji huu pamoja na umwagaji wa damu ulikuwa ni muhimu sana kama ishara ya kubariki kizazi cha watoto watakaozaliwa. Iliaminika kwamba iwapo kondoo na beberu hawa hawangechinjwa, basi huenda watoto watakaozaliwa na hawa waliooana watakumbwa na matatizo mengi kama vile ulemavu, vifo, mimba kuavya, utasa, ugumba na kadhalika. Kutochinjwa kwa wanyama hao kungemaanisha kuwa jamii zote mbili hasa ya msichana hazijasafishiana nia ya ndoa hiyo. Vilevile pombe ilinywewa iliyokuwa imetengenezwa kwa asali na maji yaliyokamwa kutoka kwa miwa.

Muriuki (1974) anafafanua kuwa wanawake nao walitakikana kubeba vikapu (*ciondo*) ambavyo vilikuwa na mazao ya shambani kama vile nafaka na vyakula vinginevyo. Mkungu wa ndizi aina ya *mitahato* pia ulihitajika. Aina hii ya ndizi ndizo zilitumika kulea watoto. Hivyo basi ndizi hizo huwa ni jazanda inayotolewa kama vifaa muhimu vilivyotumika katika ulezi wa msichana atakayekuwa mke wa mtu. Vilevile kundi la wanawake kutoka jamii ya msichana lingedai lipewe chungu cha kupikia na kingine cha kuhifadhia maji, vyombo kama bakuli, mwiko na hata buyu la asali. Upande wa mvulana hutoa bidhaa nyingi kama zawadi. Bidhaa hizi zilifidia vifaa na bidhaa ambazo familia ya msichana inakisia msichana alipoteza au kuharibu katika miaka ya ulezi.

Ulipaji huu wa mahari ulifasiliwa kama ni kununua yule msichana. Ingesemwa kwamba yule kijana "alinunua msichana" (*niaragurire muiritu*). Jambo hili lilimfanya mvulana/mwanaume huyo kuheshimiwa sana na rika lake na hata kuonekana kuchukua hadhi juu ya mkewe. Bwana na bibi waliofunga ndoa walitazamiwa kuanza majukumu yao ya kifamilia moja kwa moja. Tayari walikuwa wameshafunzwa kila mmoja jukumu lake. Baadhi ya mafunzo ambayo mwanamke alifunzwa ni kumtii mumewe, kuwa na unyenyekevu na mapenzi mengi kwa mumewe na mengineyo. Naye mwanamume alihimizwa kumtii mkewe, kumkidhia mahitaji ya nyumbani na kumlinda. Suala la uaminifu katika ndoa lilisisitizwa sana ingawa wakati fulani jamii iliruhusu mwanamume kuoa wanawake wengi hasa iwapo alidhihirisha angeweza kuwamudu na ana mali. Aidha mwanamume alisisitiziwa kuheshimu mke aliyelipia mahari anayetambuliwa kama

*Mutumia wa Mburi*. Hii ni kwa kuwa ndiye aliyetambulika kimila na desturi kama mke halali. Hata endapo mwanamume angeoa mke mwingine, hao wapya walimheshimu sana mke wa kwanza na kusikia ushauri wake (Kenyatta 1978:94-95).

Ingawa suala la kuoa wake wengi lilikubalika katika jamii nyingi za Kiafrika, Wakikuyu wakiwemo, wazee walitahadharisha sana mtu kuwa na wake wenza. Kama anavyosema Chomba (2005), wake wawili walifananishwa na vyungu viwili vya sumu/uchawi ('*atumia eri ni nyungu igiri cia urogi'*). Hii ni methali ya Kikuyu. Wake wenza wakati mwingine husababisha wivu, mafarakano na hata vita baina yao. Wake wenza huzua chuki ambayo huendelezwa hata kupitia kwa watoto wao na vizazi vya watoto wao. Hata kama wakati mwingi wanawake hao hawakuonyesha chuki waziwazi, bado ilibaki mioyoni mwao na ingesambaa hadi kwa wanao.

Kwa vile shughuli ya ndoa miongoni mwa Wakikuyu ilikuwa ni shughuli ndefu tena ya siku nyingi kuanzia uchumba, posa, utoaji mahari na maisha ya ndoa, suala la talaka lilikuwa ni nadra sana. Wakati wa utoaji mahari na ibada za kuchinja na kadhalika, waliooana walikula kiapo cha kutumikiana kama mume na mke katika maisha yote. Iwapo talaka ingeafikiwa ilibidi kwanza visababisho vijadiliwe na halmashauri ya wazee kutoka pande zote mbili kwa marefu na mapana. Mambo ambayo yangesababisha mke kupewa talaka ni ikiwa angejihusisha na matendo ya uzinzi, wizi, uchawi na kukataa kutekeleza majukumu ya kumpikia mumewe. Kuwepo kwa watoto kulikuwa ni kikwazo cha talaka kutolewa. Mume na mke wangeitwa kwenye baraza la wazee na kushauriwa sana kusameheana warejelee kwa majukumu yao ili kuondoa aibu kwa watoto na kwa jamii nzima. Baada ya kuridhiana wazee wangeshauri kondoo achinjwe kama ishara ya utakaso na ushirika mpya.

Iwapo mwanamume angezini na mke wa mtu mwingine angeadhibiwa kwa kuchapwa mijeledi mbele ya baraza la wazee na kisha kutozwa faini ya mbuzi kama kumi (Muriuki 1974). Iwapo mume wa mke aliyeziniwa angemsamehe, basi mzinifu angetoa mbuzi ambaye angechinjwa aliwe pale kwenye kikao na baraza wazee.

Bado katika suala la ndoa, ubikira wa msichana ulithaminiwa sana. Baada ya mahari kulipika kiasi kilichohitajika msichana alichukuliwa wakati wa jioni na kupelekwa kwenye chumba/nyumba ambayo ilikuwa imeshajengwa na mvulana (Kenyatta 1978:92). Ni baada ya kukaa huko na mumewe ndani ya nyumba ndipo walitarajiwa kushiriki katika tendo la ndoa. Mvulana alihitajika kutandika ngozi maalum ambayo ingetolewa nje kwa shangazi yake kudhihirisha kama ilikuwa na mabaka ya damu ambayo ingemaanisha msichana alivunjwa kizinda.

Mvulana na msichana walidadisiwa na shangazi ili kuona iwapo walikuwa na uwezo wa kuendeleza kizazi. Iwapo kungekuwa na shida, suala hilo lingeripotiwa kwenye baraza la wazee ambao wangetoa uamuzi wao katika kipindi cha wiki mbili. Ikiwa mambo yalikuwa sawa, basi kondoo angechinjwa na mafuta yake kupakwa yule msichana kama zindiko la kuzuia laana au mikosi kuingilia ndoa au kizazi chake. Hivyo basi mwanamke huyo alichukuliwa kuwa mwanachama wa matendo yote ya jamii au mbari hiyo na angeshiriki katika hafla zote za jamii zilizohitajika yeye kuwa.

Utafiti huu ulichunguza ni itikadi zipi zinazohusu masuala ya unyumba ambazo zinajitokeza kupitia lugha inayotumiwa katika nyimbo za harusi za Kikuyu.

## 4.2 Ubainifu wa Itikadi za Kimamlaka Katika Nyimbo za Harusi za Kikuyu Kutegemea Jinsia

### 4.2.1 Utangulizi

Wimbo ni utungo ulio na mdundo na mahadhi na huweza kuimbika. Nyimbo ni utanzu wa fasihi unaotumika sana katika jamii nyingi za ulimwengu katika miktadha tofauti tofauti. Miktadha kadha wa kadha ambayo nyimbo ziliimbwa ni kama wakati wa kazi, vita, mazishi, tohara, harusi, matanga na kadhalika. Kupitia kwa nyimbo jamii huweza kujifunza, ikajiburudisha, ikaomboleza, ikafarijiana na hata kupitisha taarifa za siri.

Nyimbo nyingi hueleza hisia za ndani za watu. Watu huweza kucheza kwa nguvu zao zote kufuatia mdundo wa ngoma. Kwa hakika mahadhi na mdundo wa katika wimbo huchochea wahusika kuchezesha sehemu zao za mwili. Nyimbo za harusi kwa hivyo bali na kuwa mirathi ya kitamaduni, huwa kama kitambulisho kwa wanajamii kama ilivyo lugha. Hivyo basi husaidia katika kuhifadhi na kuendeleza historia, falsafa, imani na hekima ya wanajamii. Kupitia nyimbo za harusi katika jamii ya Wakikuyu, mtazamo wao wa kimaisha kuhusiana na masuala ya ndoa au unyumba yanaweza kutambulika.

Katika harusi nyimbo huhusishwa na awamu tofauti tofauti kudhihirisha maudhui tofauti yanayoambatana na kaida na amali za jamii husika. Kwa madhumuni ya utafiti huu, mtafiti atabainisha itikadi za kimamlaka zinavyoibuliwa na nyimbo za harusi za Kikikuyu kwa namna ya ushawishi. Katika sura hii mtafiti ananukulu hoja na kuchanganua wimbo ulioimbwa katika awamu fulani ya harusi ili kupata itikadi halisi za jamii hii kuhusu mwanamke na mwanamume kutokana na nyimbo hizo.

Katika kuchanganua mtafiti anadokeza awamu tano muhimu katika harusi za Wakikuyu na kwa hivyo kuchanganua nyimbo tano za harusi ambazo zimeteuliwa kutoka kila awamu. Jinsi na hatua ambazo mtafiti alifuata kuchanganua data yake ni kama zifuatazo:

(i) Kutambulisha awamu: Mtafiti anatoa maelezo ya kina kuhusu awamu ya siku ya harusi.

(ii) Kuandika mfano wa wimbo ulioimbwa katika awamu hiyo.

(iii) Kutafsiri wimbo huo ulio katika lugha ya Kikuyu hadi lugha ya Kiswahili.

(iv) Mtafiti anatambulisha maudhui ya wimbo huo na kubainisha nyanja ya maisha inayolengwa na wimbo huo.

(v) Mtafiti anabainisha kwa maelezo ya kina jinsi lugha ilivyotumika katika kuwasilisha wimbo ule.

(vi) Mtafiti anabainisha jukumu na nafasi ya washiriki. Yaani fanani wa wimbo, washiriki na hadhira sikizi.

(vii) Mtafiti anabainisha maana ya wimbo ule kwa mujibu wa nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi na kubainisha ni itikadi zipi za kimamlaka ambazo zinaendelezwa na wimbo huo.

### 4.2.2 Awamu ya Bwana Harusi Kufika Nyumbani kwa Bibi Harusi Kumchukua.

Siku ya kufunga harusi ilipowadia mbari ya Bw. Harusi iliongoza Bw. Harusi kwenda kupokea Bi. Harusi kutoka nyumbani kwao hadi kwenye madhabahu au mahali ambapo wangefungia ndoa. Kundi la kina mama ndilo lilitangulia kuelekea uani kwa Bi. Harusi wakiimba nyimbo ili watambuliwe kwamba wamefika. Kulihitajika fanani ambaye ni gwiji katika kuongoza nyimbo huku wengine wakiitikia baada yake. Kina mama hawa wanawakilisha Bw. Harusi ambaye hufuata kwa nyuma bila kusema lolote. Kwa sauti ya juu wanahanikiza sauti zao angani ili wasikike na walio ndani. Huwa ni njia ya kujitambulisha kuwa wamefika.

Kwa upande wa ndani wa lango (uani kwa Bi.Harusi), kuna kundi lingine la kina mama ambalo linawakilisha mbari ya Bi. Harusi. Hawa nao vilevile huanza kuimba nyimbo zao kama majibizano na wale wa Bw. Harusi. **Kiambatisho I** ni mfano wa wimbo ulionukuliwa katika awamu hii.

Wimbo huu ni majibizano baina ya kundi la Bw. Harusi (a) na lile la Bi. Harusi (b). (a) wanajitambulisha kuwa wamefika uani kwa Bi. Harusi katika ubeti wa kwanza. Wanatoa sifa kwa mwenye boma kwa kutambua umuhimu wake uliowafanya wafike pale kwake. Wanamtambua kuwa alikuwa kifungua mimba na hivyo aliheshimiwa sana kuwa alikuwa amerithi uongozi wa

jamii hiyo kutoka kwa wazee wake. Upande wa ndani wanaamkuliwa na (b) ambao wanawashutumu kwa kuchelewa sana. Wanadai kwamba 'wamekataa kuja kupokelewa saa sita wafikapo kanisani misa ishakamilika'. Itafahamika kwamba mkesha wa kuamkia siku ya harusi, Bi. Harusi hulala akipambwa na kina mama huku akitiwa nakshi, waja na mapambo kemkem. Kwa hivyo shutuma zinazotolewa na kina mama hao huwa ni jazanda kudai kwamba wamekasirishwa na Bw. Harusi kuchelewa, lakini kwa hakika huwa wanataka wabembelezwe kwa kupewa kiinua mgongo na Bw. Harusi kwa kumpambia Bi. Harusi. Vilevile Bi. Harusi alikuwa akiwapikia alipokuwa huko na kwa hivyo ni sharti wafidiwe kwa vile hatakuwa akiwafanyia hivyo tena. Hii ndio sababu wanapoimba sehemu hiyo kundi la Bw. Harusi wamenyaza hadi wanapoambiwa wamefanya makosa kunyamaza. (a) nao huwarai (b) waje karibu ili wanong'onezane. (b) wanakubali (a) wakaribie ili wanong'onezane ambapo katika kule kunong'onezana kiasi fulani cha pesa hutolewa ili kuwatuliza kina mama na kuwarai wamfungulie Bi. Harusi mlango ili atolewe.

Nyanja ya maisha inayolengwa na wimbo huo ni kujenga uhusiano mwema baina ya wakwe ili waalike siku njema na mwanzo mwema kwa watoto wao ambao walitarajiwa kuunganishwa katika ndoa siku hiyo. Ni kweli wakwe kutoka kila pande walielewa fika umuhimu wa ndoa katika kuendeleza jamii hii. Kila mmoja alitazamia kutekeleza wajibu wake kuhakikisha kwamba wanao wameanza maisha ya mume na mke kwa mujibu wa utamaduni wa Wakikuyu (Kenyatta 87).

Lugha inayotumika ni sahili na yenye urudiaji mwingi hasa kwenye kiitikio ili kuleta mahadhi ya kimuziki. Ni lugha yenye kudhihirisha tasfida na mafumbo. Ni wimbo ambao unachanganya msamiati wa lugha ya Kiingereza hasa katika maneno *"welcome"* na *"sit down"* ambayo yanafanywa kutamkwa Kikikuyu kama *"welokamu"* na *"siti dauni"*. Hili linatokana na athari kubwa ambayo lugha ya Kiingereza iko nayo tangu maajilio ya wamishonari katika majanibu ya Wakikuyu.

Itikadi inayojitokeza ni kwamba Bi. Harusi anadhihirishwa kama *kitoto kichanga* ambacho kinahitaji kushikwa kwa ulaini na chenye kutunzwa. Hii ndio sababu waimbaji wanasema wamechoka kuvumilia miguu kwa kumuandaa Bi. Harusi ambaye kwa muda mrefu hajakujiwa na mumewe aende akamtunze na kumlinda. Hali hii inadhihirisha kwamba jamii ya Wakikuyu ilimpa mwanamume madaraka ya kulinda jamii yake hasa mke wake. Imani inayobainika wazi ni kwamba hakuna wakati ambapo mwanamke alihitajika kukaa bila kupewa ulinzi. Yaani alitakiwa kuwa chini ya mamlaka fulani ambayo kuna anayewajibikia maisha yake.

Hii ndio sababu awali msichana huyo anayeolewa alikuwa katika ulinzi wa babake hadi siku hii ya harusi ambayo anakabidhiwa kuwa chini ya mamlaka mumewe atakayekuwa mlinzi wake. Hii ni itikadi mojawapo inayojitokeza kupitia lugha kwamba hata waimbaji wenyewe ambao ni wanawake, wanafahamu kwamba kila mwanamke anafaa kuwa katika mamlaka ya mwanamume.

Itikadi nzito inayojitokeza katika wimbo huu ni kuwa Bi. Harusi anarejelewa kama *kana* (kijitoto). Kwa hivyo kuna mambo mengi ambayo mtoto hutarajiwa na 'watu wazima'. Mtoto hutarajiwa kutii na kuheshimu watu wakubwa. Anatakikana anapozungumza na watu wazima aongee kwa unyenyekevu. Zaidi huchukuliwa kwamba watoto hawajakomaa kufanya maamuzi dhabiti kwani akili zao bado ni changa. Utamaduni umewafanya wanawake kuelewa kuwa wao ni kama watoto. Isitoshe wanawake wenyewe wanaongoza kuimba nyimbo kama hizi za harusi zinazoendeleza itikadi zenye kuwalinganisha na watoto. Hii ndiyo sababu wanahisi kwamba kwa kuwa mtoto (Bi. Harusi) ambaye wamekuwa wakilea, sasa amekuja kuchukuliwa aende akatunzwe na mumewe ni kama mama anayenyang'anywa mwanawe. Katika dhana hiyo mwanamume anadhihirishwa kama *mtu mzima*. Yaani mtu ambaye amekomaa na aliye na maarifa ya kutoa maamuzi dhabiti. Hivyo basi huyu Bw. Harusi aliyekuja kumchukua Bi. Harusi alitazamwa kuwa na uwezo na mamlaka ya kutunza, kulinda na kikidhia *kitoto hiki*.

Washiriki katika wimbo huu ni wanawake. Wanawake hawa wametoka katika pande zote mbili za Bw. na Bi. Harusi. Muktadha wa uimbaji unatokea katika hali ya kubadilishana zamu usemi. Katika awamu hii ni rahisi kubainisha mgogoro unaojengwa na fanani kutoka kila pande huku washiriki wakiwaamkua kwa kukariri kiitikio cha wimbo. Ni mgogoro wa kimajibizano. Majibizano hayo hata hivyo kwa undani yanaongozwa na itikadi ya utamaduni inayodhihirisha jinsi mtu, hasa Bw. Harusi, anavyotakikana kufika kwa wakwe zake kwa adabu kuu na unyenyekevu. Ingawa kundi la Bw. Harusi ndilo hutanguliza wimbo kama ishara yao ya kuwasili katika himaya ya mkwe. Wimbo wao huwa ni kama mtu anayebisha hodi ugenini. Baadaye, fanani na waimbaji kutoka kundi la Bi. Harusi huchukua zamu ya kuwajibu lakini kwa ukali kiasi ili waweze kubembelezwa wafungue lango. Licha ya kuwa utoaji mahari ulikuwa ushatimizwa, wanawake waliokuwa wakimpamba Bi. Harusi hasa shangazi zake walihisi ni kana kwamba wananyang'anywa msichana wao. Hii ndio sababu wanakuwa miongoni mwa waimbaji wanaozuia kwenye lango. Jitihada zao ni kuhakikisha kwamba wamepewa kiinua mgongo kama ishara ya kuwafunga macho. Hali hii inadhihirishwa na usemi wa Kikuyu kwamba *sokwe anaponyang'anywa mtoto huwa anapewa mboko.* Mboko kilikuwa ni kubuyu chembamba

kilichotumiwa na Wakikuyu kubebea maji, uji au pombe hasa walipokuwa wakienda shambani au safari. Hivyo ilimaanisha kuwa walitaraji wapewe kitu ili waruhusu Bi. Harusi kuchukuliwa.

Aidha waimbaji hawa wote walikuwa ni wanawake. Sababu kuu ya kuwa na wanawake waimbaji ni kuwa wao ndio huchukuliwa kuwa ni walezi wa hawa watoto ambao kufikia awamu hii ya maisha yao wanaenda kuanza maisha na kuendeleza jamii kama mume na mke. Kwa hivyo wanawake ndio huonekana kuwa bora zaidi kuendeleza mafunzo ya kijamii kupitia kwa nyimbo. Vilevile sauti za wanawake hupendeza sana katika uimbaji. Wanaume wanapohitajika kuimba husisitiza kwamba sauti zao zinakoroma kama vyura. Kwa hivyo watulie ili wapishe wanawake kuimba.

Umuhimu wa wimbo huu unadhihirisha jinsi wanawake walivyokuwa na mamlaka ya kuongoza katika shughuli za harusi. Utamaduni umewatengea nafasi adimu ya kuunganisha mbari mbili kwa kupitisha matamanio ya kijamii kupitia kwa nyimbo. Wao vilevile wanaonekana kama watetezi wa mbari zao. Inaaminika kwamba mwanamke anapozungumza kwa unyenyekevu huweza kusikizwa na kuonewa huruma. Hii ndiyo sababu ule upinzani unaoibuliwa na kundi la Bi. Harusi unaweza kutulizwa na kulainishwa na wanawake kutoka kundi la Bw. Harusi kwa maneno yenye kurairai yenye kuomba wanong'onezane, wafanye urafiki hivi kwamba watu wengine wakiwaona washindwe walipendania wapi. Wimbo huu unajenga na kudumisha mahusiano baina ya familia ya Bw. na Bi. Harusi.

### 4.2.3 Awamu ya Kuungamanisha Bwana na Bibi Harusi

Katika awamu hii Bw. na Bi. Harusi hupelekwa kwenye madhabahu ambayo huchukuliwa kuwa ni mahali patakatifu pa kuabudu au kutekelezea shughuli maalum za kijamii. Kupitia kwa kasisi au mzee wa jamii, Bw. na Bi. Harusi hufanyiwa miviga fulani mbele ya wanajamii ambapo bado hupeana ahadi na kula kiapo cha ndoa. Anayeongoza shughuli hii huwahitaji maharusi hawa kurudiarudia usemi fulani anaowasomea. Usemi huu huaminika katika jamii hii kwamba unaposemwa na Bw. na Bi. Harusi kuukiri mbele ya hadhira, huwa wamekula yamini kuishi kama mume na mke kwenye ndoa. Baada ya hapo huwa ni maankuli na burudani. **Kiambatisho II** ni mfano wa wimbo unaoimbwa kushangilia Bw. na Bi. Harusi kwa kula kiapo cha ndoa.

Maudhui ya wimbo huu ni kusherehekea Bi. Harusi ambaye kufikia siku hii ametambuliwa kama mke kupitia ndoa. Wanawake wanaimba wimbo huu kwa furaha na

kushangilia kwingi. Wanacheza huku wakimshika mkono Bi. Harusi na kumtembezatembeza hapa na pale. Wanamsifu Bi. Harusi na kumwita *Gathigia. Gathigia alikuwa ni binti wa Gikuyu na Mumbi ambaye aliunda mbari ya Agathigia. Inaaminika kuwa huyu Gathigia alipenda kurejelewarejelewa sana na kutumbikiziwa sifa. Kwa hiyo fanani anatumia ufaraguzi katika wimbo huu ambao wanamsifu na kumfurahia Bi Harusi ambaye wanamtaja kwa jina lake *Wahito.

Lugha inayotumika inahusisha vitenzi vya kawaida kama *nikutembeze* na kihisishi cha kuomba radhi *Hebu*. Maneno hayo yanarudiwa sana hasa na washiriki wanaomuamkua fanani anapotanguliza. Maneno hayo kwa pamoja yanamrai na kumshawishi Bi. Harusi akubali kutembezwa na kina mama hawa waimbaji ambao wamefurahi kwamba wameongezeka ndio sababu wanamkaribisha Bi. Harusi. Katika tukio hili Bi. Harusi huenziwa na kuchukuliwa kama malkia. Hata hivyo wanapoendelea kumtembeza, wanamfahamisha atambue kwamba *umenye kindu no mwene*. Tasfiri ya usemi huo ni kuwa kila kitu kina mwenyewe. Pamoja na yote yale ya kumfurahia wanawake hawa waimbaji wanamfahamisha kuwa yeye sasa ana mwenyewe. Yaani amepata wa kummiliki. Wimbo huu unadhihirisha jinsi lugha inavyotumika kwa namna ya ushawishi kwa kumfanya Bi. Harusi afahamu kwamba yeye amekuwa milki ya mume baada ya kufunga ndoa hii. Ndio sababu Wodak (1989) anasema kwamba mamlaka hudhihirishwa kwa namna ya kidemokrasia ambapo kimsingi hailazimishwi, bali ni kwa namna ya ushawishi – ambayo ni itikadi. Itikadi inayoendelezwa na wimbo huu kwa namna ya ushawishi ni kwamba mwanamke anapoingia katika ndoa yeye anamilikiwa na mume aliyemuoa na vilevile jamii hiyo aliyojiunga nayo.

Vilevile lugha inatumia neno *kitu* kama jazanda kuashiria mwanamke – Bi. Harusi ambaye ni mali ya mume. Hii inashadidisha ile itikadi anayosema Kenyatta (1978) kuwa mwanamume pindi alipotoa mahari basi alionekana kama aliyenunua yule mke. Hii ndiyo humpatia mwanamume mamlaka ya kumiliki kile alichonunua kwa mbuzi na ng'ombe ambazo ndizo zilikuwa mali iliyoenziwa na jamii hii ya Wakikuyu.

Waimbaji katika wimbo huu vilevile ni wanawake kama ilivyokuwa katika wimbo wa kwanza. Wao wana jukumu kubwa la kumkaribisha Bi. Harusi katika maisha ya kijamii kama mke na kiambajengo cha kuendeleza kizazi cha jamii ya Wakikuyu. Wanawake huona fahari kwa Bi. Harusi aliyejiunga nao kutekeleza majukumu ya kijamii. Majukumu hayo ni kama yale ya kupata watoto na kuendeleza jamii, kupikia na kutunza familia yake na kufanya kazi nyinginezo huku akilindwa na mumewe. Kwa kumfahamisha kwamba *kindu no mwene*, Bi. Harusi alitarajiwa

kumheshimu mumewe na kufanya analotaka mumewe kwa unyenyekevu ili wasiwe na ugomvi baina yao kama ishara ya kuwa yeye ni wa mume. Baadhi ya majukumu hayo yote ndiyo ambayo mtoto wa kike alikuwa akifunzwa na mamake pindi alipokuwa akinenepa, ambapo kupatikana tena katika wimbo kama huu ni kama ukumbusho wa yale aliyofunzwa tayari.

Msamiati unaotumika pia una sababu zake. *"Huku ni kwa nani?"*. Huku ni kiwakilishi kionyeshi cha mahali. Anayeuliza ni kundi la Bw. Harusi ambao wanauliza kwa balagha kama ishara ya kujitambulisha kuwa wamefika. Kisha wanataka *kujibwaga*. Hiki ni kitenzi kinachoonyesha ujasiri wa kutaka kufanya atakalo. Katika ubeti wa pili, wanajibiwa kwamba *Huku ni kwetu* kama ishara ya kuwatambua na kisha kuwaruhusu *wajibwage kama ndama wa nyati*. Hii ni ishara ya kuwaruhusu wafanye watakalo. Katika maisha ya jamii ya Wakikuyu, wao hufuga ng'ombe na hivyo nyati ni mnyama mkubwa na mkali katika jamii ya wanyama sampuli ya ng'ombe. Nyati ana mamlaka zaidi akilinganishwa na ng'ombe. Kwa hivyo Bw. Harusi anatambuliwa na kupewa uhuru na mamlaka ya kufanya atakalo kama alivyo ndama wa nyati anavyolindwa na kundi zima la nyati. Hali hii basi inaonyesha jinsi itikadi ya kumtwika Bw. Harusi mamlaka inavyokuzwa kwa kutumia lugha.

Ubeti wa tatu unatambua kwamba Bi. Harusi *alilelewa kwa maziwa na nyama*. Maziwa na nyama ni jazanda ya aina ya vyakula na vinywaji vilivyothaminiwa sana katika jamii ya Wakikuyu. Uwezo wa kumiliki mifugo ulilinganishwa na familia tajiri na yenye bidii. Hii ndiyo sababu familia hiyo ingeweza kulisha watoto wake kwa maziwa na nyama ndipo wakawa na afya nzuri. Hii ni ishara ya kusema kuwa Bi. Harusi huyo ni mwenye afya nzuri na wa kutamaniwa. Wanajibu katika ubeti wa nne kuwa ni sharti *anunuliwe kwa mbuzi na ng'ombe*. Kenyatta (1978) anasisitiza kuwa mbuzi na ng'ombe wengi ndiyo mali ambayo ilithaminiwa sana mtu kuwa tajiri akiwa nayo. Idadi fulani ya mbuzi na ng'ombe ingetolewa kama mahari kwa msichana anayeolewa. Lengo lilikuwa ni kufidia malezi kwa familia ya msichana atakayeondoka. Hali hii huelekea kutoa itikadi kwamba msichana au Bi. Harusi kuwa thamani yake ni mbuzi na ng'ombe. Vilevile dhana ya kitenzi "*anunuliwe*" inalete fikra ya mwenye kutoa mahari kuhisi kuwa alinunua na hivyo kumiliki na kuwa na haki za matumizi ya alichonunua. Itikadi kama hii inaweza kusababisha tofauti kubwa za kimamlaka.

#### 4.2.4 Awamu ya Kusherehekea Bw. na Bi. Harusi Kufanya ndoa

Katika awamu hii, Bw. na Bi. Harusi huimbiwa nyimbo nyingi za kuwatumbuiza hasa kutokana na kitendo chao cha kufanya ndoa. Kundi la wanawake waimbaji wakiongozwa na fanani huwachukua Bw. na Bi. Harusi kutoka mahali walipotengenezewa jukwaa na kuwapeleka uwanjani ambako huwahusisha katika ngoma na densi zilizo na nyimbo za kuwasherehekea kwa kufanya ndoa. Kando na kuwa nyimbo hizi ni za kuwaburudisha, bado zinabeba maudhui makuu yanayoendeleza itikadi nzito za jamii hii kuhusiana na masuala yanayohusu mamlaka ya mume na mke katika ndoa. **Kiambatisho III** ni mfano wa wimbo ulionukuliwa katika awamu hii kwenye tukio la harusi.

Maudhui ya wimbo huu ni kushangilia Bw. na Bi. Harusi kwa kufunga ndoa. Waimbaji wanaanza kila aya kwa kujidai kuwa wao kama kizazi cha Mbari ya Gathigia, hukanyaga kama majeshi. Ishara ya majeshi ni ujasiri wa kutotishika na hivyo wanaenzi mwanao ambaye amefunga ndoa na kwa kuleta mke. Basi amefanya ukoo huu kuendelea. Mwanamke alipoolewa aliweza kujiunga na ukoo wa mume na hivyo kizazi atakachoendeleza kitadumisha ukoo wa mumewe. Linalojitokeza wazi pia katika nyimbo hizi ni kuwa ingawa zinaimbwa katika muktadha maalum wa ndoa, zimefungamanishwa pakubwa na masuala ya kihistoria ya jamii hii.

Wimbo huu unapochanganuliwa kwa uhakiki unadhihirisha dhana nzito. Lugha inayotumika kwanza inampongeza sana Bw. Harusi anayerejelewa kwa jina lake kama *Mutugi. Anapongezwa kwa kupewa shukrani na hata kupigiwa saluti. Hii inafananishwa na jinsi jemedali wa kikosi cha majeshi anapopigiwa saluti na kikosi anachoongoza. Ifahamike kwamba waimbaji wale ni wanawake ambao wanatembezatembeza Bw. na Bi. Harusi huku wakiwashangilia kwa nyimbo. Katika kucheza zile nyimbo ndipo inabainika kupitia lugha jinsi wanawake wanavyomtwika Bw. Harusi mamlaka ya kuwaongoza sawia na jemedali wa majeshi.

Aidha shukrani nyingi anazopewa Bw. Harusi ni kwa sababu ya kuletea wale wanawake (waimbaji) mwanamke mwingine ambaye kulingana nao atakuwa akitekeleza majukumu kadhaa kama vile: kukamua mifugo maziwa, kuchuma kahawa, kutia mpini na hata kuzalisha kina mama. Hizi ni baadhi ya kazi ambazo jamii ya Wakikuyu hujihusisha nazo katika kujikimu kimaisha. Hii inadhihirisha itikadi ambayo Kenyatta (1978) anataja kwamba mwanamke Mkikuyu alitarajiwa kuwa mwenye bidii kazini na hata angesisitiza kufanya kazi nzito hata kuliko mwanamume. Katika kazi zinazorejelewa na wimbo huo ni ile ya kutunza mifugo ndio sababu wanawake wanafurahi eti Bi. Harusi atakuwa akikama mifugo. Bila shaka ili kufikia kiwango cha kukamua

mifugo maziwa inagharimu kazi nyingi ya kuwalisha na kuwatunza ndiposa wapate maziwa ambayo ingekamuliwa. Aidha Bi. Harusi anatarajiwa atakuwa akichuma kahawa. Haya ni mazao ya shambani na ambapo ukuzaji wa kahawa hadi kufikia msimu wa kuchuma huwa una kazi nyingi za kulimia, kutia mbolea, kunyunyizia dawa za kuangamiza viwavi ili mazao ya kahawa yapatikane. Kwa hivyo hizi ni kazi ambazo zinahitaji mtu mwenye bidii sana.

Kazi nyingi zinazorejewa na wimbo huu ni zile ambazo zilikuwa zikitekelezwa na wanaume. Hata hivyo wimbo huu unaoimbwa na wanawake katika harusi unadhihirisha matarajio ambayo mwanamke (Bi. Harusi) anatarajiwa kuwa akitekeleza baada ya kuwa mke wa Bw. Harusi. Wimbo unaendelea kutaja kwamba, hata mpini Bi. Harusi atatia. Hii inamaanisha kuwa katika harakati za kuendelea na kazi huko shambani, iwapo mpini unaweza kuvunjika, mwanamke hahitaji kungojea usaidizi wa mwanamume – atatia mwenyewe. Hii inaleta jazanda anayotaja Kenyatta (1978) ya *Mutumia Mwihoti* (mwanamke anayejiweza). Yaani mwanamke mkakamavu na mwenye bidii kazini hivi kwamba hakuna jambo ambalo hawezi kutekeleza.

Vilevile jukumu lingine analotarajiwa kuwa akitekeleza Bi. Harusi ni kushirikiana na wanawake wengine panapotokea uhitaji kama vile harakati za mwanamke kujifungua mtoto. Fanani katika wimbo huu anauliza kwa balagha iwapo wakienda kwa mkunga iwapo watahitaji wa kuwanyoa. Ni swali ambalo linaulizwa kwa tasfida kwa maana ya kwamba kwa kuwa wamepata Bi. Harusi basi yeye ndiye atakayekuwa akiwanyoa wanapojifungua. Kwa hivyo wimbo huu unadhihirisha kwamba Bi. Harusi anatarajiwa awe mtaalam pia katika masuala ya ukunga ili endapo mwanamke yeyote atahitaji kujifungua, basi wasiwe na shaka kwamba wako na mtaalam katika shughuli za ukunga.

Lugha ambayo imetumika katika wimbo huu inachanganya vitenzi vya kawaida, tashibihi, jazanda na pia takriri nyingi. Ni lugha inayodhihirisha wazi jinsi itikadi za mamlaka zinavyoendelezwa kupitia nyimbo za harusi kwa namna ya ushawishi mkubwa na hivyo kuathiri pakubwa akili za wanajamii kuhusu majukumu yao yanayobainishwa kijisia. Lililo wazi ni kwamba jamii imekubali majukumu au mamlaka yanayotwikwa mume au mke hivi kwamba kuna njia nyingi za kufikia wanajamii wengine mafunzo hayo nyimbo za harusi zikiwa ni miongoni mwa njia hizo. Kutokana na ule urudiaji katika wimbo basi mahadhi ya wimbo huwezesha wimbo ule uweze kunata katika bongo za wasikilizaji na hivyo polepole kuathiri matendo yao.

Washiriki au waimbaji katika wimbo huu ni wanawake ambao ndio wanakuja kuwachukua Bw. na Bi. Harusi kutoka mahali walikoketi na kuanza kuwatembezatembeza

mzunguko huku wakiwaimbia nyimbo za shangwe kwa kufunga ndoa. Aliye mwanamume miongoni mwao ni Bw. Harusi pekee. Ni nadra sana kuona wanaume wakijumuika pamoja na wanawake kuimbia Bw. na Bi. Harusi. Wanaume hupendelea kukaa kitako wakiwatazama wanawake wao wakitumbuiza.

### 4.2.5 Awamu ya Kutoa Ushauri Kwa Bw. na Bi. Harusi.

Katika awamu hii, huwa kuna ushauri unaotolewa kwa Bw. na Bi. Harusi kuwahimiza katika mambo ya ndoa. Watu ambao wameonekana kuwa kielelezo katika ndoa huombwa kutoa ushauri kwa hawa wanaooana. Hivyo basi katika awamu hii aghalabu hotuba hutolewa zikihimiza umuhimu wa kuvumiliana, kuwajibikiana na kupendana katika maisha mapya ya ndoa. Mzungumzaji mmoja anaweza kusimama na kushauri Bw. Harusi huku mwingine akisisimama baadaye na kumshauri Bi. Harusi. Ushauri mwingi sana huwa hautolewi hapa ikitarajiwa kuwa ushauri mwingi kuhusu majukumu anayotarajiwa kila mmoja katika ndoa yalishatolewa zamani kwa kila mmoja, walipokuwa wakipitia miviga ya kuwafanya watu wazima kama vile tohara. Kwa hivyo mengi husemwa tu kwa namna ya muhtasari sana. Hata hivyo nyimbo zilizo na ushauri huweza kutolewa pia katika awamu hii. **Kiambatisho IV** ni mfano mmojawapo wa wimbo ulionukuliwa katika awamu hii.

Maudhui ya wimbo huu ni kuhimiza mume kuwajibika ili kufanikisha ndoa hasa kwa kuwa mwaminifu au kutokuwa na jicho la nje. Ni wimbo ambao unashirikisha itikadi ya Kikiristo na hata kuchukua malighafi ya Biblia Takatifu kwa mfano katika kitabu cha Mwanzo 2:18 ambapo ndipo Mungu alitazama na kuona kwamba si vizuri mwanamume aishi peke yake kwa upweke. Ndipo akaamua kumuumbia mwenzi. Imani katika dini ya Kikristo imefungamanishwa sana na itikadi ya Kikikuyu ambayo hutambua kuwa mwanamke aliumbwa kutoka kwa mwanamume ili amnufaishe mwanamume huyo. Hivyo basi kurejelea ile dhana ambayo Kenyatta (1978) anasema kwamba pindi mwanamume aliweza kutoa mahari ya mifugo waliohitajika basi alikuwa ndiye alitazamiwa kummiliki na kutunza mwanamke huyo kama mume wake.

Lugha inayotumika katika wimbo huu ni shawishi mno. Ni wimbo ambao unaanza kwa kuenzi mwanamume kwa kumfahamisha eti jinsi Mungu alivyomchungulia akiwa juu na kuona kwamba anahitaji mwenzi ndipo basi akamuumbia mwanamke. Imani inayomhusisha Mungu inaibua itikadi ambazo wanajamii katika jamii ya Wakikuyu huhitajika kuamini bila kuuliza

maswali. Ni imani ambayo inamdhihirisha mwanamke kama sehemu ya mwanamume na hivyo kuwa anamilikiwa na mwanamume kama anayemfaa ili waishi pamoja.

Kiitikio cha wimbo huu kinamshawishi mwanamume kumchunga mke wake na kumkidhia mahitaji yake kama mavazi mema ili arembeke na lishe bora ili awe na siha nzuri yenye kutamanika. Lugha iliyotumika inasisitiza kuwa endapo mwanamume atafanya hivyo basi hawezi kuwa na jicho la nje. Dhana ya mume kuchunga mke wake katika wimbo huu inaendeleza itikadi ya mamlaka ya mwanamume kuwa ni mlinzi kwa mwanamke. Kwamba mwanamke ni mtu anayehitaji kulindwa ili mambo mabaya yasimfike. Vilevile itikadi ya mwanamke kujidumisha kama mtu mrembo mwenye kuvutia inaendelezwa. Kinyume chake kikiwa ni chenye kudhihirisha kwamba endapo mwanamke hatakuwa mrembo, msafi na mwenye siha nzuri huenda ikachochea mwanamume kuwa na jicho la nje. Kupitia uchanganuzi hakiki wa nadharia hii, kinachojitokeza ni kwamba ushauri huu unaenda kwa mwanamke pia. Ni kama kumweleza mwanamke atunze mwili wake kwa kujinadhifisha na kujipamba au kujirembesha vyema, kula vyakula vyenye kuboresha siha yake ili aweze kumnata mumewe asije akavutiwa na wanawake wengine. Baadhi ya ushauri unaotolewa katika wimbo huu ni baadhi ya mambo ambayo vijana walikuwa wakishauriwa kuhusu majukumu yao ya kijamii wakati walipokuwa wakipitia awamu muhimu kama vile unyago na jando. Hili ni dhihirisho la kwamba nyimbo za harusi za kikikuyu huendeleza itikadi zinazobainisha mamlaka ya kijinsia. Kwamba mwanamume anafaa kumlinda mkewe naye mke anastahili kutunza na kumfurahisha mumewe kwa aina tofauti ili asije akawa na jicho la nje. Hivi ni kumaanisha kana kwamba endapo mwanamume atakuwa mzinifu, uwezekano mkubwa ni kwamba mkewe hakuwajibika kutekeleza majukumu yake kikamilifu kama anavyotakikana kijamii.

Aya ya tatu ya wimbo huu inahimiza mwanamume awe akikumbuka kwamba katika dunia nzima hakuna mwanamke mwingine ambaye ni mzuri kushinda mke huyo aliyeona akamchagua. Lugha inayotumika hapa inadhihaki uwezekano wa mume kutamani mwanamke mwingine kando na mkewe. Ni lugha shawishi inayomsisitizia mwanamume afahamu kwamba mwanamke anayefanya naye harusi aliumbwa kwa ajiri yake. Tena itikadi inayojitokeza hapa ni ile inayomfanya mwanamume kuamini kwamba aliumbiwa mwanamke. Yaani mwanamke yuko kwa manufaa ya mwanamume. Itikadi hiyo ndiyo hufanya mwanamume aamini kuwa mwanamke anatakikana aishi kumfurahisha na kumtunza mwanamume ili asije akakasirika.

Aya ya nne vilevile inaonya mume kutotamani mke wa mwingine aliyevishwa vyema akarembeka. Lugha inayotumika inamshawishi mume kumnunulia mkewe mavazi bora ili naye awe mrembo na mwenye kuvutia macho ya mumewe yasije yakaona wanawake wa nje. Kwa uhakiki zaidi, wimbo huu unaelekea kumwangazia mwanamume kama mtu ambaye mapenzi yake kwa mwanamke yanaathiriwa sanasana na kile anachoona. Ni wimbo ambao haudhihirishi ikiwa mapenzi ya mwanamume kama yanatokana na hisia za moyoni. Kwa mujibu wa historia ya utamaduni wa jamii ya Wakikuyu, suala la mwanamume kuoa wanawake wengi lilikuwa ni halali almuradi mume huyo angedhihirisha kuwamudu kwa kuwakidhia mahitaji yao. Ingawa tangu dini ya Kikristo ilipokuja katika janibu hizi za Wakikuyu yapata karne ya 18, itikadi hii imekuwa yenye kupigwa vita sana. Pengine ndio sababu lugha inayotumika katika wimbo huu inakashifu sana tamaa ambayo inaweza kumvutia mume kuwa na jicho la nje kwa wanawake wengine.

Kulingana na wimbo huu wanawake watajaribu kila namna kuhakikisha kwamba wamewafurahisha wanaume ili wasihusike na masuala nje ya ndoa. Kauli inayodhihirika na wimbo huu inashabihiana na utafiti aliofanya Dutto (1975:123) huko mjini Nyeri kwamba, wanawake wengi walioolewa ni waaminifu kwa waume wao. Lakini kulingana na Dutto (ibid) wanaume wengi huwa na uhusiano nje ya ndoa. Lugha inayotumika katika wimbo huu inakashifu sana tabia zinazoweza kuelekeza katika uhusiano nje ya ndoa.

Washiriki katika wimbo huu ni wanaume. Wanashirikisha Bw. na Bi Harusi katika kucheza huku wakiendelea kuimba kwa kucheza dansi. Fanani ambaye ni mwanamume analenga kumshauri Bw. Harusi moja kwa moja kwa wimbo huu. Hata hivyo tumedhihirisha kuwa kwa njia isiyo ya wazi ni wimbo unaolenga pia Bi. Harusi. Fanani katika wimbo huu anawakilisha wanaume Wakikuyu ambao hasa wameathirika pakubwa na dini ya Kikristo. Kupitia lugha anayotumia katika wimbo huu inabainika kwamba itikadi kuhusu mume na mke kidini zinavyoshabihiana na itikadi za mila ya Wakikuyu kuhusu majukumu ya mume na mke katika ndoa. Hasa anaposema katika aya ya kwanza kwamba Mungu alichungulia akiwa juu akaona si vyema mwanamume kuishi peke yake kwa upweke ndiposa akamuumbia mwanamke. Kumaanisha kuwa mke ni wa mume. Itikadi hiyo ni sawia na itikadi ya Kikikuyu ambayo anadhihirisha Kenyatta (1978) kwamba mwanamume aliweza kumiliki mke pindi alipolipa mahari. Hivyo basi fanani ama waimbaji hawa ambao ni wazaliwa wa jamii hii ya Wakikuyu, wamekulia na kujengeka kwa itikadi hii kwamba mke ni milki ya mwanamume.

Fanani anapotoa ushauri kupitia wimbo huu anakuwa kama kiwakilishi cha jamii hii ya Wakikuyu inayompa mawaidha Bw. Harusi. Anapopinga dhana ya kuwa na jicho la nje, anadhihirisha hoja ambayo imetolewa na utafiti huu katika sura ya nne kuhusu amali ya ndoa, kwamba wazee wa jamii ya Wakikuyu wanalinganisha kuwa na wake wenza sawa na *jungu mbili za uchawi* (Chomba 2005). Yaani wazee wa jamii hii hushauri kuwa ni hatari sana kuoa wake wawili. Kwamba familia yenye wake wenza huishi kwa ugomvi ambao hufikia hata vizazi vyao. Hii ndio sababu fanani katika wimbo huu anakashifu suala la mwanamume kutamani mwanamke mwingine. Hili ni dhihirisho kuwa lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za Kikikuyu huendeleza itikadi nyingi zinazohusu mamlaka ambayo yanatarajiwa kwa mume na mke.

Kwa hivyo washiriki katika wimbo huu wanadhihirisha jinsi utamaduni wa Wakikuyu unavyoathiri wanajamii hii katika usemi wao. Inabainika kwamba fanani anapoongoza wimbo huu amali za mila na desturi zinaoenziwa na Wakikuyu zinajitokeza kwa undani.

**4.2.6 Awamu ya Kutoa Zawadi kwa Bw. na Bi Harusi.**

Awamu hii huwa ni kilele cha shughuli za harusi. Shughuli ambazo huanza asubuhi hivi kwamba kufikia wakati huu machweo huwa imekaribia. Huenda wakati wa usiku kukawa kumeandaliwa ngoma au densi ingawa huwa sio lazima. Baada ya watu kutoa zawadi zao basi shughuli za harusi huwa zimekamilika. Watu hubeba zawadi tofauti tofauti za kupatia Bw. na Bi. Harusi. Baadhi ya zawadi huwa ni jazanda inayogumbika maana fiche. Kuna aina ya zawadi maalum ambazo hutolewa na kundi au watu fulani katika jamii hii ya Wakikuyu. Kwa mfano, mtu anaweza kuona wazee wa Bw. Harusi wakimkabidhi mkuki, ngao na upanga. Vifaa hivi ni jazanda ya silaha ambazo jamii ya Wakikuyu ilikuwa ikitumia wakati wa kupigana na kujikinga katika vita. Silaha hizi hutolewa kama ishara ya mamlaka ambayo Bw. Harusi anapewa ya kumlinda mkewe na familia yake kwa jumla. Vilevile unaweza kugundua wazee wakimpa Bw. Harusi bakora. Bakora ni mkongojo ambao uliashiria madaraka. Mathalani wanaume walipokuwa wakijumuika kwenye baraza la wazee kujadiri masuala ya kijamii, kila mwanamume alikuwa na bakora kwa mkono. Hii inaashiria kuwa mwanamume baada ya kufunga ndoa angeweza kutambulika kuwa na mamlaka ya uongozi zaidi ya mwanamume ambaye bado hajaoa. Vilevile Bw. Harusi angepewa bidhaa zingine hata akavalishwa ngozi maalum na kofia maalum zilizovalishwa viongozi. Hii ilikuwa ni ishara kuwa Bw. Harusi amepewa mamlaka ya kuongoza familia na hata jamii ya Wakikuyu kwa jumla.

Kwa upande mwingine, wazazi wa Bi. Harusi ndio hutoa zawadi ya kitanda. Katika jamii hii ya Wakikuyu kuna itikadi au imani nyingi zinazohusishwa na kitanda kinachopeanwa katika ndoa. **Kiambatisho V** ni mojawapo wa nyimbo zinazoimbwa katika awamu hii ya kutoa zawadi ambao ulinukuliwa katika tukio la harusi.

Wimbo huu unaimbwa na ukoo au mbari ambayo Bi. Harusi ametoka. Kupeanwa kwa kitanda na wazazi wa msichana huwa ni taashira inayoashiria kuwa kufikia sasa Bi. Harusi ameondolewa kabisa katika boma la babake na kukabidhiwa mumewe. Kitanda huwa ni ishara inayoonyesha kuwa msichana hana mizizi tena ya kumuunganisha na familia ya babake. Iwapo ataenda kwao basi atatambuliwa kama mgeni. Maudhui ya wimbo huu kwa hivyo ni kuaga Bi. Harusi kutoka kwa wazazi wake.

Fanani katika wimbo huu anatanguliza wimbo huu huku nao washiriki wakiamkua kwa kukariri kiitikio *gwata ndai* (kitendawili tega) kila baada ya sentensi. Kisha wote kwa pamoja hurudia kiitikio pamoja. Lugha iliyotumika katika wimbo huu ni yenye tasfida na mafumbo ambayo yanasimbikwa kama kitendawili ambacho Bi. Harusi anategewa ili ategue. Fanani anaeleza kwamba wamemsindikiza na endapo atakuja kutembea kwao basi akiambiwa akalale mvunguni mwa kitanda hafai kukasirika kwani kitanda chake ndicho hicho hapo. Hii ni ishara kwamba nyumbani kwao hakuna tena mahali pake pa kulala.

Vilevile wimbo huu unaendelea kumsisitizia Bi. Harusi kuwa kwa sasa wamempatia kitanda kwa hivyo amfungate mumewe *"unyitie muthuri"*. Lugha nzito inatumika katika wimbo huu kumshauri Bi. Harusi atumie kitanda hiki kumfungata mumewe kwa maana ya kufanya mapenzi. Itikadi katika jamii hii ilichukulia kuwa kitanda hiki cha ndoa ni kitakatifu na kinafaa kutumiwa na mume na mke kwani ni kupitia kwacho watoto watapatikana. Vilevile raha zote za ndoa baina ya mume na mke zinastahili kushirikianwa kwenye kitanda hiki. Hii ndio sababu Bi. Harusi anaambiwa kitanda ndicho hicho amfungate mumewe. Yaani kwa raha ambazo Bi. Harusi atampa mumewe ndizo zitamfunga katika ndoa hiyo asije akatamani kwengine. Kwa hivyo itikadi kuhusiana na kitanda hiki cha ndoa ni kwamba mwanamke au Bi. Harusi anapewa mamlaka ya kuendesha mapenzi baina yake na mumewe. Dhana inayojitokeza hapa ni kwamba mwanamke anachukuliwa kuwa ni kiini cha kuimarika kwa ndoa yake na mumewe kwani anatakikana amtosheleze mahitaji ya kimwili mumewe. Hiyo ndiyo maana halisi ya nahau yeye *amfungate mumewe (unyitie muthuri)*. Usemi huo wa Kikuyu *unyitie muthuri* unamaanisha kuwa mke ni *amfunge* kwa nguvu mumewe kwa shughuli za kitanda kile. Kinyume chake ni kwamba

asipomfungata atalegea na huenda aanguke nje ya ndoa. Jambo ambalo linaweza kupelekea kuporomoka kwa ndoa yenyewe. Ni kama kumwambia Bi. Harusi kwamba asipomtumikia mumewe kabisa kwenye kitanda basi huenda mumewe akamwacha. Kwa hivyo usemi huo unaendeleza itikadi nzito kwamba mwanamke anatakikana ahakikishe amedhibiti ndoa yake pamoja kwa kumkidhia mume mahitaji ya ngono kwa utoshelevu kwenye kitanda kile. Bi harusi huwa amepewa mamlaka ya kuendeleza kizazi kwa watoto atakaojifungua ambao hutarajiwa kuwa watapatikana kutokana na ushirika atakaokuwa nao kwenye kitanda hiki maalum.

Mwanamke analinganishwa na kitanda kile kwamba majukumu yake yatakuwa ni kulaliwa sawia na jinsi kile kitanda kinavyolaliwa. Mamlaka makuu yanaenda kwa mume ambaye atakuwa akijistarehesha kwa kumlalia mkewe. Jinsi kitanda kinavyoleta starehe kwa kulaliwa ndivyo dhana hiyo inavyosawiriwa kwa mwanamke anayepewa kitanda na wazazi wake aende nacho kwa mumewe. Maisha ya mume na mke katika jamii ya Wakikuyu yanahusishwa sana na suala la kitanda. Kitanda huwekwa katika chumba cha faragha ambacho mume na mke hulala. Hivyo basi yanayotendwa ndani ya chumba kile hufaa kubaki yakiwa ni siri tu ya wawili wale. Hata hivyo jamii huchunguza matendo ya mume na mke huko nje na iwapo kuna yeyote atakayeonekana akitupa jicho kwingine basi jamii hukisia kwamba masuala ya mume na mke kwa kitanda hayaendi vyema.

Hiyo ndiyo sababu wanapomwambia mke afungate mumewe katika kile kitanda kwa namna ya kufumba kitendawili, wanamaanisha kuwa mwanamke anastahili kumpa mumewe mapenzi bila kupimapima ili aweze kutulia katika ndoa hiyo hasa kupitia katika tendo la ngono. Hivyo basi mwanamke amepewa mamlaka ya kudhibiti ndoa yake kwa kuhakikisha anatekeleza jukumu lake hilo kwa mumewe. Kwa hivyo mwanamke huelewa wazi jukumu lake kwa mumewe ni lipi kuhusiana na kitanda.

Kwa kuwa Bw. na Bi. Harusi wanapewa kitanda hiki mbele ya hadhira ambao huwa ni mashahidi wa kushuhudia kuwa mume na mke huyo ndio halali tu kulalia kitanda kile, basi ilikuwa ni mwiko sana kuwepo hali kwamba mtu mwingine nje ya ndoa anaweza kuletwa na mmoja wao wakalala kwenye kile kitanda. Ingechukuliwa kuwa ni haramu kwa mtu mwingine kuletwa kisiri na aitha Bw. au Bi. Harusi kulala pamoja kwenye kitanda kile. Ni katika kitanda hiki ambacho watoto ambao wangezaliwa walikuwa wamekubalika na wakabarikiwa na wazee wa jamii hii.

Itikadi nyingine inayosimbikwa na dhana hii ya kusindikiza Bi. Harusi kwa kitanda ni kwamba ndoa ilitarajiwa kuwa ni mkataba wa kudumu maisha baina ya mume na mke na hivyo suala la talaka au utengano lilikuwa halitazamiwi kamwe. Jamii ya Wakikuyu huthamini ndoa sana hivi kwamba kabla ya mvulana na msichana wafike kiwango cha kufunga ndoa, wao huhitajika wathibitishe kwa ukamilifu mbele ya baraza la wazee kutoka pande zote kuwa wako tayari kuishi pamoja kama mke na mume. Ni kupitia awamu ambazo familia ya Bw. Harusi walikuwa wakienda kupeleka mahari kwa kina Bi. Harusi ambapo wote wawili walikuwa wakidhihirisha wako tayari kuishi pamoja kama mke na mume. Kwa hivyo azma ya mwanamke na mwanamume kuishi kama mke na mume haikutokana na uamuzi wa dharura. Lilikuwa ni suala ambalo walikuwa na ushauri na msimamo thabiti kulihusu. Msimamo ambao ulitokana na mawaidha ya tangu utotoni ambayo kila mmoja alikuwa akielimishwa kuhusu matarajio ambayo jamii yake ilikuwa ikimtarajia kwa misingi ya kijinsia. Itakumbukwa kwamba kila mwanajamii alitazamia kuoa ama kuolewa na kupata watoto ili aendeleze jamii yake. Vilevile kulikuwa na msamiati ghasi sana uliotumiwa kuelezea watu ambao walionekana kuwa na kasoro katika majukumu ya ndoa au waliokosa kushiriki katika ndoa. Mtu ambaye angetimia umri wa kuoa kisha akose kuoa huku rika lake lote wakioa, basi yeye alitengwa na kuonekana mwenye dosari.

Kwa kuwa kila mwanajamii alitazamia kuondoka nyumbani kwa wazazi wake aende akaanze familia yake, basi dhana hii ya kitanda ilikuwa ni jazanda iliyomaanisha kuwa binti amepewa ruhusa kuondoka kwao na hangetarajiwa tena kuita kwa babake kuwa ni kwake tena. Itikadi hii inafungamana sana na ile imani kutoka kwa familia ya Gikuyu na Mumbi ambao walipooza binti zao waliwaruhusu waondoke waende sehemu tofauti tofauti wazaane ili wajaze dunia. Kwa mujibu wa kisasili hicho cha Gikuyu na Mumbi, Wakikuyu huthamini ndoa sana na huamini kwamba mtu hafai kurejea kwa wazazi wake pindi anapoolewa. Yaani haitakikani arudi kwa wazazi wake kutokana na talaka bali arudi kama mgeni. Hivyo basi wimbo huu unadhihirisha kwamba athari za kihistoria kuhusu imani za kitamaduni za Wakikuyu zinaendelezwa kupitia kwa nyimbo za harusi.

Washiriki katika wimbo huu ni wanawake. Wao ndio wanamwimbia Bi. Harusi. Inaelekea kwamba jamii imewafanya kutambua kuwa jukumu lao katika ndoa huegemea sana ushirika watakaopatia waume wao. Ni kupitia wimbo huu ambapo inabainika kwamba wanawake wenyewe wanaendeleza itikadi za kimamlaka ambazo tayari zimejengeka akilini mwao. Wanaonekana kuamini kuwa ni sharti wawajibike kufanya mapenzi na waume wao kiasi cha

kuridhisha mwanamume. Aidha inaelekea kwamba wanaamini mwanamke *asipomfungata mume* kwa mapenzi huenda mumewe akashiriki mapenzi kwingine. Inaelekea kumaanisha kwamba wanawake hawa waimbaji wanaweza kuamini kuwa iwapo mume anaweza kuwa na jicho la nje, lawama hizo zinaweza kutokana na hali ya mkewe kutomkidhia mahitaji ya kimapenzi katika ndoa. Hii ndiyo sababu waimbaji hawa wanawake wanatoa tahadhari kwa Bi. Harusi kupitia wimbo huu kwamba kwa kuwa wamempa kitanda basi amfungate mumewe (*unyitie muthuri*).

## 4.3 Muhtasari wa Uchanganuzi Huu

### 4.3.1 Lugha

Nyimbo hizi zinadhihirisha matumizi tofauti ya lugha. Jinsi lugha inavyotumika kurejelea mwanamume na mwanamke inadhirisha wazi tofauti kubwa ya kijinsia. Nomino *kana* (kijitoto) imetumika kurejelea mwanamke – Bi. Harusi. Bila shaka Bi. Harusi si mtoto na hivyo nomino hiyo inakuwa ni jazanda inayomtambulisha mwanamke sawa na mtoto. Hii ndiyo sababu Bi. Harusi anakabidhiwa mumewe ambaye atakuwa akimchunga au kumwongoza sawa na jinsi mtoto anavyoelekezwa na mtu mzima. Ni muhimu kutambua kuwa neno hili pia liko katika hali ya udogo. Katika hali ya wastani neno mtoto lingetumika. Aidha neno hili linamdhirisha mwanamke kama mtu asiye na maarifa huku mwanamume akitambulishwa kama mwenye maarifa au busara na pia mlinzi. Imani hiyo inaweza kuibua mkinzano mkubwa hasa wakati mwanamke anapotaka kudadisi mambo fulani ilhali mwanamume anaamini kwamba mwanamke ni wa kuambiwa mambo.

Kuna msemo *kindu no mwene* (kila kitu kina mwenyewe) unalenga kumfahamisha mwanamke kuwa yeye ni milki ya mwanamume. Kwamba kila kitu kina yule anayekimiliki. Yaani mwanamke yuko chini ya mamlaka ya mwanamume. Kwa maana pana, hali hiyo inampa mwanamume mamlaka ya kutumia kile anachokimiliki kwa namna anayotamani.

Tashibihi inatumika kudhihirisha mamlaka ya uongozi. Waimbaji wanamtukuza Bw. Harusi kwa kumpigia saluti na kumwambia *wakanyage kama majeshi*. Mwanamume anapongezwa kwa kuleta mke na hivyo kufanya jamii hii kuongezeka. Wanawake wa jamii hii wanamtukuza mwanamume huyu ambaye amewaletea mfanyikazi atakayekuwa akitunza mifugo, akifanya kazi shambani na pia kazi za nyumbani. Lugha katika nyimbo hizi pia inambainisha mke kama

mfanyikazi. Mwanamume anabainishwa kwa madaraka sawa na kamanda au jemedali wa majeshi. Hali hii inabaisha jinsi lugha inavyobainisha itikadi tofauti za kijinsia.

Nyimbo hizi pia zinatumia lugha yenye mafumbo yaliyo kwenye jazanda. Waimbaji wanamfumbia Bi. Harusi kitendawili ambacho anatarajiwa ajitegulie. Ni fumbo lililo kwenye dhana ya *kitanda* ambacho Bi. Harusi hupewa kama zawadi na wazazi au ukoo wake. Kitanda ni taashira inayoashiria mambo mengi. Kwanza, inaashiria kuwa Bi. Harusi amehama kwao daima. Ameacha ukoo wake na kwenda kujiunga na ukoo wa mume. Pili, Bi. Harusi hushauriwa afanikishe ndoa yake kwa kuhakikisha kwamba amemfungata mumewe kwa mapenzi. Aidha kitanda hicho huwa ni jazanda ya chanzo cha kizazi kipya kitakachoendeleza jamii hii. Kwa hivyo ni kitanda kinachoheshimiwa na huhitajika kutakaswa ili kusiwe na laana katika familia hii mpya.

Ni lugha inayotumia vitenzi na vivumishi vya kawaida lakini vyenye kuwakilisha itikadi nzito. Mwanamke anatarajiwa kudumisha urembo ili kuhakikisha mumewe anafurahia asije akatamani mwanamke mwingine. Hakuna mahali ambapo nyimbo hizi zinaeleza kuhusu mwanamume kijipamba ndio afurahishe mkewe. Hazitaji kamwe.

Lugha inayotumika ni shawishi mno. Mwanamke anashawishika kuamini kuwa yeye aliumbwa kwa minajili ya mwanamume. Hali hii inashajiishwa na imani ya kidini hasa dini ya Kikristo ambayo imekolea sana katika maeneo ya Wakikuyu. Ajabu ni kwamba waimbaji wengi wa nyimbo hizi za harusi ni wanawake. Inadhihirika kuwa wameathirika katika akili na itikadi hizo hivi kwamba wao wenyewe ndio wanaimbia Bi. Harusi na kumfahamisha majukumu anayotarajiwa na jamii hii.

Jedwali lifuatalo linaonyesha baadhi ya istilahi za lugha na jinsi zilivyotumika katika nyimbo zilizochanganuliwa.

**Jedwali 2. Istilahi za Lugha Zilizotumiwa Katika Nyimbo za Harusi za Kikuyu.**

| **Istilahi** | **Mfano kutoka kwa wimbo** | **Maana inayohusishwa nayo** |
|---|---|---|
| Nomino | (a) Maziwa na nyama | Vitu vya thamani vinavyotumiwa kwa malezi ya mtoto. Watu wanaolea kutumia vitu hivi ni wenye bidii na hivyo Bi. Harusi anahimizwa kuwa na bidii kazini ili aweze kumiliki mifugo wengi ndiposa amudu kulea wanawe kwa lishe bora. |

| | | |
|---|---|---|
| | (b) Mbuzi na ng'ombe | Ni mifugo wanaothaminiwa sana ambao humpa anayemiliki mamlaka na hadhi mbele ya wengine. Vilevile vinaashiria thamani ya mwanamke kwani ndio hutumiwa kulipia mahari yake. |
| | (c) Kitoto (udogo wa Mtoto) | Ni nomino inayomrejelea Bi. Harusi (mwanamke) kama mtu dhaifu anayepaswa kutunzwa kwa umakini na tahadhari nyingi na mwanamume. |
| Sitiari | (a) Kitanda | Dhana ya kitanda inatumiwa kurejelea jukumu la mwanamke ni kumfurahisha mwanamume kitandani kwa kufanya kitendo cha ngono. Aidha hali ya kitanda kulaliwa inampa mwanamume mamlaka ya kulalia mwanamke wake. |
| | (b) Ndama wa nyati | Istilahi hii inawashiria mwanamume kama mwenye mamlaka ya kufanya atakavyo. Sifa inayojitokeza ni ile ya kujionyesha kwa wengine kuwa Bw. Harusi ni mwenye uwezo na hivyo amemudu kulipa mahari ya mkewe. |
| Msemo | (a) Kitu huwa na mmiliki | Ni tafsiri kutoka *kindu no mwene* (kwa Kikuyu) kumaanisha kila kitu huwa na mmiliki wake. Neno kitu linamrejelea mwanamke ambaye kufikia wakati wa harusi amepata mmiliki. Vilevile neno hilo linamaanisha sehemu fulani ya mwili wa mwanamke ambayo kupitia shughuli ya ndoa imepata mmiliki. Hivyo basi mwanamume anapewa mamlaka ya kummiliki mkewe. |
| | (b) Kemi za wanaume hufanywa wanapokula nyama tu | Wanaume wanadhihirishwa kama watu ambao hufurahi sana (kutoa kemi) wakati wanakula nyama. Hivyo ni nadra sana kwa wanaume kudhihirisha furaha iliyokithiri hasa kwa kupata mke. Suala la ndoa kwa mwanamume huchukuliwa kama kawaida kulitenda ili kuwa mkamilifu katika jamii ya Wakikuyu (Kenyatta |

| | | |
|---|---|---|
| | | 1978:87). |
| Tashibihi | (a) hukanyaga kama majeshi | Bw. Harusi anaambiwa akanyage kama majeshi kwa kufanya jambo zuri la kuletea jamii yake mwanamke atakayekuwa akifanya kazi tofauti zilizotajwa. Mwanamume anapewa mamlaka kama alivyo jemedali wa majeshi wanaomtukuza. |
| Kitenzi | (a) alinunuliwa | Kenyatta (1978: 38) anasema kitendo cha mwanamume kukamilisha kulipa mahari husemekana kuwa 'amenunua' kwani mbuzi na ng'ombe huwa wameshatolewa. Dhana hii ya kununua inampa Bw. Harusi mamlaka na uwezo mkubwa wa kudhibiti kile alichonunua. Lugha hii inadhihirisha itikadi kuwa mwanamke ni milki ya mumewe. |
| | (b) nijibwage | Hiki ni kitendo kinachomaanisha kujiangusha kwa nguvu ili kutoa kishindo. Ni kitendo kinachofanywa kwa maksudi kwa namna ya kujionyesha au kutaka utambulisho. Katika Kiambatisho II, wimbo unamrejelea Bw. Harusi ambaye anataka kujibwaga mbele ya watu ili watambue kuwa amepata mke. Yaani kudhihirisha mamlaka na uwezo wa kupata mke. Ni kitendo cha kuonyesha ushujaa kwa wengine. |
| | (c) umfungate | Kitenzi hiki kinaambiwa Bi. Harusi baada ya kupewa zawadi ya kitanda ili akitumie kumbana au kuzuia mumewe asisambaratike au kutoka nje ya ndoa. Yaani amfunge mumewe kwa kitendo cha ngono ili asije akawa na jicho la nje. |
| Kiwakilishi | (a) huku ni kwa nani? | Kiwakilishi 'huku' kinaulizwa katika swali la balagha ambapo wanaouliza ni kundi la Bw. Harusi kama ishara ya kujitambulisha kwa wengine. Ni dhana inayoonyesha kuwa Bw. Harusi kama mwenye mamlaka ya usemaji na hivyo angetaka kila mmoja atambue hilo. |

Lugha inayotumika kurejelea mwanamume na mwanamke inaidhinisha tofauti kubwa ya kijinsia.

**Jedwali 3. Tofauti Baina ya Mwanamume na Mwanamke Inavyobainika Katika Nyimbo za Harusi za Kikuyu**

| Mwanamume | Mwanamke |
|---|---|
| Mtu mzima | Kijitoto (hali ya udogo ya mtoto) |
| Mwenye hekima | Asiye na hekima nyingi |
| Mlinzi | Wa kulindwa |
| Ni mmiliki wa mke | Ni milki ya mume |
| Jemedali | Mtumishi au mfanyakazi |
| Mwenye mamlaka katika shughuli za nje | Mwenye mamlaka katika shughuli za nyumba |
| Mwamuzi wa mambo | Mshauri |
| Mwenye kukidhia mahitaji ya familia | Mwenye kutunza na kuhakikisha utumiaji bora |

### 4.3.2 Maudhui

Maudhui makuu yanayojitokeza katika nyimbo tano zilizochanganuliwa katika awamu hizo tano tofauti yanajikita katika ndoa, kazi, utawala na umiliki wa mali.

Kuhusiana na ndoa, mwanamke alitarajiwa kumtii mumewe. Thamani kubwa ya mwanamke ilipimwa kwa mizani ya urembo na uwezo wa kuzaa. Kama inavyobainika katika nyimbo hizi mwanamke alitarajiwa sana kumfurahisha mumewe na pia aweze kuendeleza jamii kwa kupata watoto. Mume alitarajiwa kulinda mkewe na kumkidhia mahitaji ya pale nyumbani.

Kuhusu kazi, mwanamke anatarajiwa kulisha na kutunza familia yake. Vilevile kuna kazi nyingi sana ambazo mwanamke anatarajiwa kufanya kama vile kulima shambani na kutunza mifugo na kushirikiana na wanawake wengine katika kazi za ukunga. Uwezo wa mwanamke kutekeleza kazi tofauti tofauti ndio hubainisha bidii yake. Mwanamke hutarajiwa kuwa na bidii sana kazini ili aweze kufunza familia yake umuhimu wa kazi na vilevile yeye mwenyewe kuwa kielelezo mwafaka katika utenda kazi.

Katika kuzingatia maudhui ya utawala, nyimbo hizi zinambainisha mwanamke kama mtu anayestahili kulindwa. Maisha ya mwanamke yanaonekana kuwa chini ya utawala fulani. Katika

utotoni mwanamke (msichana) huwa katika ulinzi wa babake na anapoolewa hukabidhiwa mumewe ambaye hutakikana aishi chini ya mamlaka yake. Hivyo mamlaka ya uongozi yamepewa mwanamume. Nyimbo hizi zinabainisha hayo zinapomrejelea mwanamke kama mtoto (*kana*) na hata anapokabidhiwa mumewe dhana ya kumchukulia kama mtoto huenda ikaendelea kujengeka akilini mwa wanaume.

Kuhusiana na maudhui ya umilikaji mali, inadhihirika wazi kupitia nyimbo hizi kwamba mwanamke hana chake wala kwao kwani wazazi wake wameshampeana kwa kubadilisha na mahari inayolipwa. Nyimbo hizi zinamdhihirisha mwanamke kama milki ya mwanamume aliyemuoa. Hii inamaanisha kuwa mali atakayopata mke kwa bidii zake kazini itakuwa ni mali ya familia nzima. Mke hufunzwa kwamba kilicho chake ni cha mumewe kwani yeye pamoja na watoto wake ni hazina inayomtambulisha mumewe.

### 4.3.3 Maana

Maana ya kijumla iliyojitokeza kuhusu itikadi zenye mamlaka ya kijinsia ni kwamba lugha inatumika sana kuendeleza tofauti za kijinsia kupitia kwa nyimbo za harusi za jamii hii Ni kupitia kwa uchanganuzi wa nyimbo hizo ambapo tunagundua kwamba wanawake na wanaume walikuwa na majukumu waliyotarajiwa kila mmoja kutekeleza katika ndoa. Inaelekea kwamba njia zilizotumika kufunzia kila jinsia majukumu yake zilikuwa na sifa za kipekee. Mfano wa njia hizo ulikuwa ni kupitia kwa nyimbo ambazo zilitumia lugha yenye ushawishi mkubwa sana. Lugha ambayo imetumika katika nyimbo za harusi za Kikikuyu imedhihirika kuwa na sifa zenye kuathiri sana fikra za wanajamii katika jamii hii. Kwa mfano mwanamke alitarajiwa kuwa mtiifu kwa mumewe, kuwa chini ya mamlaka ya mumewe, kutunza familia yake kwa kuipikia na kufunza watoto mkondo wa tabia unaokubalika. Pia mwanamke alitarajiwa kuwa mwenye bidii kazini; katika kazi za nyumbani na za shambani. Naye mwanamume alitarajiwa kutoa ulinzi kwa familia yake, kukidhia familia kwa mahitaji ya chakula na mavazi. Vilevile mume alitarajiwa kuwa kiongozi katika familia hiyo kwa kufanya maamuzi ya mambo atakayohitaji familia ifanye. Mwanamume alihitajika kutoa mwongozo wa maadili ya jamii nzima.

Kinachobainika ni kwamba jamii hii imekubali majukumu haya kwani katika nyimbo tano zilizochanganuliwa asilimia 80% ziliimbwa na wanawake wakiwaimbia Bw. na Bi. Harusi. Wanawaimbia kuwafahamisha majukumu ambayo kila mmoja anatarajiwa kutekeleza katika kufanikisha maisha yao ya ndoa. Wanaume wanaimba wimbo mmoja tu katika tukio nzima la

harusi ambalo kwa mujibu wa nyimbo zilizochanganuliwa ni asilimia 20%. Ingawa ni wimbo unaolenga kumshauri mwanamume bado kwa uchanganuzi hakiki unalenga kufahamisha zaidi mwanamke jinsi anavyostahiki kufanya amfurahishe mumewe ndiposa ndoa yao idumu.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ataeleza maswala muhimu yaliyoibuka kutokana na utafiti huu. Aidha mtafiti atagusia matatizo na ufanisi wa utafiti. Hatimaye ametoa mapendekezo ambayo yanaweza kuelekeza kwenye sehemu zinazohitaji utafiti wa ziada.

## 5.2 Hitimisho

Kupitia utafiti huu ilibainika kwamba jamii ya Wakikuyu hupitisha na kuwarithisha wanajamii wake thamani na amali ambazo husimbikwa katika lugha wanayoitumia. Nyimbo za harusi zilizochanganuliwa zinaafiki ukweli wa nadharia tete ya kwanza inayodai kuwa lugha inayotumika katika nyimbo za harusi za Kikuyu ina sifa maalum. Maelezo ya uchanganuzi katika kila awamu pamoja na maelezo katika ibara 5.7.1 yanadhihirisha kwa kina jinsi istilahi fulani za lugha zinavyotumika kubebea maana iliyofichika. Kuna matumizi mengi ya lugha kama vile nomino, misemo, tashibihi, jazanda na hata vitenzi ambavyo vimetumika kuelezea itikadi fulani zinazoenziwa na jamii ya Wakikuyu.

Itikadi zinazobainika kupitia kwa nyimbo hizi ni kwamba:

(i) Jamii ya Wakikuyu ilihitaji mume na mke wawe wenye bidii kazini ili waweze kuzalisha mali nyingi ndiposa wamudu kuwapa wanao malezi mema.

(ii) Mwanamke alifaa kujua yeye ni milki ya mwanamume aliyemuoa.

(iii) Mwanamume ndiye kiongozi wa familia na hivyo anahitaji kuheshimiwa na maagizo yake kufuatwa.

(iv) Mwanamume anafaa kulinda na kukidhia mahitaji ya familia yake.

(v) Mwanamke anastahili kuhakikisha kuwa familia yake wamekula na wako na afya jema.

(vi) Mwanamke anastahili kufunza wanawe jinsi ya kutenda kazi ili wapate maarifa ya kazi.

(vii) Mwanamke anaonyeshwa kama mtu anayestahili kumtegemea mwanamume kwa ulinzi au usalama wake.

(viii) Mwanamume anabainishwa kama mtu wa kutoka kwenda kutafuta, mwenye nguvu kwa kazi nzito na anayestahili kufanikiwa ilia pate cha kuleta nyumbani.

Lugha vilevile inatumika katika nyimbo za harusi kuendeleza itikadi tofauti za jamii ya Wakikuyu. Hilo linathibitisha nadharia tete ya pili inayodai kwamba nyimbo za harusi huendeleza

itikadi katika jamii ya Wakikuyu. Mathalan, nyimbo hizi zinaendeleza itikadi inayofanya jamii kuamini na kukubali kwamba mwanamke aliumbwa kwa minajili ya mwanamume. Vilevile mwanamke anapoolewa huwa hana mizizi kwao tena kwani huhama huko na kubadilisha ukoo wake akajiunga na ukoo wa mumewe. Itikadi nyingine inayobainika kupitia nyimbo za harusi ni kwamba mwanamke na mwanamume katika jamii hii hawakutakikana kuwa na uvivu. Hivyo bidii kazini ilifaa kuonyeshwa kwa vitendo na hata kufunzwa watoto. Jamii ya Wakikuyu huchukulia kuwa ni mwiko na aibu kwa mtu kuwa na tabia ya kuombaomba wengine ilhali yeye ana akili timamu, uwezo na nguvu za kufanya kazi. Itikadi hizi zinabainika wazi kwenye nyimbo hizo hasa waimbaji wanapomwimbia Bi. Harusi na kumkaribisha katika maisha ya ndoa. Wanataja baadhi ya kazi tofauti tofauti atakazokuwa akifanya. Wakikuyu huamini kwamba utajiri hutafutwa na mtu anaweza kupata chochote atakacho maishani almuradi asilaze damu.

Jamii ya Wakikuyu huamini katika mgao wa mamlaka katika familia. Baba ama mume ndiye huaminika kuwa kiongozi wa familia (Kenyatta 1978:5). Mama ama mke huwa ndiye wa pili kwa mamlaka wakati mumewe hayupo. Itikadi hii inaendelezwa na hata huweza kubainika kupitia nyimbo zilizochanganuliwa za harusi. Kila mwanajamii huonekana kuafikiana na hilo na kuamini kwamba kila mara katika taasisi yoyote hata ya ndoa ni sharti pawe na kiongozi ambaye ana mamlaka na ushawishi ili maisha yaweze kuendeshwa bila mizozo na ugomvi. Nyimbo hizi zinabainisha itikadi hii na kutambua mwanamke kama kiongozi wa familia yake.

Mwanamume na mwanamke katika ndoa walikuwa na majukumu yaliyokuwa wazi kwa kila mmoja. Nyimbo zilizochanganuliwa zinabainisha wazi mamlaka ya kijinsia ambayo mume na mke walitarajiwa kutekeleza. Hili linathibitisha nadharia tete ya tatu inayosema kuwa nyimbo za harusi za Kikuyu huendeleza mamlaka ya kijinsia. Mwanamume alikuwa ndiye kiongozi wa familia. Mwanamke alitarajiwa kumheshimu na kunyenyekea kwake. Heshima hiyo ilitarajiwa ingefanya waweze kuwa na masikilizano yasiyo na ugomvi. Kwa kuwa ndoa ni baina ya mume na mke, jamii hii iliona ni sharti pawe na mmoja mwenye mamlaka zaidi kwani waliona kwamba watu wawili wanapoanza kubishana kuhusu jambo moja, ingekuwa ni vigumu kuwa na maelewano. Inavyoelekea basi wao huchukulia kuwa ili kuepukana na hali ya ushindani baina wa mke na mume ni vyema mume anatoa kauli ya mwisho.

Mwanamume alitazamiwa kutoa ulinzi kwa mkewe na familia nzima na pia kukidhia mahitaji ya nyumba ya mkewe (Muriuki 1974). Kwa upande mwingine mwanamke alitarajiwa kupikia na kutunza familia yake, kufanya kazi kwa bidii pamoja na mumewe ili waweze

kuimarisha maisha yao. Pia alitarajiwa kuongoza na kuimarisha jukumu la kufanya mapenzi na mumewe ili ndoa yao iwe na faraja.

Inabainika kupitia uchanganuzi hakiki wa nyimbo hizo kwamba jamii hii ilijizoesha na kuwa na tajiriba katika mambo hayo ambayo yalithaminiwa na kupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kinachobainika ni kwamba jinsia zote huonekana kurithika na amali zao hata wanaporithisha wengine wanaoingia katika ndoa. Hivi ndivyo mtafiti na msomi Wodak (2001) anaeleza kwamba kuna itikadi za mamlaka ya kijinsia ambazo huendelezwa katika jamii pasipo kutumia nguvu lakini kupitia njia zenye ushawishi. Nyimbo zilizochanganuliwa zinadhihirisha hali hiyo inayotumia lugha kwa namna yenye ushawishi mwingi kupitisha itikadi zinazohusu mamlaka ya kijinsia baina ya wanaume na wanawake katika jamii ya Wakikuyu.

## 5.3 Changamoto Zilizomkabili Mtafiti

Changamoto kubwa ilikuwa katika kutafsiri matini za nyimbo kutoka lugha asilia ya Kikuyu hadi Kiswahili kwa manufaa ya kazi hii. Baadhi ya dhana katika lugha ya Kikuyu zilikosa visawe kamili katika lugha ya Kiswahili. Ilibidi mahali pengine kuwa na maneno mengi. Lugha ya Kikuyu huwa na viambishi vingi kwenye vitenzi ambavyo hupelekea kuwa na maneno mawili au matatu katika Kiswahili. Kiimbo na kidatu pia kilikuwa ni shida kulinganisha katika wimbo asilia na wimbo uliotafsiriwa. Hata hivyo mtafiti alijaribu uwezo wake na kuleta uwiano wa matini katika lugha chanzi na lugha pokezi.

## 5.4 Mapendekezo

Kuna mambo mengi muhimu ambayo yanadhihirika kutokana na utafiti huu. Mtafiti aligundua kuwa nyimbo za harusi zinapambanua thamani za ndoa ambazo jamii ya Wakikuyu ilithamini sana kama mihimili ya kufanya ndoa iimarike na kudumu. Wakikuyu, sawa na jamii nyingi za kiafrika, walifuata taratibu nyingi sana kabla ya mwanamume na mwanamke kukubaliwa kuishi kama mume na mke. Ni kupitia taratibu hizo ambazo walifunzwa masuala halisi yanayohusu ndoa na mambo ambayo hutatiza ndoa na hivyo kujiepusha nayo. Ni kweli kwamba lugha ndiyo hutumika kutolea mafunzo hayo. Jamii ya Wakikuyu haikupendelea talaka hata kidogo. Wao waliamini kwamba familia hujengwa na mume na mke kwa kushirikiana.

Kufikia karne ya 21 kumekuwa na wasomi na watafiti wengi wanaochunguza lugha inayotumiwa kurejelea mwanamke na mwanamume. Wamegundua kuwa mwanamke

anadhulumiwa sana na mwanamume na wakati mwingine kuteswa kwa kufanyiwa matendo mabaya yanayojitokeza katika lugha. Watafiti hao wakawa wenye kuonea mwanamke huruma. Mwanamke akawa anaonekana kama kiumbe dhaifu. Katika kujikomboa wanawake wamehisi ni sharti wadhihirishe kuwepo kwao. Baadhi yao waliegemea nadharia ya Ufeministi wakawa wanatumia istilahi kali dhidi ya mwanamume. Kufikia sasa kumekuwa na mvutano mkubwa baina ya jinsia hizi mbili za ulimwengu. Hakuna jinsia inayotaka kuregeza kuwa chini ya ile nyingine. Makabiliano hayo yamepelekea wanawake kudai haki sawa na wanaume katika nyanja tofauti za kimaisha kama vile katika ajira, elimu, matibabu, ndoa na kadhalika.

Inaelekea kuwa kuliko jinsia hizi mbili kulaumiana na kutumia msamiati usiofaa kuelezea jinsia nyingine, ingefaa sana kutambua kuwa kila jinsia ina upekee wake ambao ni tofauti na ile nyingine. Ni muhimu jamii na hata Wizara ya Elimu ihakikishe kuwa vitabu vinavyochapishwa havitambui jinsia moja kwa uovu huku vikitukuza jinsia nyingine. Ni sharti taasisi tofauti tofauti za kijamii zijitahidi kuelimisha jamii umuhimu wa kuonea fahari jinsia zetu na kutobagua jinsia nyingine. Mafunzo yanayotolewa na lugha inayotumika inafaa iwe kwa namna ambayo itadhihirisha kuwa jinsia hizi mbili zinakamilishana na moja ni muhimu kwa nyingine.

Kwa kuwa tafiti zinazohusu masuala na itikadi za kijinsia ni changamano kwani wakati mwingine ni vigumu mtafiti kujiepusha na athari ya jinsia yake, ni vizuri wanaotafiti wajaribu kuziba mwanya uliowekwa na wasomi wanaopendelea tu jinsia moja huku wakionyesha nyingine kuwa ni mbaya. Kwa kufanya hivyo itakuwa ni sawa na kuzika shimo moja kwa udongo uliochimbwa shimo lingine.

Ni muhimu kutahadhari katika mazungumzo kwani lugha huweza kukuza na kuendeleza itikadi ambazo zinaweza kufasiriwa kwa maana tofauti tofauti na mpokeaji na hivyo kuathiri maana.

## MAREJELEO


Brown, G. and Yule, G. (1993). *Discourse Analysis.* Cambridge: Cambridge University Press.

Bottignole, S. (1984). *Kikuyu Traditional Culture and Christianity.* Nairobi:Heinemann Educational Books.

Chacha, N.C. (1982). *Mke Mwenza.* Nairobi: Heinemann Educational Publishers.

Chesaina, C. (1987). "Women in Africa drama: representation and role". Tasnifu ya PhD, School of English University of deeds (Haijachapishwa).

Chomba, E.N. (2005). "Usawiri wa Mwanamke katika Methali za Kikuyu." Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Egerton (Haijachapishwa).

Chomsky, N. (1965). *Syntactic Structures.* The Hague: Mouton.

Collins, H.P. (1991). *Black Feminist Though.* New York: Chapman and Hall Inc.

Dutto, C.A. (1975). *Nyeri Townsmen Kenya.* Nairobi: East African Literature Bureau.

Eagleton, M. (1996). *Feminist Literary Theory.* New York: Basil and Blackwell.

Engels, F. (1975). *The Origin of the Family, Private Property and State.* Moscow: Pathfinder Press.

Fairclough, N. (1992). *Critical Language Awareness.* (ed) Essex: Longman.

Fairclough, N. (1992). *Discourse and Social Change.* London: Polity Press.

Fairclough, N. (1989). *Language and Power.* Harlow: Longman.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa.* NewYork: Oxford University Press.

Halliday, M.A. (1978). *Language as Social Semiotics: The Interpretation of Language and Meaning.* London: Heinemann Publishers.

Izugbara, C. (2005). *Hypothesis on the Origin of Hegemonic Masculinity, in Sexuality.* In. African Magazine. Lagos: African Regional Sexuality Resource Centre 2(1): 13 – 14.

Kabira, W. na Mutahi, K. (1993). *Gikuyu Oral Literature.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Kendall, G. (2007). *What is Critical Discourse Analysis?* Ruth Wodak in Conversation with Gavin Kendall [38 paragraphs]. Forum: Qualitative Social Research. 8(2). Art. 29. http://www.qualitative-research.net/fqs-texte/2-07/07-2-29-e.htm.

Kenyatta, J. (1978). *Facing Mount Kenya.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Kerre, R. (1989). *God Meets Us. Christian Religious Education* . Nairobi: East African Educational Publishers.

Kipury, N. (1983). *Oral Literature of the Maasai.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Lugano, R.S. (1989). "Mwanamke katika riwaya za Kezilahabi", Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Maclenness, J. (1998). *The end of Masculinity.* Buckingham: Open University Press.

Materu, M. (1982). "The Image of Women in Tanzania Oral Literature", Makala katika Kiswahili Toleo 49/2. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mbiti, S.J. (1969). *African Religions and Philosophy.* Nairobi: Heinemann.

Mbughuni, P. (1982). "The Image of Women in Kiswahili Prose Fiction". Makala katika Kiswahili, Toleo 49/1. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Milroy, J. (1987). *Observing and Analysing Natural Language.* London: Basil Blackwell Publishers.

Mugenda, O. and Mugenda, A. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Act Press.

Mule, K. (1991), Swala la mwanamke katika Tamthilia ya Kiswahili; Waandishi wa kike katika njia panda. Tasnifu ya M.A chuo Kikuu cha Kenyatta.

Munene, W.A. (1995). "*Muramati Mugikuyu*". Nairobi: East African Educational Publishers.

Muriuki, G. (1974). *A History of the Kikuyu, 1500 – 1900.* Nairobi. Oxford University Press.

Nida, E.A. (1964). *Towards a Science of Translating.* London: E.J. Brill.

Onyango, J.O. (2007). "Masculinities in Kiswahili Children's Literature in Kenya". Katika SWAHILI FORUM 14:245-254.

Onyango, J.O. (2008). " The Masculine Discursive Construction of Rape in the Kenyan Press". Katika, *Masculinities in Contemporary Africa* - Egodi Uchendu, Codesria Gender Institute: pg 54.

Okindo, A.O. (1995). Sura ya mwanamke katika methali za Ekegusii. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Egerton.

Nyerere, J. (1985). Utangulizi katika, "The Arusha Stategies for the Development of Women in Africa, OAU."

Richmond, A.M. (1992). *Masculinity and Feminine: Gender Role Over the Life Cycle.* NewYork: Mc Graw Hill Inc.

Sankan, S.S. (1971). *The Maasai.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Senkoro, P. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press Publicity Centre.

Taban, L.L. (1972). *Popular Culture of Eastern Africa Oral Literature.* Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Thiong'o, N.T. (1970). *The River between.* Nairobi: Heinmann Kenya Ltd.

Timammy, R. (2002). A Stylistics Analysis of Swahili Wedding songs of Mombasa. M.A Thesis, University of Nairobi (Unpublished).

Tracy, D. (1806). What is Ideology? http://www.answer.com/library/ Britannica_Concise_Encyclopedia

T.U.K.I (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

T.U.K.I (1996). *English Kiswahili Dictionary.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Uchendu, E. (2005). " Masculinity from perspective of Youth." Paper presented at the Gender Institute of CODESRIA.

Van Dijk, T. (1997). *Discourse as Social Interaction.* London: Sage Publications.

Wandera, S.P. (1996). "Ushairi wa Kiswahili 1800 – 1900 Uhalisia au Ugandamizaji?" Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Egerton (haijachapishwa).

West, G. and Rhoda, L. (1990). *Women and Social Protest.* Oxford: Oxford University Press.

Wodak, R. (2007). "Editorial: Language and Ideology – Language in Ideology". *Journal of Language and Politics* 6/1, 1- 6.

________ (2007). "Pragmatics and Critical Discourse Analysis. A Cross Disciplinary Analysis". *.Pragmatics and Cognition. 15:1, 203 – 225.*

________ (2006). "Critical Linguistics and Critical Discourse Analysis". *Handbook of Pragmatics,* Benjamins.

________ (2006). "Mediation between Discourse and Society: Assessing Cognitive Approaches." *Discourse Studies* 8:1 pp 179 – 190.

________ ( 2001). "The Discourse Historical Approach." In Wodak and Meyer, (eds.) *Methods of Critical Discourse Analysis: Introducing Qualitative Methods.* London, Thousand Oaks and New Delhi, Sage Publications. Pp 63-95.

________ (1989). ed., *Language Power and Ideology: Studies in Political Discourse*. London: Benjamins Publishing Company.

## VIAMBATISHO

Zifuatazo ni nyimbo zilizofanyiwa uchanganuzi katika awamu tofauti tofauti kwenye shughuli za harusi. Matini zenyewe ziko katika lugha asilia ya Kikuyu na tafasiri ya kila wimbo katika Kiswahili.

### KIAMBATISHO I

**Wimbo katika Awamu ya Bwana Harusi Kufika Nyumbani kwa Bibi Harusi Kumchukua**

| Fanani | Washiriki |
|---|---|
| *(a)* *Menya gũkũ nĩkuo kwa ndeha* | *welokamu* |
| *Mwene arĩ irigithathi* | *welokamu* |
| *Welokamu na wakinya kwa Kĩragũ* | *siti dauni* |
| *(b)* *(i) Nĩndarega kũmĩrĩrĩa magũrũ* | *Nĩtwarega* |
| *Nĩndarega* | |
| *Nĩndarega* | |
| *kũgĩragwo thaa thita* | |
| *tũgikinya kanithainĩ* | |
| *magongona mathomirwo. (kiitikio)* | |
| *(ii) Nĩũcereirwo naniĩ njĩkĩte na ciĩko* | *nĩndarega* |
| *(iii) Na nĩ kana nĩko karia gaitũ* | *nĩtwarega* |
| *(iv) No tugire nĩ mahitia nĩ mwakira na tiwega* | *nĩndarega.* |

*(a)*

*Twendane aai*
*Twendane aai*
*Andũ matuona*
*Moragie twendanĩire kũ. (kiitikio)*

| | |
|---|---|
| *Reke tũke hakuhĩ* | |
| *Nitũĩ twĩ mahĩtia* | *enhe!* |
| *No mugituiguĩre tha* | *enhe!* |

*Twoka twĩnyihĩtie* *enhe!*

*Tũnyenyane wega kanyanya* *enhe!*

*Andũ matwona moragie twendanĩire kũ*

(*b*) *ndũgĩũke hakuhĩ* *enhe!*

*Gĩũke hakuhĩ* *enhe!*

*Nĩkĩo tũnyenyane* *enhe*

*Nauge nĩwega* *enhe!*

*Ngũkũira nĩwega* *enhe*

*Na rũciu no ngoka .... Twendane aai*

**Tafsiri ya wimbo huo katika lugha ya Kiswahili.**

| | Fanani | Washiriki |
|---|---|---|
| (a) | Jua huku ndiko kwanileta | karibuni! |
| | Mwenyewe alikuwa mwanambee | karibuni! |
| | Karibuni na ufikapo kwa Kiragu | keti chini. |

(b) (i) Nakataa kuvumilia miguu nakataa

Tumekataa

tumekataa

Kukujiwa saa sita

Tufikapo kanisani

Misa imeshakamilika. (*kiitikio*)

(ii) Umechelewa nami nimefanya kwa matendo nakataa!

(iii) Ni kitoto kile chetu nakataa!

(iv) Ni makosa mmenyaza na si vizuri tumekataa!

(a) Tupendane aai

Tupendane aai
Watu wakituona
Wajiulize tulipendania wapi.

Hebu tuje karibu — enhe!
Tumejua tuna makosa — enhe!
Twaomba mtuwie radhi — enhe!
Twaja kwa unyenyevu — enhe!
Tunong'onezane vizuri ma'mkwe
Watu wakituona wajiulize tulipendania wapi.

(b) Basi njoo karibu — enhe!
Njoo karibu — ehne!
Ndivyo tunong'onezane — enhe!
Useme ni ahsante — enhe!
Nakwambia ahsante — ehne!
Na kesho nitakuja — ehne!

## KIAMBATISHO II

**Wimbo Katika Awamu ya Kuungamanisha Bwana na Bibi Harusi**

Fanani hutanguliza huku washiriki wakiitikia na kukariri kiitikio.

| **Fanani** | **Washiriki** |
|---|---|
| *Gikeno twĩnakĩo* | *Reke ngũtembeiye* |
| *Gũkũ wĩ *Gathigia* | *Reke ngũtembeiye* |
| *Nĩtwongerereka* | *Reke ngũtembeiye* |

*Reke ngũtembeiye *Wahĩto ooii*
*Ũmenye kĩndũ no mwene*
*Reke ngũtembeiye mũhiki ooii*
*Ũmenye kĩndũ no mwene.(kiitikio: mara mbili)*

| | |
|---|---|
| *Karibu ũingĩre* | *Reke ngũtembeiye* |
| *Nĩwoka rĩngĩ ii* | *Reke ngũtembeiye* |
| *Mũthenya ni waku ii* | *Reke ngũtembeiye.* |

*Gũkũ ni kwaũ?*
*Gũkũ ni kwaũ?*
*Ndenda gwĩtemania*
*Ndĩtemanie Aaaĩ*
*Aaaĩ aaiya Aaaĩ aaiya Aĩ*
*Aaaĩ aaiya.*

*Gũkũ nĩ gwitũ*
*Gũkũ nĩ gwitũ*
*Wenda gwĩtemania*
*Wĩtemanie ta njaũ ya mbogo. Aaaĩ*
*Aaaĩ aaiya Aaaĩ aaiya Aĩ*
*Aaaĩ aaiya.*

**Wahito gĩũke*

*Wahito gĩũke*

*Warerirwo na iria na nyama*

*Aaaĩ aaiya Aaaĩ aaiya Aĩ*

*Aaaĩ aaiya*

*Agũrirwo goro*

*Agũrirwo goro*

*Na mbũri na ng'ombe*

*Aaaĩ aaiya Aaaĩ aaiya Aĩ*

*Aaaĩ aaiya*

*Matiri ngemi*

*Matiri ngemi*

*Ngemi ciao no makiria nyama*

*Aaaĩ aaiya Aaaĩ aaiya Aĩ*

*Aaaĩ aaiya*

(**Wahito* – linaweza kuwa jina lolote la msichana kutegemea na jina la anayeolewa).

**Tafsiri katika Kiswahili**

| Fanani | Washiriki |
|---|---|
| Furaha tunayo | Hebu nikutembeze |
| Huku u *Gathigia | Hebu nikutembeze |
| Tumeongezeka | Hebu nikutembeze |

Hebu nikutembeze *Wahito ooii
Ujue kitu kina mwenyewe
Hebu nikutembeze Bi. Harusi ooii
Ujue kitu kina mwenyewe. (kiitikio)

| | |
|---|---|
| Karibu uingie | Hebu nikutembeze |

Umekuja tena                Hebu nikutembeze

Siku ni yako hii            Hebu nikutembeze.

*Huku ni kwa nani?*
*Huku ni kwa nani?*
*Nikitaka kujibwaga*
*Nijibwage, Aaai*
*Aaai aaiya Aaai aaiya Ai*
*Aaai aaiya.*

*Huku ni kwetu*
*Huku ni kwetu*
*Ukitaka kujibwaga*
*Ujibwage kama ndama wa nyati*
*Aaai aaiya Aaai aaiya Ai*
*Aaai aaiya.*

**Wahito kuja*
*Wahito kuja*
*Ulilelewa kwa maziwa na nyama*
*Aaai aaiya Aaai aaiya Ai*
*Aaai aaiya.*

*Alinunuliwa kwa bei ghali*
*Alinunuliwa kwa bei ghali*
*Kwa mbuzi na ng'ombe*
*Aaai aaiya Aaai aaiya Ai*
*Aaai aaiya.*

*Hawana kemi*
*Hawana kemi*

*Kemi zao ni wanapokula nyama*

*Aaai aaiya Aaai aaiya Ai*

*Aaai aaiya (tafsiri yangu)*

(**Waithera* – linaweza kuwa jina lolote la msichana kutegemea na jina la anayeolewa).

## KIAMBATISHO III

**Wimbo Katika Awamu ya Kusherehekea Bw. na Bi. Harusi Kufanya Ndoa.**

**Fanani anatanguliza huku washiriki waimbaji wakiitikia.**

*Ici cia Gathigia* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*Nĩ kanyu wĩciarĩire ĩĩ* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*Mũkĩhũre thaluti ĩĩ* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*

*Ici cia Gathigia* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
**Mũtugi niurona ĩĩ* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*Ukĩhũrĩrwo thaluti ĩĩ?* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*Nĩ aciari anyu ĩĩ* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*Mũteveva guteveva ĩĩ* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*

*Ici cia Gathigia* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*Gĩkeno twĩnakio ĩĩ* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*Mũtugi ni wega ĩĩ* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*Nikũrehe mũkami ĩĩ* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*Mũtui kahua ĩĩ* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*Mũti-ucu niegwĩkĩra ĩĩ* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*Mwathani ni mwega ĩĩ* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*Twathiĩ kwa njoherio ĩĩ..* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*
*twaceria mũtweji ĩĩ ?* — *ĩĩ aaĩĩ ikinyaga ta majeshi ĩĩ*

**Tafsiri katika Kiswahili**

Hawa wa Gathigia — ee ae hukanyaga ja majeshi e
Ni wenu mmejizalia e — ee ae hukanyaga ja majeshi e
Basi pigeni saluti e — ee ae hukanyaga ja majeshi e

Hawa wa Gathigia — ee ae hukanyaga ja majeshi e
*Mutugi unaona e — ee ae hukanyaga ja majeshi e
Ukipigiwa saluti e? — ee ae hukanyaga ja majeshi e

| | |
|---|---|
| Na wazazi wenu e | ee ae hukanyaga ja majeshi e |
| Mjishaue kujishaua e | ee ae hukanyaga ja majeshi e |

| | |
|---|---|
| Hawa wa Gathigia | ee ae hukanyaga ja majeshi e |
| Furaha tunayo e | ee ae hukanyaga ja majeshi e |
| Mutugi ahsante e | ee ae hukanyaga ja majeshi e |
| Kwa kuleta mkamuaji e | ee ae hukanyaga ja majeshi e |
| Mchumaji kahawa e | ee ae hukanyaga ja majeshi e |
| Mpini anatia e | ee ae hukanyaga ja majeshi e |
| Mungu ni mwema e | ee ae hukanyaga ja majeshi e |
| Tukienda kwa mkunga e | ee ae hukanyaga ja majeshi e |
| twatafuta mnyoaji e? | ee ae hukanyaga ja majeshi e |

## KIAMBATISHO IV

**Wimbo Katika Awamu ya Kutoa Ushauri Kwa Bw. na Bi. Harusi.**

*Nake Ngai agicũthĩrĩria akĩona*
*Arĩ igũrũ*
*Ti wega mũndũ aikarage ewiki*
*Ena ihoru*
*Akimũmbĩra mũndũ amũteithagie*
*Mũndũ mwega*
*Maganĩrĩirwo nake matũranie*

*Mũthuri ngatha*
*Nĩamenyagĩrĩra mũka wake*
*Akamũhumba wega agathakara*
*Akagema*
*Akamũhũnia wega agatunguha*
*Akanyoroka*
*Ndangĩmũtiga athiĩ agacarie ũngĩ. (kiitikio)*

*Rĩrĩa weciririe nĩ ũkũhikania*
*Ugie mũciĩ*
*Nĩ kurĩ na airitu aingĩ watigire*
*Vũrũriinĩ*
*Ndwacũthĩrĩirie ũkĩona ũngĩ mwega*
*Kũmũkĩra*
*ũyũ nĩwe wombiro nĩũndũ waku.*

*Wona mũka wene mũhumbe wega*
*Agathakara*
*Ndũkamwĩrĩrĩrie thiĩ ũhumbe waku*
*Athakare.*
*Nĩguo maitho maku maiganire*

*Magacire*
*Uhingie mwĩhĩto na irĩkanĩro.*

**Tafsiri Katika Kiswahili.**

Naye Mungu alichungulia akaona
Akiwa juu
Si vizuri mtu aishi peke yake
Kwa upweke
Akamuumbia mtu awe msaidizi
Mtu mzuri
Anayefaana naye waishi pamoja

Mume mwadilifu
Humchunga mke wake
Akamvalisha vyema akarembeka
Akang'aa
Akamshibisha vyema akawanda
Akanyooka
Hawezi kumwacha akatafute mwingine. (*kiitikio)*

Wakati ulifikiria utaoa
Upate nyumba
Kuna wasichana wengi aliacha
Duniani.
Hukuchungulia ukaona mwingine mzuri
Kumshinda
Huyu ndiye aliuumbwa kwa ajiri yako.

Ukiona mke wa mwenzio aliyevishwa vyema
Akarembeka

Usimtamani nenda uvishe wako
Arembeke
Ndiyo macho yako yatosheke
Yanawiri
Utimize kiapo na ahadi.

## KIAMBATISHO V

**Wimbo Katika Awamu ya Kutoa Zawadi Kwa Bw. na Bi. Harusi.**

Fanani anaongoza kuimba wimbo wenyewe huku washiriki wenzake wakiitikia baada yake.

| **Fanani** | **Washiriki** |
|---|---|
| *Nĩtwakumagaria* | *gwata ndaĭ* |
| *ũngĩgoka mũciĩ ĭ* | *gwata ndaĭ* |
| *Wero ũgakome rungu ĭ* | *gwata ndaĭ* |

*Gwata ndaĭ*
*Gwata ndaĭ*
*Kũgwata*
*Gwata ndaĭ (kiitikio)*

| | |
|---|---|
| *Gĩtanda nĩkĩo gikĭ* | *gwata ndaĭ* |
| *Rĩu nĩtwakũnengera* | *gwata ndaĭ* |
| *ũnyitie mũthuri ĭ* | *gwata ndaĭ* |

| | |
|---|---|
| *Ndakanaigue heho i* | *gwata ndai* |
| *Murathimo muno i* | *gwata ndai* |
| *Tuhii na tuiritu i* | *gwata ndai* |

**Tafsiri katika Kiswahili.**

| **Fanani** | **Washiriki** |
|---|---|
| Tumekusindikiza | kitendawili tega |
| Ukakuja nyumbani | kitendawili tega |
| Uambiwe ukalale mvunguni | kitendawili tega |

Kitendawili tega
Kitendawili tega
Tega

Kitendawili tega *(kiitikio)*

| | |
|---|---|
| Kitanda ndicho hiki | Kitendawili tega |
| Sasa tumekupatia | Kitendawili tega |
| Ufungate mumeo | Kitendawili tega |
| | |
| Asihisi baridi | Kitendawili tega |
| Mbarikiwe sana | Kitendawili tega |
| Kwa wavulana na wasichana | Kitendawili tega |

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY